**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha NNE – Tarehe 19 Juni, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mbele yetu tunao wageni mbalimbali wakiwemo wageni wa Mheshimiwa Spika, ambao ni ujumbe wa Waheshimiwa Madiwani wa Wilaya ya Urambo pamoja na Maofisa waliofuatana nao ukiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo. Karibuni sana. (*Makofi*)

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:**

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 na mwelekeo wa Mpango wa Mendeleo kwa mwaka 2006/2007.

**MHE. KABWE Z. ZITTO - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI, MIPANGO UCHUMI NA UWEZESHAJI:**

Taarifa ya Waziri Kivuli wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Taarifa ya Waziri Kizuri wa Fedha kuhusu hali ya Uchumi wa Taifa na mapendekezo ya muda wa kati na mfumo wa matumizi ya Serikali katika kipindi cha mwaka 2006/2007. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Viwango Tanzania kwa Mwaka 2003/2004. *(The Annual Report and Accounts of Tanzania Bureau of Standard for the Year 2003/2004).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 29

**Uboreshaji wa Barabara – Manispaa ya Musoma**

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Musoma umepewa hadhi ya kuwa Manispaa, na kwa kuwa Serikali inao utaratibu wa kuboresha kwanza Miji yenye hadhi ya Manispaa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami, ili barabara hizo ambazo nyingi ni mbovu ziendane na hadhi ya Manispaa zingine chini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini (Mbunge Viti Maalum) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Musoma ulipandishwa hadhi kuwa Manispaa mwaka wa fedha 2005/2006. Manispaa hiyo inazo aina mbalimbali za barabara zikiwemo zile zenye lami, changarawe na zile za udongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliagiza Miji yote iliyopandishwa hadhi kuwa Manispaa kufanya tathimini ya matengenezo ya barabara za kilomita nne kwa kiwango cha lami kwenye Halmashauri zao ikiwemo Halmashauri ya Manispaa ya Musoma. Katika kutekeleza maagizo haya Halmashauri hiyo imetayarisha mpango wake wa matengenezo ya barabara za Mkendo, Shabani, Sokoni, Kusaga na Indira Gandhi. Halmashauri hiyo imeshawasilisha makisio yake na yana jumla ya shilingi 1.6 bilioni katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo ya barabara za lami za Miji hasa Mji wa Musoma yatafanyika wakati Serikali itakapokuwa na uwezo wa kutekeleza mpango wake wa kuzipatia Halmashauri zote mpya za Manispaa angalau matengenezo ya kilomita 4 za lami. Mpango huu utatekelezwa tu pale uchumi wa nchi yetu utakapokuwa umetengemaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo barabara za Manispaa ya Musoma zitaendelea kuboreshwa kwa kutumia fedha za mfuko wa barabara za Halmashauri

zinazotolewa kila mwaka. Tunashukuru Halmashauri kuweka vipaumbele kwenye barabara mbovu ili ziweze kupitika wakati wote.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini bado nina swali moja la nyongeza kwa niaba ya wananchi wa Mara.

Wananchi wa Mkoa wa Mara wamekuwa wakitegemea sana barabara ziendazo kwenye Magati, sasa je, Serikali inaweza kutuahidi wananchi wa Mkoa wa Mara ni lini barabara muhimu kama ya Bunda – Mwibara na Kisorya itatengenezwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Serikali itatengeneza barabara katika sehemu alizozitaja Mheshimiwa Mbunge kulingana na fedha zitakavyopatikana.

Na. 30

**Ujenzi wa Madarasa na Nyumba za Walimu Geita**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Geita walihamasika na kuweza kujijengea majengo ya madarasa na Walimu kwa kiwango cha kuridhisha; na kwa kuwa malengo ya ujenzi huo kwa wananchi ilikuwa kufikisha kwenye lenta na Serikali imalize, hali ambayo haijafanyika mpaka sasa kwani kuna maboma zaidi ya mia nane (800);-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyamalizia majengo hayo?

(b) Kama Serikali inakuwa na kigugumizi na kauli zake; je, si vyema sasa wananchi waliosumbuliwa kujenga mabomba hayo watulie bila kufanya kazi zozote za kujitolea mpaka Serikali itakapomaliza maboma hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mabina, Mbunge wa Geita, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuwapongeza wananchi wa Wilaya ya Geita kwa kutambua umuhimu wa kuwapatia watoto wao elimu kwa kuboresha mazingira ya kutolea Elimu. Vilevile kwa kuona umuhimu wa kujenga nyumba za Walimu. Maendeleo ya wananchi yataletwa na wananchi wenyewe kwa

kutumia fursa na vikwazo vilivyopo katika maeneo yao kwa kutambua kuwa Serikali ni mshiriki wao katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukamilishaji wa majengo yaliyojengwa na wananchi katika Wilaya ya Geita yatakamilishwa kwa awamu kadri fedha zitakavyopatikana.

Kwa mwaka huu mwezi Februari, 2006 Serikali ilipeleka Sh.130,200,000/= kwa ajili ya madarasa 42, Sh. 93,600,000/= kwa ajili ya nyumba za Walimu 26 na Sh.12,600,000/= kutengeneza madawati 840 katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita na vivunge 462 vya Hisabati Sh.39,270,000/=. Serikali itakamilisha majengo hayo kwa awamu kulingana na Mpango wa Elimu ya Msingi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ni kushirikisha wananchi katika kufanya kazi za kujitolea na sio kuwasumbua. Hakuna mfadhili atakayekuja kutujengea au kutuletea maendekeo kama si sisi wenyewe kwa kushirikisha nguvu za wananchi. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kuwa Serikali imefanya mengi kabla Wilaya yake kuingia katika kutekeleza MMEM. Hivyo haina kigugumizi kuhusu kauli zake. Mafanikio ya MMEM yanatokana na kauli dhabiti za Serikali katika kuwaletea wananchi wake maendeleo. Hata hivyo, naomba kupitia Bunge lako Tukufu nitoe wito kuwa tuendelee kuwahamasisha wananchi kujenga madarasa na nyumba za walimu.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa maboma mengi ya Wilaya ya Geita mpaka sasa hivi bado hayaja kamilika na mpango ambao Naibu Waziri anasema kwamba tutaenda awamu kwa awamu.

Lakini ukiangalia kwamba sisi ni binadamu hatuagani na Mwenyezi, unakuta mvua inanyesha maboma ni yaliyojengwa na wananchi sasa hivi yanaendelea kubomoka. Je, Serikali inampango gani wa dharura wa kuweza kuyanusuru haya maboma ya wananchi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu ningependa kuongezea majibu kwa Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza imenisikitisha kusikia kwamba mvua ikinyesha maboma yatavunjika. Kwa sababu ni matumaini yangu na ya Serikali pia kwamba maboma yanayojengwa ni imara na kwa hiyo hayawezi kubomoka. Namwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuvuta subira Serikali itaongezea fedha Serikali kadri zinavyopatikana. (*Makofi*)

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wananchi wa Geita walihamasika wamejenga nyumba nyingi za walimu na madarasa hayo na kwa kuwa wanafunzi wengi sasa wameandikishwa shule za msingi. Je, Serikali sasa itatoa upendeleo wa pekee kwa Wilaya ya Geita kuwapa walimu wa kutosha maana yake walimu kule hakuna?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningemwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali sasa hivi inalifanyia kazi suala la upatikanaji wa walimu. Kwa hiyo ni suala ambalo linajulikana wazi na mikakati imeshawekwa ninachomwomba Mheshimiwa Mbunge ni subira.

Na. 31

**Uwiano wa Jinsia katika Fani za Sayansi na Teknolojia**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa juhudi kubwa inahitajika ili kuleta uwiano wa kijinsia hasa katika fani za Sayansi na Teknolojia:-

(a)Je, ni juhudi gani za makusudi zinazochukuliwa kuinua jinsia moja ya kike ili kwenda sambamba na nyingine katika Vyuo vyote?

(b)Je, tathimini zinaonyesha wastani wa wanaume na wanawake katika vyuo vyetu ukoje?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Niabu Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuendeleza jinsia zote katika Elimu ya Juu na hususani katika fani za Sayansi na Teknolojia, Vyuo Vikuu pamoja na Wizara yangu tayari zimekwisha kuchukua hatua za makusudi katika kuinua jinsia ya kike ili iende sambamba na ile ya kiume katika kujiunga na elimu ya Vyuo Vikuu. Hatua zilizochukuliwa ili kufikia azma hii ni pamoja na:-

(i) Wizara na Vyuo Vikuu vina utaratibu wa kuwatuma wanataaluma wake kutembelea shule za sekondari za wasichana na za mchanganyiko kwa lengo la kuwahamasisha wajiunge na Vyuo Vikuu na hususani katika masomo ya Sayansi na Teknolojia. Aidha, wasichana huhamasishwa kujiunga na Vyuo vya Elimu ya Ufundi.

(ii) Wizara na Vyuo Vikuu vimeanzisha mafunzo maalum *(Pre-Entry Programme for Female Science Students)* kwa ajili ya wanafunzi wa kike ambao hawakufikia kiwango cha kudahiliwa ambao hupewa mafunzo ya wiki sita wakisomeshwa masomo ya mchepuo waliosomea Kidatu cha tano na Sita na kisha kutahiniwa. Wanaofaulu katika mitihani hiyo hudahiliwa na kujiunga na masomo ya Chuo Kikuu. Kozi hizi huwasaidia wanafunzi wa kike kufikia kiwango kinachotakiwa ili kuwawezesha kupewa udahili.

Baadhi ya Vyuo vinavyoendesha mafunzo chini ya mpango huu ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*UDSM*), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (*SUA*), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*), Chuo cha Ufundi – Arusha, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia – Mbeya (*MIST*) na Vyuo Vikuu binafsi kama vile *Hubert Kairuki Memorial University – Dar es Salaam.*

(iii) Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia hutoa zawadi kila mwaka kwa wahitimu wa kike, wa kidato cha Nne, Kidato cha Sita na wa Vyuo Vikuu walioongoza katika kufaulu katika masomo ya Sayansi na/au fani za Sayansi na Teknolojia.

Aidha walimu wanaofundisha masomo ambayo mwanafunzi wa kike ameongoza katika hiyo shule naye hupewa zawadi na Wakuu wa Shule zilizofanya vizuri katika masomo ya Sayansi nao hupewa zawadi. Zawadi hizi zimekuwa ni changamoto kwa wanafunzi, Waalimu na Shule/Vyuo kushindana kitaaluma.

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la zawadi hizi ni kutoa motisha kwa wanafunzi wa kike kufanya vizuri katika masomo na kuwavutia wanafunzi wengine wa kike hupewa upendeleo maalum wa kudahiliwa katika Vyuo Vikuu pale ambapo kuna kulingana kwa alama za kufaulu baina ya wanafunzi wa kike na wanafunzi wa kiume.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hatua nilizozitaja, Wizara inaamini kuwa uwiano wa kijinsia usioridhisha katika fani za sayansi na teknolojia utatoweka.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na juhudi za makusudi zinazofanywa na Wizara, Vyuo Vikuu na vyuo vya Ufundi uwiano wa wanafunzi wa kike umeongezeka kutoka 23% mwaka 2000/2001 na kufikia 33.5 mwaka 2004/2005. Lengo ni kufikia 50% ifikapo mwaka 2010.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipatia nafasi hii kuuliza swali dogo la nyongeza. Tatizo kubwa alilosema Mheshimiwa Naibu Waziri kuna Tume ambayo inahamasisha jinsia ya wanawake kupenda masomo ya sayansi, lakini tatizo bado lipo katika vyuo vya ufndi kama alivyovitaja vya Arusha, Mbeya na baadhi ya vyuo vya *VETA.* Je, hatua gani ambayo itachukuliwa kwa maksudi kuhakikisha kuwa vyuo kama hivi vya ufundi wanawake wanaingia wengi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimwa Naibu Spika, nimesema sio Tume inayohamasisha ni wanataaluma. Maana yake walimu na wafanyakazi wa Wizara ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia kwa

makusudi hutembelea shule hizi na kuhamasisha, na kati ya mwaka 2003 na 2005 tumetembelea shule 33 vikiwemo vyuo vya ufundi. Kwa hiyo hili suala litaenda taratibu tunaomba na ninyi Wabunge muwahamasishe wasichana ili waweze kuchukua masomo ya sayansi hasa katika zile shule zenu ambazo maanzisha huko katika Kata.

Na. 32

**Vijana Wanaojiunga na Jeshi la Wananchi**

**MHE. BAHATI ALI ABEDI** aliuliza:-

Kwa kuwa vijana wetu wanaoujiunga na Jeshi la Wananchi huwa hawaruhusiwi kuoa au kuolewa mpaka wamalize miaka (3)

(a) Je, huo ni utaratibu tu au ni sheria ya Jeshi hilo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja sasa suala hili liangaliwe upya ili hii miaka ipunguzwe na vijana hawa waweze kuwa huru katika masuala ya ndoa kama haki yao ya msingi kwa binadamu?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wapya walioandikishwa katika majeshi ya ulinzi hawaruhusiwi kuoa au kuolewa mpaka wamalize miaka mitano ya utumishi tangu tarehe ya kuandikishwa katika majeshi ya ulinzi na si miaka mitatu (3) kama maelezo ya utangulizi katika swali la msingi.Baharti hilo lipo kwa mujibu wa sheria na kanuni za majeshi ya ulinzi kama ifuatavyo:-

(1)Aya 1.23 (1) ya kanuni za Majeshi ya Ulinzi, Juzuu ya kwanza (utangulizi) inampa mamlaka Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, kutunga au kutoa amri (*orders*) na au maelekezo (*instructions*) kwa majeshi ya Ulinzi ili mradi amri au maelekezo hayo yasipingane na sheria ya ulinzi wa taifa, kanuni za majeshi ya ulinzi, amri au maelekezo yoyote yaliyotolewa awali na Waziri wa Ulinzi  Kwa kuzingatia aya hiyo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, mnamo tarehe 24 Machi, 1992 alitoa amri nambari 6 yenye kichwa cha maneno Sera ya maendeleo ya Utumishi kwa askari *(Career Development Policy for Men)*. Sera hiyo, ndiyo inayoelekeza kila anachopaswa afisa au askari kufanya au kutokufanya katika kipindi kilichoamuliwa.Baada ya kutoa maelezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bahati, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Amri ya kutoruhusiwa kuoa/kuolewa kwa askari wapya hadi baada ya miaka mitano ya utumishi wake katika Jeshi ni taratibu za kijeshi (*forces routine order*) na ni sehemu ya sheria ya Ulinzi wa Taifa, Na. 24 ya mwaka 1966.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kila aina ya kazi ina masharti ya ajira/utumishi kulingana na asili (*nature*) na desturi za kazi hiyo katika jamii ya kazi husika. Sharti la kutoruhusiwa kuoa/kuolewa kwa askari wapya hadi baada ya muda wa miaka mitano ya utumishi katika majeshi ya ulinzi linazingatia mahitajio ya kisera, nidhamu ya kijeshi, sheria, kanuni na asili (*nature*) ya utumishi katika majeshi ya ulinzi pamoja na mila na desturi za jamii ya majeshi kote ulimwenguni. Katika kuweka kipindi hicho cha ukapera, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi alizingatia vigezo mbalimbali vinavyohusiana na mambo yaliyotajwa hapo juu. Kipindi cha miaka mitano bado kinakidhi matarajio ya kiutendaji kijeshi na hakiingiliani kwa vyovyote vile na ukiukwaji wa haki yoyote ya msingi kwa askari hao. Vijana wetu wanajiunga na jeshi wakiwa na umri kati ya miaka 18 hadi 23. Umri ambao wanahitajika kujenga Taifa zaidi na kujijenga wao wenyewe kabla ya kufikiria kuoa au kuolewa.(*Makofi*)

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa taratibu hizi au sheria hizi ziliwekwa siku nyingi kabla hatujashuhudia janga la UKIMWI na kwa kuwa mojawapo ya njia za kujilinda na UKIMWI ni watu kuwa waaminifu katika ndoa zao na hasa watu katika ndoa.

Je, haoni sasa ni wakati muafaka wa kurekebisha taratibu na sheria hizo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge nadhani atakubaliana nami kwamba takwimu zinaonyesha kwamba ni kweli vijana wengi ndiyo wanaoathirika na tatizo la UKIMWI. Lakini vyama hizo hizo zinaeleza kwamba vijana wengi ambao walioko katika ndoa ndiyo wameathirika zaidi na tatizo la UKIMWI. Kwa maana hiyo haitakuwa busara kwa vijana wa kiaskari kuwaingiza katika ndoa wakiwa katika umri mdogo.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa suala linalozungumzwa hapa kwenye swali la mwanzo ni kuoa au kuolewa. Je, endapo askari wa kike atapata mamba kabla ya wakati uliowekwa na hajaolewa. Jeshi linampa adhabu gani?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za jeshi zinakataza askari yeyote kuolewa au kuoa au kishika mimba kabla ya miaka mitano. Kwa maana hiyo kama itatokea hiyo itampasa askari huyo aache kazi.

Na. 33

## Hifadhi ya Lukwika – Nanyumbu

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA** aliuliza:-

Kwa kuwa Hifadhi ya Lukwika iliyopo Nanyumbu ina wanyama wengi wa kuvutia Watalii wa ndani na nje ya nchi hali inayoweza kuingizia nchi fedha na kuongeza pato la Taifa:-

(a) Je, kwa nini Serikali haiitangazi Hifadhi hiyo kama inavyofanya kwa Hifadhi nyingine hapa nchini ili iweze kuvutia Watalii wawindaji?

(b) Je, vijiji vinavyoizunguka Hifadhi hiyo vinafaidika vipi na kuwepo kwa Hifadhi hiyo na ni lini mipaka itawekwa kwenye vijiji vinavyopakana na Hifadhi hiyo ili kuzuia migogoro na uwindaji haramu?

(c) Je, wanyama wanapoharibu mashamba ya wanakijiji, kwa nini huwa hakuna fidia, na kama ipo inachelewa sana?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Eneo la Uhifadhi la Lukwika linatambulika kama Pori la Akiba ambalo kisheria hadhi yake ya uhifadhi ni tofauti na Hifadhi za Taifa. Hivyo, kulingana na Sheria ya Hifadhi ya Wanyama Pori ya mwaka 1974, hivi sasa matumizi ya pori hilo ni ya shughuli za Uwindaji wa Kitalii. Katika kitalu cha uwindaji wa kitalii, Pori la akiba la Lukwika limegawiwa kwa Kampuni ya *Miombo Safaris Ltd*. Hivyo, licha ya Wizara yangu kushiriki katika kuendeleza na kutangaza vivutio vya utalii kwenye Ukanda wa Kusini *(Southern Circut)*likiwemo suala la uwindaji wa kitalii kwenye nchi mbalimbali duniani, Kampuni ya *Miombo Safaris Ltd*. pia imekuwa ikiuza safari za uwindaji kwa kutangaza aina ya wanyama wanaopatikana katika maeneo inakowinda likiwemo pori la akiba la Lukwika. Aidha, Wizara kupitia Idara ya Wanyama Pori inaandaa vipeperushi na vijarida vya kutangaza mapori ya akiba yanayotumika katika utalii wa uwindaji na ule wa picha. Pori la Akiba la Lukwika ni miongoni mwa mapori ya kwanza yaliyomo kwenye mpango huo.

(b) Mheshimiwa Spika, wananchi waishio jirani na Pori la Akiba la Lukwika wamekuwa wakinufaika na Pori hilo kwa namna mbali mbali kama ifuatavyo:-

- Kampuni ya *Miombo Safaris Ltd*. imetoa michango mbali mbali kwenye shughuli za maendeleo, kwa mfano kati ya mwaka 2001 – 2005 jumla ya Tshs. 44,928,857 zilitolewa.

- Halmashauri ya Wilaya ilipata asilimia 25% ya mapatao yatokanayo na uwindaji wa kitalii ambayo ni shilingi 8,665,402.

- Mwaka 2002 mifuko 600 ya dawa ya kuua wadudu wanaoshambulia zao la korosho aina ya *Sulphur* yenye thamani ya Tshs. 5,400,000 ilitolewa na Kampuni ya *Miombo Safaris Ltd*. kwa wananchi wa Vijiji 8.

- Mwaka 2003 jumla ya Tani 10 za chakula zilitolewa kwa wananchi wa vijiji 6. Aidha, mwaka 2004 magunia 160 ya mahindi yalitolewa na Kampuni ya *Miombo Safaris Ltd*. kwa wananchi wa vijiji 4 kwa ajili ya kupunguza makali ya njaa.

- Vile vile ajira hutolewa kutokana na uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mipaka, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Pori la Akiba la Lukwika linasimamiwa kwa pamoja na Pori la Akiba la Masanjesi. Hivyo, mipaka yenye urefu wa kilomita 36 katika Pori la Akiba la Lukwika na KilomIta 42 katika Pori la Akiba la Masanjesi imetambuliwa na kufyekwa upana wa mita 10. Mbali ya kufyekwa, mipaka hiyo pia imewekewa alama za vibao vinavyoonekana wazi wazi. Kwa kuzingatia maelezo haya, suala la mipaka haliwezi kuwa sababu ya uwezekano wa kuwepo kwa migogoro au uwindaji haramu katika pori hili.

(c) Kulingana na Sheria na Sera ya Wanyamapori, suala la kulipa fidia kwa mazao na mali nyingine zinazoharibiwa na wanyamapori halipo. Hali hii inatokana na ugumu wa utekelezaji wake hususan katika kuzingatia mtawanyiko wa maeneo ya wanyamapori, mfumo wa makazi ya wanavijiji ambao katika maeneo mengi vijiji na mashamba vimezungukwa na mapori. Hivyo, kutokana na mazingira haya, hivi sasa utaratibu unaotumika ni Wizara yangu kuchangia kupunguza athari za uharibifu unaosababishwa na wanyamapori kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya katika kuchukua hatua mbali mbali. Hatua hizo ni pamoja na kuwaua wanyama wanaobainika kusababisha hatari na kuwaelimisha wanavijiji kuhusu jinsi ya kukabiliana na wanyamapori waharibifu na pia kubaini mbinu nyingine za kuokoa mazao na mali yao.

**NAIBU SPIKA:** Swali la nyongeza, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa!

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Tembo ambao wanaonekana kwamba wamezaliana sana katika Hifadhi hii ya Lukwika, wamefanya uharibifu mkubwa kwenye mashamba na pia wameua watu. Je, Serikali itawapa chakula cha msaada hawa walioathirika na kuwalipa fidia hawa ambao wamekufa? Swali la pili, wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu wamemwomba Waziri au Naibu Waziri atembelee Wilayani kwetu. Je, mwaliko huu umekubaliwa? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba niwape pole wananchi wa Nanyumbu ambao wamepata uharibifu wa mali zao na wengine kuuwawa na Tembo. Katika Sheria ya Wanyamapori, kinachotolewa kwa watu ambao wameuwawa na wanyamapori ni kifuta jasho cha shilingi 50,000/=. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane, tupate majina

ya wale ambao wameuwawa na tembo hao ili Wizara iweze kuwalipa kifuta jasho. *S*wali la pili la Mheshimiwa Mbunge kuhusu mwaliko; Kusema kweli kazi yetu ni kutembelea maeneo yote ambayo yanahusika na Wizara yetu ikiwapo pamoja na pori la Lukwika. Hivyo basi, kwa kuwa umetoa mwaliko, mimi ninaahidi nitakuja huko tukiongozana na wewe. Kwa hiyo tutaongozana na Mheshimiwa Mbunge na vile vile ingekuwa vema tukawape pole wale ambao wamefiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Swali hili limechukua dakika kumi na sisi huwa tunatumia dakika tano. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa *Col*. Feteh Saad Mgeni, kwa ajili swali lingine!

Na. 34

**Maafa Yaliyotokea Katika Mlima Kilimanjaro 2006**

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa mwezi Januari mwaka 2006 baadhi ya mawe katika Mlima Kilimanjaro yaliporomoka na kusababisha maafa kwa baadhi ya Watalii wa kigeni na Watanzania ambao walikuwa wakipanda Mlima huo; na kwa kuwa Mlima huo ni kivutio kikuu cha barabara ya utalii hivyo kutuingizia fedha nyingi za kigeni:- Je, Serikali imejizatiti vipi kuhakikisha kuwa maafa kama hayo hayatokei ili tusije poteza biashara hii muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:- Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Col. Feteh Saad Mgeni, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Mwezi Januari 2006, kulitokea ajali iliyosababisha vifo vya watalii watatu raia wa Marekani na majeruhi watano akiwemo Mtanzania mmoja ambaye alikatwa mguu. Ajali hiyo ilitokana na mawe yaliyoporomoka kutoka katika kingo za kilele cha Mlima Kilimanjaro. Mara baada ya kupokea taarifa za ajali hiyo, uongozi wa Hifadhi za Taifa ulipeleka Askari wa uokoaji katika eneo la tukio pamoja na magari mawali ya kubeba wagonjwa. Majeruhi wote walichukuliwa na kupelekwa katika Hospitali ya *KCMC* Mjini Moshi kwa matibabu. Baadaye majeruhi wawili kati yao walichukuliwa na kusafirishwa kwa Helikopta hadi Nairobi kwa matibabu zaidi. Maiti zilitafutwa na kupatikana kisha kusafirishwa kwenda Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya tukio hilo, Wizara yangu kupitia Shirika lake la Hifadhi za Taifa, ilifunga njia iliyohusika na ajali ili kuruhusu kufanyika kwa uchunguzi zaidi kuhusu chanzo cha ajali hiyo. Shirika la Hifadhi za Taifa na Kampuni ya Kitalii ya *African Environment* kwa nyakati tofauti walifanya uchunguzi. Matokeo ya uchunguzi yalibaini kuwa bado kuna majabali juu ya mlima yanayoweza kuanguka wakati wowote. Hivyo, eneo lililohusika na ajali ni hatari kwa wapanda mlima na kuonya kuwa ajali zaidi zingeweza kutokea tena muda wowote. Hivyo, walishauri hatua kadhaa za kuchukuliwa iwapo njia hiyo itabidi kufunguliwa. Hatua hizo ni kama zifuatazo:-

•Kuchepusha njia hiyo kwa lengo la kupunguza muda ambao mgeni atapita katika eneo la hatari.

•Wakati wa baridi majabali kwenye eneo husika yanakuwa na sura ya kushikamanishwa na barafu . Hivyo, wapandaji wanapaswa kuanza safari mapema asubuhi kabla jua halijachomoza ili kukwepa muda ambao kuna uwezekano mkubwa wa maporomoko ya mawe.

•Uchunguzi wa kina na wa kitaalam kuhusu ajali hiyo umekwishaanza ukiongozwa na Mtaalam wa Masuala ya Milima.

**NAIBU SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni!

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ndogo ya kuongezea swali moja au ushauri. Kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kanipa majibu mazuri yanayoridhisha. Lakini, naomba kumshauri kwamba inaonekana Mheshimiwa Waziri kwamba uharibifu wa Mazingira unachangia masuala haya. Je, Mheshimiwa Waziri ataweza kutusaidia au kuisaidia jamii katika kuelimisha elimu ya mazingira kwa manufaa ya taifa hili?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wake ni sahihi kwamba uharibifu wa mazingira nao pia unachangia katika kuleta maafa. Kwa hiyo, ushauri huo tumeuchukua na tutatoa elimu hiyo ambayo ninaamini mpaka sasa inatolewa. Lakini tutaendelea kuitoa elimu hiyo ya mazingira.

Na. 35

**Mahitaji ya Umeme Vijijini**

**MHE. WILSON M. MASILINGI (k.n.y. MHE. EUSTACE O. KATAGIRA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Karagwe ina huduma ya Umeme wa *TANESCO* katika Makao Makuu ya Wilaya na maeneo ya karibu na Makao hayo:-

Je, ni lini vijiji vya Wilaya ya Karagwe vitapatiwa umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:- Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mbunge wa Kwera, kama ifuatavyo:-

Ni kweli Wizara ya Nishati na Madini kupitia *TANESCO*, imekwisha peleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe na maeneo ya karibu na Makao Makuu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itavipatia umeme vijiji vya Wilaya ya Karagwe baada ya kukamilisha upembuzi yakinifu unaotarajiwa kukamilika mwezi Juni 2006 na baada ya kukamilishwa taratibu za kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi kwa msaada wa Serikali ya Sweden chini ya Shirika lake la maendeleo la *SIDA*. Maeneo ambayo yamelengwa kupewa umeme jimboni Karagwe kupitia mpango huu ni Nyaishozi, Ihembe, Nyakanyanja na Bisheshe, Nyabwegira, Lukaka, Lunyanga, Kakiro, Rushe, Katembe, Kituntu, Rwambaizi na Nakainga.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, kijiji cha Kasheshe katika Wilaya hiyo ya Karagwe kina umuhimu wa kihistoria katika Wilaya ya Karagwe; Na kwa kuwa, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amejitahidi kueleza jitihada kubwa na nzuri za Serikali ambazo zinastahili kupongezwa kutafuta msaada kutoka *SIDA* ambayo ina uwezo mkubwa wa kifedha. Je, Bisheshe kijiji ambacho ni maarufu kihistoria, kitapewa umuhimu wa kipekee kupata umeme na hivyo iwe rahisi kupeleka umeme huo mpaka kijiji cha Kashanda?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imesikia ombi la Mheshimiwa Wilson M. Masilingi na itaangalia kufuatana na uwezekanao wa kuingiza kwenye mradi huu. Ningeomba kwamba baada ya kipindi hiki cha Bunge tuwasiliane na Mheshimiwa Mbunge kuangalia uwezekano wa kuingiza kijiji hicho kwenye mpango wa kupeleka umeme katika Wilaya ya Karagwe.

Na. 36

**Kampuni Ya Kuhakiki Takwimu Za Sekta Ya Uchimbaji Madini Nchini**

**MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH (K.n. y. MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** aliuliza:- Kwa kuwa wakati wa kupitia upya mikataba ya uchimbaji madini nchini, Serikali iliajiri Kampuni ya kiuhakiki takwimu ili kupata ukweli juu ya Sekta ya uchimbaji madini nchini *Assayers*.

(a) Je, Kampuni hiyo imechukua muda gani kufanya kazi hiyo mpaka sasa, na kama bado itachukua muda gani zaidi?

(b) Je, Kampuni hiyo imegundua nini hadi sasa?

(c) Kulingana na mkataba, Kampuni hiyo italipwa fedha kiasi gani na kiasi gani kimeishalipwa mpaka sasa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:**-** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Alex Stewart* iliingia mkataba wa miaka miwili na Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Tanzania kuanzia tarehe 14 Juni, 2003 kwa ajili ya kuhakiki gharama za uzalishaji, usafirishaji wa dhahabu pamoja na uwekezaji na uendeshaji migodi mikubwa nchini. Mkataba huo uliisha muda wake tarehe 13 Juni, 2005. *(Makofi)*

Hata hivyo Mkataba huo uliongezewa muda kwa miaka mingine miwili kuanzia tarehe 28 Mei, 2005 hadi tarehe 27 Mei, 2007 kwa masharti yale yale. Mpaka sasa, Kampuni hiyo imechukua muda wa miaka takriban mitatu kufanya kazi ya kuhakiki uzalishaji, usafirishaji dhahabu na uendeshaji wa migodi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Kampuni ya *Alex Stewart* imebaini kuwa taarifa za Makampuni makubwa ya uchimbaji wa dhahabu zinazohusu gharama za uzalishaji na usafirishaji madini hayo nje ya nchi haziko sahihi. Kampuni hiyo bado inaendelea kufanya ukaguzi wa gharama za uwekezaji na uendeshaji wa migodi hiyo kwa lengo la kubaini matumizi halisi ya migodi hiyo ili kuhakikisha makampuni hayo yanalipa kodi kwa mujibu wa sheria. Ni matumaini ya Serikali kuwa taarifa itakayowasilishwa serikalini na Kampuni hiyo kuhusiana na gharama halisi za uendeshaji na uwekezaji wa migodi husika itasaidia kubaini ni lini na kiasi gani cha kodi makampuni hayo yatatakiwa kulipa.

(c)Ada za ukaguzi *(audit fee)* hulipwa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha. Malipo hayo hufanywa kila mwezi baada ya Mkaguzi kuwasilisha *invoice* inayoonyesha ada ya ukaguzi. Tangu mkataba ulipoanza mwezi Julai 2003 hadi mwezi Mei 2006, jumla ya Dola za Marekani 30,915,642.80 zimelipwa kwa Mkaguzi kama ada ya ukaguzi.

**MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Ni kitu cha kawaida makampuni haya makubwa yanayochimba dhahabu kuuza hisa zake kwa makampuni mengine. Wanapouza hisa hizi, hivi utaratibu wetu wa kisheria nchini unasemaje, *transaction* hii inapofanyika iwe ndani ya nchi au nje ya nchi? Wanalipa kodi au hawalipi kodi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Suala la kulipa kodi kwenye mauzo ya hisa ya hizi kampuni, inategemeana na hizo kampuni zimeuza hisa kwa njia gani. Pale ambapo hisa zimeuzwa kutokana na kampuni ambazo ziko hapa hapa ndani ya nchi kutokana kwa mujibu wa sheria za nchi yetu, kodi kutokana na mauzo ya hisa inatakiwa kulipwa. Lakini, pale ambapo hisa ambazo zinauzwa ni hisa ambazo ziko kwenye kampuni ambazo ziko nje ya Tanzania, kutokana na sheria zetu kwa sasa hivi, mauzo ya hisa katika makampuni ambayo yako nje ya nchi, kodi kutokana na mauzo ya hisa hizo, haitakiwi kulipwa hapa nchini.

Na. 37

## Maendeleo ya Elimu Mkoa wa Rukwa

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwa mikoa iliyo nyuma kielimu katika Taifa letu; na kwa kuwa uchumi wa wananchi wake bado uko chini pamoja na kuwa wana uwezo mkubwa wa kuzalisha chakula cha ziada:-

(a) Je, isingekuwa vema Serikali ikatoa upendeleo maalum katika kugawa fedha za MMES wakati huu wa kujenga shule za Sekondari?

(b) Kwa kuwa kuna upungufu wa waalimu katika Mkoa wa Rukwa kila mwaka. Je, isingekuwa vyema walimu wanaohitimu Chuo cha Ualimu Kantalamba walio wengi wapangiwe Mkoa wa Rukwa?

(c) Je, ni nini hatma ya Mpango wa Wizara wa kutoa vivutio kwa walimu wanaopelekwa kwenye maeneo yenye hali ngumu ya maisha?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA)** alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua tofauti za kimaendeleo ya elimu nchini, fedha za MMES zinagawiwa kwakuzingatia vigezo vilivyowekwa vikiwemo vya mahitaji yaliyopo katika maeneo mbali mbali, idadi ya wanafunzi wanaojiunga kidato cha kwanza ikilinganishwa na wanafunzi waliomaliza Darasa la Saba katika eneo husika na pia Wilaya zilizo chini ya wastani wa asilimia iliyotarajiwa ya watakaoingia Sekondari Kitaifa *(Transition Rate)* ambayo kwa mwaka 2005 ilikuwa asilimia 35, kwa kutumia vigezo hivyo, Wilaya zilizo nyuma hunufaika zaidi.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwa mikoa ambayo ina upungufu mkubwa wa walimu. Vyuo vya ualimu ni vya kitaifa, hupokea wanachuo kutoka Mikoa yote na Wilaya zote. Ugawaji wa walimu wanaohitimu katika Vyuo hivyo huzingatia mahitaji ya kila Mkoa na hasa Mikoa yenye upungufu mkubwa wa walimu ukiwemo Mkoa wa Rukwa. Orodha ya majina ya wahitimu wanaopangwa katika kila mkoa hutumwa kwa Maafisa Elimu wa Mikoa ambao huwapangia vituo vya kazi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kulifanyia kazi suala la kutoa vivutio kwa walimu wanaopelekwa kwenye maeneo yenye hali ngumu ya maisha. Hata hivyo, njia bora zaidi ni kuweka mazingira ambayo yatasaidia walimu wanaopangwa katika kila mkoa kubaki na kufanya kazi na hasa ujenzi wa nyumba za walimu pamoja na kutatua kero zilizopo kwenye maeneo yao ya kazi.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

La kwanza, kwa kuwa, Serikali yetu ya Awamu ya Nne imeishatamka rasmi ya kwamba itatoa upendeleo maalum katika maeneo yote yale ambayo yako nyuma kimaendeleo na ambayo yako pembezoni. Je, katika kutekeleza ahadi hiyo, bajeti ya mwaka huu imefikiria na imeweka fedha maalum kwa kuweka vivutio kwa ajili ya walimu wa sehemu hizo? La pili, kwa kuwa, tuliona Serikali ina kigugumizi kidogo kuhusiana na kutoa motisha kwa walimu wanaoishi katika maeneo ambayo yana matatizo, sisi Mkoa wa Rukwa kwa kushirikiana na Wabunge wote na wananchi, tuliamua kuanza kuchanga fedha sisi wenyewe mpaka sasa zaidi ya shilingi 48 milioni tumetoa kwa walimu kutoa angalau motisha kwa walimu. Katika hali hiyo, Je, Serikali haioni ya kwamba kuna umuhimu wa kutuunga mkono katika jitihada hizo? Na kwa sababu ilikuwa imeahidi ya kwamba itasaidia. Je, kwa nini wasiturudishie milioni 48 tulizotoa kwa niaba ya...

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MWANTUMU BAKARI MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Napenda niseme kwamba Bajeti ya mwaka huu ya Wizara ya Elimu imetoa kipau mbele kwenye mambo muhimu na moja wapo ikiwa ni hilo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelizungumza.

(b) Kwanza, kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Serikali kuu, ninaomba kupongeza kwa dhati kabisa Wabunge wa Mkoa wa Rukwa kwa jitihada walizozifanya za kuhakikisaha kwamba wanawaandalia mazingira mazuri walimu watakaokwenda kwenye Mkoa wao. Aidha, naomba niseme, Serikali kwa jumla inafanyia kazi kwa dhati kabisa ili kuweza kutatua mazingira hayo magumu kisayansi. Mimi binafsi nimetembelea baadhi ya Mikoa na nimebaini mazingira magumu yanatofautiana mkoa mmoja na mwingine na ya kwamba si pesa tu inaweza ikabadilisha mazingira magumu, kunahitaji kazi ya ziada ambayo Serikali kuu inafanyia kazi.

Wizara yangu kwa kupitia mpango wa MMEM ilibuni mkakati wa dharura wa kutoa mafunzo kwa Daraja la Tatu “A” katika awamu mbili zilizogawanya mafunzo ya nadharia na yale ya vitendo yaani uzoefu kazini. Wakati wa mafunzo kwa vitendo walimu wanafunzi walipata ushauri wa kitaalam kwa lengo la kuwapatia ujuzi wa kazi yenyewe. Kwa kutumia mkakati huo malengo ya MMEM yalifanikiwa ya upatikanaji wa walimu 43,370 kati ya walimu waliohitajika 45,796 ambao ni asilimia 96 ya malengo. Serikali bado inafanyia kazi asilimia 4 iliyobaki ambao ni sawa sawa na walimu 2,426. Aidha tunaziomba Halmasharui nazo zizingatie ugawaji wa walimu kwa uwiano sawa katika maeneo yake yote.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali inawatumia walimu wastaafu kwa shule za Sekondari tu. Serikali kwa kupitia uongozi wa Mikoa inaendelea na maandalizi ya kuwapa mkataba wa miaka 2 walimu wastaafu 250 wa shule za Sekondari

mwaka 2006 kutokana na upungufu wa walimu katika shule za sekondari ikiwa ni moja ya mikakati ya kukabili upungufu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa walimu ni mkubwa zaidi hasa katika maeneo ya vijijini. Tunaomba Halmashauri na wananchi waendelee kujenga shule na nyumba za walimu, kuweka huduma muhimu na kujitahidi kutatua kero zilizopo ili kuwawezesha walimu kufundisha katika maeneo hayo.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inafikiria nini kuwatumia walimu wa MEMKWA ambao wamefanya kazi vizuri kuwaingiza katika mpango wa kuweza kusaidia kupunguza tatizo la walimu? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wanaosaidia katika mpango wa MEMKWA yaani elimu kwa waliokosa, siyo wote wenye vigezo vya kutosha kuingiza kwenye vituo vya ualimu kwa sababu kwa uzoefu tulionao wale si walimu bali ni watu wanaosaidia tu waliomaliza kidato cha nne.

Kwa hiyo, utakuta wengine hawana sifa za kuwawezesha kuingia katika chuo cha ualimu. Kwa mfano sasa wanaochukuliwa wa mwisho kabisa ni wale ambao daraja la nne *(Division Four)* ambao si zaidi ya pointi 28. Kwa hiyo, kama wapo wale ambao wana pointi si zaidi ya 28 wanaweza kuomba tu na sisi tukawapa nafasi ya kujiunga na vyuo vya ualimu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na bahati nzuri maswali yamekwisha. Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba tunapambana na muda kwa sababu mbili maswali ya nyongeza yanakuwa marefu na baadhi ya majibu yanakuwa marefu, nasema baadhi kwa sababu kuna *a lot of improvement* kwa kweli kwa upande wa majibu.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache, kwanza naomba Wabunge, wanaotaka kuchangia Hoja hizi na hoja zitakazokuja tunavyo vikaratasi maalum vya kuomba kuchangia, msiandike vikaratasi namna hii kwa sababu hivi si *official*. Hivyo ni *official* kwa mfano sasa wanaochangia katika hotuba hii ya fedha wamefika 85.

Sasa mnaweza kuendelea kuomba kwa sababu na Ofisi ya Waziri Mkuu tunaendelea nayo, mnaweza kuzungumza yote hayo. Lakini iwe katika *format* ya *official*. Namna hii mimi siwezi kumweka kwenye rekodi.

La pili wale wanaopokea vitambulisho kama vina matatizo vimeandikwa vibaya naomba mumpelekee Katibu. Pia napenda niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Uwezekaji na Biashara kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati leo Jumatatu tarehe 19Juni, 2006 saa 4.30 baada ya kipindi hiki cha maswali katika ukumbi Na. 133 ghorofa ya kwanza katika jengo la utawala.

## KAULI ZA MAWAZIRI

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge, ili kuharakisha maendeleo ya elimu ya Sekondari, Serikali ilianzisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) mwaka 2004. Serikali inaendelea na utekelezaji wa mpango huo ambao sasa umefikia mwaka wa tatu na mafanikio yake yameanza kuonekana. Wahitimu wa elimu ya msingi 243,359 kati ya 493,946 wamejiunga na Kidato cha Kwanza hadi 31 Machi, 2006. Waliojiunga na Kidato cha Kwanza ni sawa na asilimia 49.3

Mafanikio haya yamevuka lengo la asilimia 40 ya wahitimu wa elimu ya msingi ya kupata nafasi ya elimu ya sekondari mwaka huu wa 2006. Yote haya yamewezekana kutokana na msukumo wa Serikali na mwitikio wa wananchi, kwani asilimia 49.3 ya wanaojiunga na kidato cha kwanza iliyofikiwa mwaka huu ililengwa kufikiwa mwaka 2009 kulingana na malengo ya MMES ya mwaka 2004 hadi 2009. Haya ni mafanikio makubwa ya kujivunia. Aidha shule mpya za Sekondari za Serikali zimeongezeka katika kipindi cha miaka mitatu kama ifuatavyo:- Mwaka 2004 shule 184, mwaka 2005 shule 384 na mwaka huu wa 2006 shule 484. Ongezeko hili la shule 1050 ni sawa na asilimia 161 ikilinganishwa na shule zilizokuwepo mwaka 2003 yaani 649.

Baada ya ongezeko hili idadi ya shule za Serikali hadi tarehe 30 Mei, 2006 ni shule 1699. Serikali inawashukuru wananchi kwa kuitikia wito wa kuchangia katika jitahada za kuendeleza elimu ya Sekondari. Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi inamshukuru Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Wakuu wa Mikoa mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge na Wakuu wa Wilaya kwa ushiriki wao kwenye jitihada hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuyalinda na kuyaendeleza mafanikio haya yaliyofikiwa nchi yetu itahitaji walimu 9,500 mwaka huu wa 2006 ili kukidhi mahitaji ya walimu yaliyotokana na ongezeko la shule. Tayari tuna walimu wahitimu 3,207 kutoka katika vyuo vyetu vya ualimu vyenye kutoa stashahada ya ualimu na tunao pia wahitimu 500 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanaoandaliwa kuajiriwa. Kwa hiyo, bado upo upungufu wa walimu 5793.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia upungufu wa walimu tulionao Serikali imeandaa mkakati wa muda wa mfupi wa kupata walimu wa shule za sekondari za Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Kuendesha mafunzo maalum ya muda wa mwezi mmoja kuhusu mbinu za ufundishaji kwa ajili ya wahitimu 3500 wa kidato cha sita wenye ufaulu wa si chini ya daraja la tatu (*Division Three)*, Vyuo vya ualimu saba vya kanda vitahusika katika zoezi hili ambavyo ni Butimba, Mtwara, Morogoro, Monduli, Tabora, Tukuyu na Korogwe. Mafunzo haya yataanza tarehe 1 Julai, 2006. Lengo ni kuwapanga walimu hao katika vituo vya kazi ifikapo mwezi Agosti 2006. (*Makofi*)

(b)Kuwapa mkataba wa miaka miwili walimu wastaafu 250 ambao wana uzoefu wa kufundisha na wameonyesha utayari wa kufanya kazi.

(c)Kuajiri wahitimu 260 wa Vyuo Vikuu ambao hawajasomea ualimu na wameonyesha utayari wa kuajiriwa na baadaye kupatiwa mafunzo ya ualimu.Hizi ni hatua za dharura za kukabiliana na uhaba huu. Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 8 ili kukabiliana na dharura hii ya mafanikio. Aidha Serikali itaendelea kubuni mikakati mingine na kuendelea na mipango ya kutoa mafunzo ya ualimu kama moja ya majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio ya Serikali kuwa kwa kutekeleza mkakati huu tutakuwa tumepunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la upungufu wa walimu katika shule zetu za Serikali.Jambo moja muhimu tulilojifunza kutokana na mafanikio ya ujenzi wa shule za sekondari ni kwamba panapokuwa na uongozi mahiri na mwitikio wa wananchi kwa lengo mahususi Watanzania wanaweza kufanya maajabu kwa manufaa ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, wadau wa elimu na wananchi kwa jitihada zao za kujenga shule ikiwa ni pamoja na vyumba vya madaraja, vyoo na nyumba za walimu. Lakini napenda kusisitiza kwamba, lazima shule zinazojengwa ziwe na viwango vinavyokubalika, maana lengo letu si kutoa elimu tu bali ni kutoa elimu iliyo bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2005, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2006/2007

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nitoe maelezo ya kawaida katika mazungumzo ya namna hii. Kanuni yetu inasema baada ya Mawaziri wa Mipango na Fedha kutoa hotuba zao nitamwita Mwenyekiti wa Kamati, iliyoshughulikia Wizara ile. Sasa siku ya Alhamisi Spika, alieleza kwamba Msemaji wa Kamati, atakuwa na saa moja halafu atafuatiwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, nao pia watakuwa na saa moja watagawanyika katika sehemu mbili. Haipo kwenye Kanuni kuna mtu amenihoji lakini tuna uzoefu katika Bunge lililopita la Bajeti tulivyofanya hivi. Kwa hiyo, baada ya kusema hayo namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda. (*Makofi*)

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 43(5) (b) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kuhusu hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2005, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2006/2007.Kwanza niwapongeze Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji

Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, Mbunge na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji, Mbunge kwa Hotuba zao walizowasilisha Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaipongeza kwa dhati Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa Misingi ya Kiuchumi iliyokwishawekwa haikufumuliwa. Mipango yote muhimu iliyoanzishwa na Awamu zilizopita imekuwa ndio msingi wa Mipango na Bajeti iliyowasilishwa Bungeni. Kwa maana hii Mipango na Bajeti yetu ni endelevu na hivyo kuendeleza jitihada tulizofikia badala ya kubuni gurudumu lingine tena. Hali inathibitisha kauli ya Mheshimiwa Rais wetu aliyoitoa katika ziara yake wakati akizungumza na Watanzania waishio Dubai kuwa anayefikiria kuwa anaweza kubadilisha mambo yote ya msingi ya Serikali za Awamu zilizopita hatoweza kufanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mipango na Bajeti iliyowasilishwa inatoa matarajio na matumaini kwa wananchi katika muda huu tulionao sasa. Aidha ni Mipango na Bajeti ambayo licha ya kutekeleza maagizo ya CCM kupitia Ilani yake ya Uchaguzi 2005, vile vile inajumuisha Chama chenyewe kuona ni vipi nacho kitatekeleza maagizo hayo kwa faida ya Watanzania. Kwa CCM imefikia wakati sasa kuhakikisha Siasa ni Uchumi na si jukumu la Serikali peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kujadili Mpango na Mwelekeo wa Bajeti ya Serikali, Kamati yangu ilitoa angalizo kwa Wizara ya Mipango na Wizara ya Fedha. Ushauri tulioutoa kwanza ni kuhakikisha kuwa mpango na Bajeti iliyowasilishwa hapa Bungeni zinatoa matarajio na kujibu hoja zitokanazo na wazo la Kiuchumi *(Economic Thought)* iliyozingatia kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais wetu, ya Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Wazo hili la kiuchumi limezingatia dhana ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini; uwezeshaji wa Watanzania; ajira kwa vijana pamoja na maisha bora kwa kila Mtanzania. Angalizo la pili ni kuhakikisha kuwa Serikali kwa kusaidiana na wananchi inaendelea kutekeleza zile ahadi mahususi kama zilivyoorodheshwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwani wananchi wanazijua ahadi hizo baada ya kuzisoma. Kwa maana hiyo Mpango na Bajeti yetu ni lazima ziwe nyenzo (*tools*) za kuchochea utekelezaji wa malengo haya ya jumla badala ya kuwa ni zoezi la utaratibu tu (*routine work*). Lengo kubwa sasa ni kuhakikisha kwa kadri uchumi mkuu unapokua na kupata utulivu na hivyo vigezo vyake kukua, kwa mfano Pato la Taifa, mafanikio yake yaendelee kutiririka kwa wananchi wa kawaida mijini na vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupitia Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa na Bajeti ilijitokeza wazi kuwa, pamoja na misukosuko ya ukame, njaa, umeme na bei kubwa za mafuta, Serikali imeweza kutekeleza bajeti yake bila kuyumba. Huu ni uthibitisho kwamba mageuzi na maboresho ambayo Serikali imekuwa inatekeleza yameanza kuleta matunda hasa uwezo wa uchumi wa kustahimili misukosuko kama hiyo.

Kamati yangu inaipongeza Serikali. Mafanikio kama haya hayawezi kupatikana bila ya Mipango thabiti na utekelezaji mzuri wa Sera za CCM. Kamati inashauri mipango iliyoleta mafanikio haya iwe endelevu, iimarishwe na kuboreshwa ili uchumi ukue zaidi na huduma kwa wananchi ziongezeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya mwaka 2006/2007 ni ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne, kufuatia Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge na Madiwani. Hotuba za Mawaziri zimeonyesha matumaini kuwa uchumi wetu unaendelea kukua kama ilivyoainishwa kuwa Pato la Taifa, linatarajia kukua kwa asilimia 6.9.

Aidha, Mpango na Bajeti hii itaendeleza mipango maalum (*program*) za maendeleo ya kiuchumi na kijamii tuliojiwekea. Mipango hii ni pamoja na: Mikakati wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini, Utekelezaji wa mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania, Mpango maalum wa kuharakisha maendeleo Tanzania *(Tanzania Mini Tiger Plan -2020)*, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii(*TASAF*), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania na Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Ni matumaini ya Kamati yangu, kuwa misingi ya kuimarisha uchumi jumla iliyowekwa na awamu zilizopita za uongozi wa nchi yetu itaendelezwa kama Serikali ilivyoahidi ili kuweza kufikia malengo ya kukuza uchumi wetu kupitia mipango tuliojiwekea. (*Makofi)*

Pale ambapo pana umuhimu wa kuboresha Kamati inashauri Serikali isisite kufanya hivyo kwa maana ya kuleta mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua kuwa Serikali yetu ya Awamu ya Nne, imeanza kazi na changamoto kubwa. Tatizo la ukame limeathiri sekta ya kilimo hasa katika upungufu wa chakula pamoja na upungufu wa nishati ya umeme ambayo kwa asilimia kubwa huzalishwa na maji. Maeneo yote haya mawili katika kuyatafutia ufumbuzi wake yameligharimu Taifa fedha nyingi pamoja na akiba ya fedha za kigeni.

Ukweli ni kwamba Serikali itatumia fedha nyingi katika muda mfupi kwa kukodisha na kununua majenereta yatakayozalisha umeme pamoja na mikakati mingine ya kujenga mitambo. Ushauri wa Kamati ni kuwa Mpango na Bajeti ya Serikali hazina budi kujiwekea utaratibu na mikakati mizuri inayolenga, hasa katika muda huu mfupi, kutatua na kutoa ufumbuzi wa changamoto hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Serikali inapambana na changamoto ya kuwa na vipaumbele vingi, hivyo inabidi iamue, hata baada ya Mipango na Bajeti ya Serikali kuwasilishwa, ianze na lipi na baadaye iendelee na lipi. Karibuni katika kila Sekta yapo maeneo muhimu ambayo yanahitaji utatuzi na hapo hapo kuna tatizo la ukomo wa fedha tunazohitaji kutumia ili kuibua uzalishaji wa raslimali zetu ili zichangie vyema kwenye kukuza uchumi wetu. Hasa tukielewa kuwa Bajeti inategemea takriban asilimia 39 ya fedha kutoka nje kama misaada au mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pato la Taifa limekua kwa asilimia 6.8 mwaka 2005 ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 6.9 na ukuaji halisi wa 6.7 mwaka 2004. Makusanyo ya Mapato yalifikia wastani wa shilingi 196 bilioni kwa mwezi hadi kufikia Mei 2006. Hata hivyo mfumko wa bei umepanda kutoka asilimia 4.3 mwezi Julai 2005

hadi asilimia 6.9 mwezi Aprili 2006 na akiba yetu ya fedha za kigeni imepungua kidogo hadi kufikia kiwango cha kukidhi mahitaji yetu ya nje kwa miezi 6.3 ikilinganishwa na miezi 8.2 kwa mwaka 2004.

Mfumko wa bei wa asilimia 6.9 ni kiwango kikubwa kwa zaidi ya miaka 6 iliyopita. Chakula kimechangia kutoka asilimia 7.2 Desemba, 2005 hadi kufikia asilimia 11.2 Aprili 2006 ya mfumko huo wakati mafuta yamechangia asilimia 5.2. Hili ni eneo ambalo Kamati yangu inashauri, Serikali haina budi kulitupia macho haraka hata kwa kutumia *administrative controls* ili kupunguza makali ya maisha kwa wananchi.

Mfumko wa bei kimsingi ni kipimo cha utulivu wa bei (*price stability)* hasa za mahitaji muhimu ya wananchi na utulivu wa uchumi mkuu *Macro Economic Stability*). Kamati inashauri sera zetu za fedha (*Monetary Policies*), kodi *(Fiscal policies)* na mfumo wa bajeti ya Serikali *(Budgetary Framework),* zifuatiliwe kwa karibu sana ili zisaidie kufikia malengo ya MKUKUTA tuliyojiwekea. Kamati inashauri Serikali iendelee kudhibiti mfumko wa bei ili kuchochea ukuaji wa uchumi, kuvutia wawekezaji nchini kwa vile watakuwa na uwezo wa kutabiri gharama zao. Misingi ya kiuchumi inaonyesha kuwa mfumko mkubwa wa bei unaumiza Watanzania wa kipato cha chini na kuwapa nafuu wale wenye kipato cha kati na cha juu. Sababu kubwa ni kuwa wale wenye kipato cha chini inawachukua muda mrefu kurekebisha mfumo wa matumizi yao ya mahitaji muhimu hapo panapokuwa na mabadiliko makubwa ya bei za bidhaa za msingi ikilinganishwa na wale wenye kipato cha kati na cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili linavyoonekana linawezekana kuwa la muda mfupi hasa baada ya mavuno yanayo tarajiwa kuvunwa mashambani na hivyo kuondoa upungufu wa chakula. Taarifa ya Wizara ya Kilimo iliyotolewa hapa Bungeni, imeeleza kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula utafikia tani milioni 10.73 zikiwemo tani milioni 5.19 za mazao ya nafaka na tani milioni 5.54 za mazao yasiyo nafaka. Mahitaji ya Chakula kwa mwaka 2006/2007 yatakuwa tani milioni 9.75 hivyo kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 110.

Kamati yangu pia inaridhishwa na juhudi kubwa za Serikali za kuendelea kuongeza uwezo wa Taifa letu wa kumudu majanga haya hasa kwa kuweka mikakati mzuri ya kuhakikisha Taifa lina akiba ya chakula cha kutosha. Pamoja na jitihada kubwa zinazochukuliwa na Serikali katika kupunguza tatizo la upatikanaji wa nishati hasa ya umeme. Hatua mbalimbali za kibajeti zilizochukuliwa na Serikali za kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya taa, gesi, na kadhalika na kuondoa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta ya Petroli na kodi nyingine kwenye mkaa zitasaidia kuboresha hali ya maisha nchini. Hata hivyo Kamati inashauri hatua hizi zilizochukuliwa ziendane sambamba na *impact* ya kuwasaidia wananchi wakati wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia imeangalia na kutathimini suala la kutetereka kwa thamani ya sarafu yetu. Tatizo hili tunaweza kulidhibiti ikiwa tutaendelea na jitihada za kubadili mfumo wa uzalishaji katika uchumi wetu, ule wa kuzalisha zaidi bidhaa za kuuza nje kupitia mikakati tuliyojiwekea ya kukuza uchumi.

Hivi sasa tunaagiza bidhaa nyingi kutoka nje kuliko zile tunazozalisha. Hadi Aprili, 2006 tuliuza bidhaa nje za dola 2919.8 milioni ikilinganishwa na tulizoagiza toka nje zilizofikia dola 4012.4 milioni. Kamati yangu imeshauri Serikali kuwa, labda iwe ni lazima, lakini utaratibu wa kudhibiti kushuka kwa thamani ya sarafu yetu kwa kutumia udhibiti wa kiutawala *(administrative controls)* unaoweza kufanyika na Benki Kuu, hautachochea tija na ufanisi katika mikakati ya kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kipindi kilichopita Bajeti ya Serikali ilitanuka sana (*Expansionary Budget)* na kuleta ongezeko la *ukwasi (Excess Liquidity)* katika uchumi kwa sababu ya matumizi makubwa yaliyojitokeza nje ya matarajio ya Serikali. Matumizi hayo yalihusu, ruzuku itolewayo na Serikali ya kuisaidia *TANESCO*, gharama za mishahara ya waalimu na madaktari, malipo ya madeni ya pensheni na hatimaye, gharama za kuagiza chakula kutoka nje pamoja na zile za kuagiza mafuta. Mwaka 2004/2005 Serikali ilitumia dola 473.8 milioni ikilinganishwa na dola 940 milioni mwaka 2005/2006 kwa kuagiza mafuta.

Matumizi yote haya yameleta nakisi katika ukuaji wa Pato la Taifa ya asilimia 3. Mpango na Bajeti yetu Kamati yangu inashauri itabidi iongeze nguvu kuimarisha nyenzo za kiuchumi za kurejesha tena utulivu wa bei. Utulivu katika mfumo wa fedha na utulivu katika akiba ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuepukana na matatizo haya vile vile huko tunakoelekea ni vyema Serikali ikaendelea na uimarishaji wa kukuza uwezo na viwango vya Taifa vya Hifadhi ya Chakula kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa pamoja na kurejea uamuzi wa makusudi wa kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Mafuta. Wawekezaji wanaotaka kuanzisha miradi ya Hifadhi ya Mafuta, Kamati yangu inashauri wapewe kipaumbele kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na malengo mazuri ya kukuza Pato la Taifa ambalo kwa kiasi kikubwa linatarajiwa lichangiwe na Sekta ya Kilimo. Kamati imepatwa na wasiwasi kutokana na janga la ukame linalotuathiri mara kwa mara, tukizingatia kwa kiasi kikubwa kilimo chetu kimekuwa kinategemea maji ya mvua. Ukuaji wa sekta hii umekuwa ukishuka mwaka hadi mwaka.

Mwaka 2005 sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 5.2 ukilinganisha na asilimia 5.8 mwaka 2004. Kilimo ndiyo mwajiri mkubwa wa Watanzania. Kamati inashauri umefika wakati sasa mpango kamambe wa kilimo cha umwangiliaji utekelezwe kwa nguvu zote, sambamba na upatikanaji wa pembejeo na huduma za ugani. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuhamasisha zaidi suala nzima la uhifadhi wa mazingira kama ilivyoanishwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Taaluma na manufaa ya kuvuna maji na ujenzi wa mabwawa au malambo ya hifadhi ya maji vizingatiwe. Kamati inasisitiza mkakati wa kuendeleza viwanda vidogo na vikubwa vya kilimo tuliokwisha ukubali wakati wake ni sasa. Lakini hili litawezekana endapo Serikali itaanzisha Benki za Maendeleo zitakazokuwa na viwango vya riba nafuu,

ili kuwawezesha wakulima, wafanyabiashara wadogo wadogo, wavuvi na wafugaji kuweza kukopa na kurejesha mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Sekta ya Madini inaweza kuchangia uchumi wetu kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko hivi sasa. Sekta ya Madini ilikuwa kwa asilimia 15.7 mwaka 2005 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 15.4 mwaka 2004. Aidha mchango wa Sekta ya madini uliongezeka kwa asilimia 3.5 mwaka 2005 kutoka asilimia 3.2 mwaka 2004 katika Pato la Taifa. Kamati yangu inaamini kuwa mchango wa Sekta ya madini ni mdogo ukilinganisha na uvunaji wake.

Kamati inatoa rai na kuunga mkono kauli ya Mheshimiwa Rais, kuwa tutafute utaratibu mpya wa kila upande kwa maana ya Serikali na wawekezaji kufaidika na uvunaji wa raslimali hii, hasa tukizingatia kuwa Serikali imekwishapata uzoefu wa tozo za kodi za madini na faida na gharama za kuanzisha migodi mikubwa katika nchi yetu. Kamati vile vile inaunga mkono juhudi za Serikali ambazo zinalenga kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini. Kamati inasisitiza kuwa uzalishaji wao urasimishwe ili mapato yatokanayo na kazi zao yasajiliwe katika takwimu za uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imejadili kwa kina suala la ughali wa nishati nchini kwetu. Gharama za umeme unaozalishwa na *TANESCO* zimeendelea kupanda siku hadi siku. Kamati inashauri na kusisitiza mradi wa makaa wa mawe wa Mchuchuma na Kiwira ipewe kipaumbele cha haraka, ili Taifa linufaike na umeme rahisi na wa uhakika. Serikali imeanzisha *Export Processing Zones (EPZs)* na *Special Economic Zones (SEZs),* vyote hivi ni vyanzo vikubwa kwa ajira kwa vijana na hivi karibuni Mheshimiwa Rais ametembelea maeneo mengi duniani kukaribisha wawekezaji nchini kwetu.

Kutokana na hali hii tatizo la umeme wa uhakika na bei nafuu lazima lipatiwe ufumbuzi haraka iwezekanavyo ili tuvutie vizuri wawekezaji na tukuze uchumi wetu. Gharama kubwa za umeme zimechangia sana katika uzalishaji mdogo pamoja na kuongeza gharama za bidhaa. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitahada zinazofanyika hivi sasa za kutatua tatizo hili lakini inashauri Serikali ijielekeze kwenye kupunguza tatizo la urasimu. Hatuna muda wa kupoteza. Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya. *(Makofi)*

Aidha, Mheshimiwa Naibu Spika, umefika wakati sasa kwa Serikali kuanza utekelezaji wa mradi wa umeme wa *Stiglers Gourge* ambao umekuwa ukiahirishwa mara kwa mara. Umeme utakaoweza kuzalishwa pale ni zaidi ya uwezo wa Vituo vyote tulivyonavyo nchini hivi sasa. Gharama ya mradi huu ni kubwa lakini kuchelewa kutekelezwa kwa mradi huu gharama za kujirudiarudia zitakuwa kubwa mno kwa uchumi wetu. Tuige mfano wa Caborabasa Msumbiji na mfano wa Bwawa la Inga kule Congo.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** mwezi Aprili 2006, Bunge lako Tukufu lilipitisha rasimu ya Sheria mpya ya Mabenki na Asasi za Fedha ya mwaka 2006 na Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006. Moja ya malengo muhimu ya Sheria hizo ni kuipa Benki Kuu uwezo na uhuru zaidi wa kusimamia kikamilifu Benki na Asasi za fedha nchini ili

kupanua huduma za sekta hiyo, hasa kuwawezesha wananchi kupata mikopo ya masharti nafuu ili washiriki kikamilifu kujiondolea umaskini. Aidha Serikali imeendelea kudhamini mikopo ya mabenki kwa wananchi kupitia Mfuko wa Dhamana ya Mkopo ya Mauzo nje ya Nchi *(Export Credit Guarantee Scheme – ECGS)* na Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa Biashara Ndogo ndogo *(SME Credit Gaurantee Scheme*) inayoratibiwa na Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Waziri wa Fedha ni jambo lililo wazi kuwa yapo malalamiko kutoka kwa wananchi ya kutoridhishwa na utendaji wa mifuko hiyo ya dhamana. Kamati inashauri mifuko hiyo ifanyiwe tathimini ya kina ili iweze kutekeleza malengo yaliyokusudiwa, hususan yale ya kuwasaidia moja kwa moja wananchi wenye vipato vya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba hivi sasa tuna Mabenki mengi bado wananchi wa vijijini ambao ni wengi hawajajua utaratibu wa kuzitumia Benki hizi na huduma zake, matokeo yake wanaonufaika na Benki hizi ni wachache. Kamati inapendekeza hatua za makusudi zichukuliwe na Serikali ikishirikiana na Mabenki haya yaliyopo kutoa elimu huko vijijini ili kusaidia wananchi kufaidika na huduma hizi muhimu. Ama sivyo, jitihada za kuwawezesha wananchi hususani walio na kipato cha chini kupitia mitaji na mikopo itakayofanywa na Serikali haitazaa matunda yanayotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo wa Kamati ni kwamba Sekta za uzalishaji wa moja kwa moja katika uchumi wa Tanzania hazitaendelea haraka bila ya kuwepo chombo cha kutoa mikopo ya muda wa kati na muda mrefu kwa masharti tofauti na yale yanayowekwa na benki za kibiashara. Na kwamba Serikali isisubiri wawekezaji binafsi kuanzisha benki ya aina hiyo. Badala yake Serikali iwe ndiyo chimbuko la mpango huo. Kamati inachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kukubali kuibadili Benki ya Rasilimali kuwa Benki ya Maendeleo *(TIB).* Nchi nyingine zinazoendelea kama yetu zimetumia mfumo huu kwa tija. Ni vigumu kwa Sekta za kilimo na viwanda kufanikiwa na kupanuka bila ya mikopo ya muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu pia imeshauri Serikali, ili kuwaletea maendeleo ya kweli wananchi walio wengi inabidi kuwawezesha wananchi hao kuwa na makazi bora na ya kisasa. Kamati inashauri kuwa baada ya kufutika kwa Benki ya Nyumba *(Tanzania Housing Bank)* Serikali iangalie upya uwezekano wa kuanzisha chombo kingine kitakachotoa mikopo yakujenga nyumba za kuishi kwa utaratibu wa *Mortgage Financing.* Kamati inaishauri Serikali kwa ahadi iliyotoa ya kuunda Kamati ya kufuatilia masuala haya itoe mapendekezo kama ilivyoelezewa kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepiga hatua kwa kiasi fulani katika kuboresha mipango miji ikiimanisha iko haja sasa ya kuboresha mipango ya vijijini ikiandamana na msisitizo wa kuboresha kilimo cha kisasa. Kwa vile kilimo ndio chanzo cha ajira na mapato cha wakulima vijijini maendeleo ya sekta hii yaende sambamba na utamaduni wa

ujenzi wa nyumba bora utakaosaidiwa na "*Mortgage Financing*" pamoja na kuboreka kwa kilimo chenyewe wanachokiendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Fedha; lakini bado mchango wa Sekta ya Fedha katika ukuaji wa uchumi ni mdogo na unahitaji kuongezeka zaidi ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Mathalani, kwa sasa mikopo ya sekta binafsi ni wastani wa asilimia 10 ya pato la Taifa ambacho ni kipimo cha mchango wa sekta binafsi katika ukuaji wa uchumi. Kiwango hiki ni chini sana ukilinganisha na Kenya (asilimia 21.3 ya Pato la Taifa).

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ambalo linaelekea sasa litakuwa sugu ni pengo kubwa kati ya riba anayolipwa mtu anayeweka fedha zake benki, yaani amana na riba anayolipa mtu anayekopa benki. Mathalani mtu anayeweka amana benki hulipwa asilimia 2.5 tu na anayekopa benki hutozwa riba ya asilimia 15.12, tofauti ya asilimia 12.71. Hali hii inadidimiza motisha ya kuweka akiba baina ya Watanzania na kuwazuia kabisa wale wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inashauri kuwa, kwa kuwa Sheria mpya ya Benki Kuu ya 2006 imeshapitishwa, watumie fursa waliyopewa katika sheria hiyo kusimamia masuala haya ili kukabiliana na changamoto zilizopo katika Sekta ya Fedha, eneo hili lisipofanyiwa kazi hatua za uwezeshaji zilizopangwa na Serikali hazitaweza kufanikiwa, zitaathiri tu si wale wenye vipato vya juu bali hata wale wenye vipato vya chini hususan vijijini. Hata kama *SACCOSS* zikianzishwa Riba ikiwa kubwa lengo la mkakati mzima halitazaa matunda yanayotarajiwa. Aidha, suala la mgawanyo wa hisa kutoka Benki Kuu kwenda kwa wanahisa, yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Tume ya pamoja ya Fedha *(JFC)* likamilishwe.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kupata mafanikio katika Sekta ya miundombinu hususan katika ujenzi wa barabara na mawasiliano ya simu. Ukosefu wa miundombinu yenye ubora wa Kimataifa ni gharama kubwa ya uwekezaji nchini. Miundombinu ya kiuchumi zikiwemo Reli, Barabara, Bandari, mfumo wa umeme, maji, teknolojia ya habari na mawasiliano zikiendelea kuboreshwa vitatoa chachu muhimu katika kuongeza uzalishaji katika sekta zote nchini, kuleta ushindani katika mauzo ya nje na pia kuiwezesha Tanzania kufaidika na soko la nchi zinazotuzunguka katika kutoa huduma za bandari na reli kwa maana ya uchumi wa kijiografia. Kamati yangu inaishauri Serikali kuwa suala la muhimu sasa katika eneo hili ni kushughulikia haraka mpango wa kuboresha reli yetu.

Hii haitasaidia nchi yetu tu bali hata nchi za jirani ambazo ni wateja wetu wa uhakika. Mpango huu hauna budi kupewa kipaumbele na Serikali. Kamati yangu inashauri Serikali kuchukua hatua za haraka za kupunguza tofauti kubwa za Uwekezaji na Maendeleo baina ya maeneo na Mikoa. Ingawaje misingi ya Kiuchumi inaonyesha kuwa penye maendeleo zaidi ndipo panapovutia Wawekezaji, hatua za makusudi zichukuliwe na Serikali katika kuboresha miundombinu katika baadhi ya Mikoa, ili kuondoa au kupunguza tofauti kubwa zinazojitokeza.

Hili lisiporekebishwa zitajengeka hisia kwamba upo mkakati wa makusudi wa kuendeleza maeneo mengine dhidi ya mengine nchini. Kamati yangu inaisisitiza Serikali kuwa na msukumo wa uwekezaji *Investment drive* ndiyo njia pekee ya kujenga uchumi imara.

Tumejitahidi kujenga mazingira bora ya uwekezaji lakini hata hivyo kero zinazozuia kasi ya uwekezaji nchini kama vile Sheria zetu mfumo wa kodi zetu, uwekaji wa malengo wa upimaji wa ufanisi na matokeo ya utendaji wa taasisi zinazosimamia na kuhudumia sekta binafsi urasimu, uzito wa kutoa maamuzi na kadhalika au ziboreshwe au zitafutiwe ufumbuzi wa haraka. Serikali itoe kipaumbele katika kushughulikia maeneo haya ili tuvutie wawekezaji wa ndani na wa nje. Duniani eneo linalopunguza kasi ya uwekezaji Tanzania ambalo linazungumziwa ni lile la Sheria zetu za kodi. Haya yafanyiwe kazi haraka ili kuvutia wawekezaji wa nje na wale wa nyumbani. Kamati inaipongeza Serikali kwa kupeleka fedha ngazi ya Serikali za Mitaa ili zikasimamiwe na Halmashauri za Vijiji, Wilaya, Manispaa na Jiji. Mpango huu ni mzuri, lakini upo wasiwasi mkubwa juu ya matumizi ya fedha hizo kwa sababu Halmashauri nyingi hazina uwezo wa kumudu kusimamia fedha hizo, uwezo wa kiutawala na kihasibu bado ni mdogo. Kwa hiyo, fedha hizi zinazopopelekwa kuna uwezekano mkubwa wa kupotea na hivyo kushindwa kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Kamati kupitia Wizara ya Fedha imebaini kuwa jumla ya mapato ya Sh.4,850,588 milioni Halmashauri za Wilaya zimetengewa Sh.730,285 milioni karibu asilimia 15.05 ya fedha zote. Hata hivyo kiwango kikubwa cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya Wizara Sh. 2,037,536 milioni, na zile za Mikoa Sh.60,514 milioni kwa sura ya Bajeti ya mwaka 2006/2007 fedha hizo nyingi zitaelekezwa kwenye Halmashauri za Wilaya kwa njia ya MEM, MES, *TASAF*, ruzuku ya shilingi bilioni 21 ya pembejeo na kadhalika.

Kutokana na mantiki hii Halmashauri za Wilaya zinapata karibu zaidi ya asilimia 70 ya fedha zote za Bajeti. Hapa ndipo tatizo linapotokea kuhusu usimamizi na matumizi ya fedha zote hizi huko Wilayani. Imefikia wakati sasa Serikali ijiulize uwezo wa Halmashauri hizi katika kutumia fedha hizi. Fedha hizi zikitumika vizuri zitasaidia sana Serikali kufikia malengo yake iliyojiwekea katika Mpango wa MKUKUTA. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imebainisha kuwa matatizo ya rushwa ambalo limechukua asilimia 30 nchini, tatizo la ufisadi ambalo limechukua asilimia 20, tatizo la mgongano wa maslahi *(conflict of interest)* ambalo limechukua asilimia 25 na lile la kutokujali sheria za nchi lilochukua asilimia 25 ni matatizo makubwa katika upotevu wa fedha za Serikali hasa, kwenye Halmashauri zetu ambako matatizo hayo yanafanya kazi kwa pamoja.

Hii ni changamoto kubwa kwa Wizara hizi mbili, hususani Wizara ya Fedha. Kamati yangu inashauri kwamba umefika wakati kufuatilia kwa karibu matokeo kwa maana ya *(impact)* ya kufuatilia kwa karibu matokeo kwa maana ya *impact* ya fedha katika Halmashauri zinavyotumika katika maeneo yaliyopangiwa na kuwafikia walengwa.

Serikali inapimaje thamani ya fedha zinazotolewa maana yake *(value for money)* kwenye Halmashauri hizo. Zoezi hili lisiangalie tu jinsi fedha zilivyotumika bali pia litathmini raslimali zilizopatikana kutokana na matumizi hayo.Serikali iwe na rejista ya raslimali *"fixed asset register"* Serikali ifanye maandalizi ya kutosha ya kujenga uwezo katika kuboresha viwango vya watumishi, vitendea kazi na elimu ya mipango ya nchi na kuimarisha usimamizi wa ufuatiliaji hasa katika Halmashauri zetu za Wilaya. Kamati vile vile inatoa pongezi kwa uamuzi wa Serikali wa kuingia Mikataba na Halmashauri za Wilaya ili kupima viwango vya utekelezaji kutokana na fedha zinazotolewa huko kuhudumia maendeleo. Ingawa nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali iko chini, iko haja ya kuboresha vipengele vya Kisheria ili kuongeza udhibiti wa fedha za umma ili matumizi ya Serikali yawe yenye tija kubwa. Kwa vile Serikali imekiri udhaifu huu, ina wajibu wa kulisimamia suala hili hasa ikizingatiwa kiwango kikubwa cha fedha zinazopelekwa kwenye maeneo hayo ni mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo maalum cha kufuatilia matumizi ya fedha katika Halmashauri, *Expenditure Tracking Unity* kilichoanzishwa na Wizara ya Fedha sasa hakina budi kiimarishwe zaidi. Aidha, Halmashauri za Wilaya lazima sasa zifanye kazi. Kamati yangu haina kipingamizi na mchakato wa Serikali wa kubinafsisha Mashirika na Makampuni, bali inatahadharisha kuwa ubinafsishaji wa Mashirika yaliyosalia ya Reli, *TANESCO* na Maji kwa njia ya ukodishaji unahitaji uangalifu na umakini mkubwa. Mashirika haya yanagusa maisha ya watu moja kwa moja na yanagusa uhai wa uchumi wa Taifa letu. Shirika lolote kati ya haya haliwezi kufa peke yake, likifa na sekta nyingine nyingi nazo zitakufa pamoja nalo. Umeme unagusa viwanda, maji yanagusa viwanda nakadhalika. Aidha, usalama na ustawi wa wananchi unakuwa mashakani. Kutokana na umuhimu huo Kamati yangu inashauri Serikali ichukue tahadhari zote muhimu wakati wa kubinafsisha Mashirika haya. Kamati vile vile inaishauri Serikali ijitahidi kukamilisha mkakati wa kukodisha Reli, ili ichangie kwa ukamilifu katika kujenga Uchumi wa nchi pamoja na kutoa huduma bora za usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania inafanya kazi nzuri katika kufanikisha jukumu lake la kusimamia na kukusanya mapato. Katika miaka miwili ya fedha iliyopita 2003/2004 na 2004/2005, Mamlaka ya Mapato imeweza kukusanya mapato zaidi ya malengo yaliyowekwa. Aidha, takwimu zilizopo zinaoonyesha kwamba makusanyo ya mwaka wa fedha 2005/2006 hadi kufikia Aprili yalifikia shilingi 1,585,709.1 milioni ukilinganisha makisio ya shilingi 1,578,193.0 milioni katika kipindi hicho. Mwelekeo hadi Juni 2006 ni kwamba makusanyo yatafikia lengo au kuzidi kiasi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** haya ni mafanikio makubwa lakini bado *TRA* inahitajika na kuwajibika kuongeza juhudi za kukusanya mapato zaidi. Mapato ya Serikali bado hayawiani na matumizi, hali inayosababisha kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ili kuziba pengo la bajeti. Uwiano wa mapato yetu na Pato la Taifa *(GDP)* bado uko chini na kazi zaidi inatakiwa kufanyika. Kamati yangu inaunga mkono kauli ya Mheshimiwa Rais alipotembelea *TRA* kuwa waongeze juhudi za makusanyo ya mapato ili waweze kufika wastani wa shilingi bilioni 200 kwa mwezi ifikapo mwishoni mwa mwaka huu wa fedha. Bajeti yetu hadi sasa ni tegemezi kwa asilimia 39.

Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudi ya kukusanya mapato yetu ya ndani. Hali hii itasaidia kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha unaotokana na mikopo na misaada kutoka kwa Wahisani, ili uendane na kiwango halisi cha Uchumi wetu. Serikali iendelee kudhibiti mfumko wa bei na kushuka kwa uzalishaji wa bidhaa nje unaoweza kutokea, kutokana na fedha na misaada kutoka kwa Wahisani, kitaalam wanaita *dutch disease effect.* Aidha, tunapokusanya mapato mengi kutokana na kuongeza wigo wa kodi tutaboresha Bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu kwa ujumla inapongeza Serikali kwa kuwa sikivu hususani baada ya kuzingatia kuwa imekubaliana kwa kiwango kikubwa na ushauri uliotolewa na wana Kamati katika kujadili Mpango na Bajeti zilizowasilishwa. Huu ni utaratibu mzuri na unahitaji kuboreshwa ili kazi za Kamati za Bunge zipate ufanisi zaidi. Hapa niseme, *given the current social economic circumstances of our economy there could be no good plan and budget like this one.* Nina maanisha, kwa hali ya sasa tuliyonayo hii ni bajeti nzuri na mipango mizuri, kilichobaki ni utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu, inatambua kuwa Mipango na Bajeti ni mwelekeo na Dira ya utekelezaji wa Serikali yetu katika kipindi kijacho. Kwa hiyo, basi katika mchakato wa kuandaa Mipango na Bajeti, moja ya kazi ya Bunge ni kuishauri na kuikosoa Serikali *(Constructive Criticism)* kwa kushiriki kikamilifu.

Kamati yangu imegundua udhaifu mkubwa, katika eneo hili ambalo unahitaji marekebisho. Kwa utaratibu wa sasa Bunge lako tukufu linaonekana kama vile kazi yake ni kupitia tu shughuli za Serikali. Mara baada ya Mipango na Bajeti kuwasilishwa mbele ya Kamati za Bunge, uwezo wa Kamati hizo kufanya mabadiliko ni mdogo. Aidha Kamati zote za Bunge hazijapatiwa fursa nzuri na muda wa kutosha wa kujadili Taarifa hizo za Kamati kwa ukamilifu. Hali hii inaondoa uzingatiaji wa hoja za Wabunge na hata mchango wa Bunge kwa ukamilifu. Kamati yangu inashauri tuweke utaratibu utakaojibu ni wakati gani ambapo maoni na mawazo ya Wabunge yapokelewe ili yawe ni sehemu ya Mchakato mzima wa Bajeti na Mipango inayowasilishwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu utaleta tija na ufanisi katika mipango na Bajeti zetu ikiwa misingi muhimu itakayokubalika kutoka Kamati za Bunge inakubaliwa na kuingizwa katika Mipango na Bajeti. Yatakapozingatiwa mawazo na maoni ya Kamati za Bunge hatima yake mijadala yetu ya mipango yetu na Bajeti zetu hapa Bungeni zitakuwa na manufaa zaidi. Kamati ya Fedha na Uchumi inashauri utaratibu huu ufuatiliwe haraka ili uanze kutumika katika kipindi cha 2007/2008.

Mheshimi8wa Spika, utaratibu huu utaongeza nguvu ya ushauri wa Wabunge Serikalini, lengo likiwa ni moja tu kusaidia maendeleo ya nchi. Huko ndio inakofaa tuelekee. Napenda kusema kwa wazi na kwa dhati kabisa kwamba Kamati yangu ya Fedha na Uchumi, itakuwa bega kwa bega katika kuhakikisha matarajio ya wananchi kwa serikali yao ya Awamu ya Nne ya CCM yanatekelezwa kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati yangu ya Fedha na Uchumi kwa kazi nzuri walioifanya na kwa ushirikiano wao walionipa. Naomba nitumie fursa kama kawaida hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda - Mwenyekiti, Mheshimiwa wa Kamati, Mheshimiwa Adam K. Malima, Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke ambaye ni Mjumbe.

Wajumbe wengine ni Meshimiwa Parmoukh S. Hoogan, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Eustace, O. Katagira, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o na Mheshimiwa Elisa D. Mollel. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wajumbe wengine ni Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Omar S. Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Mzeru O. Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa na Mheshimiwa Hamad R. Mohammed. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Adam K. Malima, Mbunge wa Mkuranga ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kunisaidia kuongoza Kamati hii muhimu.

Aidha namshukuru Ndugu Anselm Mrema na Ndugu Hellen Mbeba, Makatibu wa Kamati kwa kuihudumia Kamati vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kuwapeni shukrani maalum Mheshimiwa Spika na wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge letu Tukufu, kwa kutuongoza vizuri na kutoa fursa kwetu sisi kutekeleza majukumu yetu ya Kibunge vizuri tena kwa viwango na spidi inayohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI (MIPANGO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kusoma maelezo ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, napenda kutambua nikiwa kama Mwafrika, ushindi wa timu ya Ghana dhidi ya timu ya *Czech Republic.* Naamini kabisa kwamba wataendelea kufanya vizuri na kutoa heshima kwa Bara letu la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwa niaba ya Kambi ya Upinzani napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya Bajeti kuhusu Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1) toleo la Mwaka 2004. Aidha nakupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kwenu kushika nyadhifa hizo. Tuna imani kubwa na ninyi na tunaamini kuwa mtaitumia imani hiyo kujenga Bunge lililo imara lenye uwezo wa kuisimamia Serikali katika utendaji wa kazi za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Edward N. Lowassa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania na Kiongozi wa Upinzani Bungeni sawia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile natoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ushindi wake ni ishara ya imani walionayo Watanzania kwake. Naamini hatawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima nawapongeza viongozi wote wa vyama vya upinzani waliogombea urais kwa kazi walioifanya, japokuwa uwanja wa mashindano haukuwa sawa. Nawapongeza kwa kazi walioifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa mara nyingine kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kigoma Kaskazini kwa kunichagua kuwa Mbunge wao. Nitahakikisha kuwa imani waliyo nayo kwangu kwa kunichagua nairudisha kwao kwa kutimiza yale yote yaliyomo ndani ya uwezo wangu kwa kuyafanya kwa dhati kwa maendeleo ya Jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu za dhati kwa Shirika la *Fredrick Hubert Foundation* kwa kunilea kiuongozi na kunipa elimu na maarifa kupitia mafunzo na baadaye kazi. Mchango wao ninauthamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze kwa dhati kabisa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa hizo. Fanyeni kazi za umma kwa uadilifu, kwa viwango na kwa kasi bila ubaguzi wa aina yoyote kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa na kutekeleza wajibu wetu ya kitaifa. Namwomba Mwenyezi Mungu atujalie afya njema na hekima ili tuwatumikie vyema Watanzania. Mungu atupe busara ili tuwatumikie Watanzania bila kujali rangi, kabila, dini, jinsia, hali ya maungo, hali ya afya na bila kujali itikadi ya vyama vyetu vya siasa. Ni jukumu letu kuhakikisha kuwa Serikali inatekeleza mipango ya maendeleo kwa Watanzania bila kubagua. Yasipotekelezwa

tutawaambia wananchi walikosea kuchagua. Hivyo sisi ni changamoto kwa chama kinachounda Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutakaa kimya tukiona Serikali inakosea. Tutaisema humu Bungeni na kutoa mwelekeo mzuri kwa maslahi ya Mtanzania. Na Serikali isipotusikiliza humu Bungeni tutaenda kusema nje ya Bunge. Tunawatahadharisha Mawaziri waliopewa dhamana na Rais kutekeleza majukumu yao kwa kasi na viwango ili tija iwe wazi kwa kila Mtazania. Dira ya nchi ni moja kama tulivyokubaliana kutengeneza *vision 2025.* Mkakati wa nchi ni kutekeleza dira hiyo nao ni umoja. Hata hivyo, kila chama kinaweza kuwa na mtazamao au utekelezaji unaotofautiana. Mitazamo hiyo isigawe Watanzania, wala kubaguana kwa vile ina lengo la kutajirisha na kufikia haraka malengo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo bajeti ya mpango ni utekelezaji wa dira ya Taifa na inapaswa kuwa shirikishi na yenye kutuunganisha zaidi kuliko kutugawa. Serikali inapaswa kutekeleza dira na mikakati ya Taifa ambayo imetungwa na Watanzania wote kufuatia mbinu shirikishi. Mfano halisi ni dira ya maendeleo ya taifa *Vision 2025* na Mpango wa kupunguza umaskini MKUKUTA. Mpango huu ulitungwa na wananchi wote kupitia mashirika yasiyo ya Kisirikali na Warsha za kikanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Siasa vinapaswa kutoa miongozo ya namna bora ya kutekeleza hiyo mipango iliyopangwa na wananchi, na vyama hivyo havitegemei kutumia bajeti ya Serikali katika kutoa miongozo hiyo, kwani hiyo ni majukumu rasmi ya vyama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa nijadili hali ya uchumi wa nchi na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuboresha mpango wa MKUKUTA. Serikali iliyoko madarakani ni hiyo hiyo iliyoko madarakani toka tupate uhuru, tukiacha tofauti ya majina, maneno ya awamu, ni lugha tu, lakini wahusika wakuu ni wale wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo tunapopitia hali ya uchumi tunapima utekelezaji wa Serikali moja ya CCM kwa kipindi chote. Hivyo, Chama cha Mapinduzi hakiwezi kukwepa mapungufu ya Serikali zilizopita kama jinsi ambavyo hakiwezi kukwepa pongezi kwa awamu zilizopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa Ujumla na maoni ya Kambi ya Upinzani. Wakati akitoa hotuba ya hali ya uchumi mwaka 2004, Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Ubinafsishaji, aliliambia Bunge lako Tukufu tarehe 9 Juni, 2005 kwamba, pato la Taifa litakuwa kwa asilimia 6.5 mwaka 2005, asilimia 7.2 mwaka 2006, asilimia 7.6 mwaka 2007 na asilimia 7.9 mwaka 2008. Kiwango cha kasi cha upandaji bei kisichozidi asilimia nne, kitakuwa kimefikiwa ifikapo mwezi Juni, 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa uchumi ulifikia asilimia 6.8 tu, na kasi ya upandaji wa bei mpaka mwezi Juni imefikia takribani asilimia saba. Hali ni mbaya zaidi kwa kuwa kasi ya upandaji wa bei ya chakula imefikia asilimia 11 mpaka mwezi Aprili.

Mheshimiwa Waziri amesema uchumi mwaka 2006 utakua kwa asilimia 5.6 tu, tofauti na makisio ya mwaka jana 2005. Hii inaonyesha kwamba Serikali imeshindwa kufikia malengo iliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za kwamba uchumi umeharibiwa na ukame na tatizo la umeme, hazitoshi. Lengo la asilimia 7.2 kushuka mpaka asilimia 5.9 linahitaji maelezo zaidi ya ukame, umeme na mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukame hutokea nchini kwa wastani wa kila baada ya miaka kumi. Ni kosa tu la kutumia takwimu za hali ya hewa vizuri na kutokuwa na sera za kuweka tahadhari wakati wa maafa kama hayo. Hata Afrika ya Kusini na hata Ulaya hupata maafa kama haya, lakini kwa sera nzuri huweza kujikimu ndani kwa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa wapi kuweka mipango bora na sera sahihi za kuzuia ukame kutuathiri? Tulikuwa wapi kuweka sera bora za kuhakikisha umeme unakuwepo wa kutosha? Madhara tunayoyapata sasa ni makosa ya kisera na kimfumo yaliyofanyika miaka ya nyuma. Madhara tutakayoyapata kesho ni matokeo ya sera mbaya tutakazoziweka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu, kuna mipango gani ya baadaye ili kuepuka madhara ya ukame mwakani 2007 ili malengo ya mwakani yaweze kufikiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uchumi wetu sio nzuri kwa sasa. Tangu mwezi Januari mwaka huu mfumuko wa bei umekuwa ukiongezeka kwa wastani wa asilimia 0.2. Shirika la nchi zenye viwanda *OICD* limekisia kuwa ukuaji wa uchumi wa Tanzania utashuka mwaka huu 2006 na kwamba uchumi unakadiria kukua kwa asilimia 5.8 tu na sio asilimia 5.9 kama alivyobashiri Mheshimiwa Waziri wa Mipango. Hii ni hatari, kwani kwa ukuaji huu hatuwezi kufikia wastani wa kukua uchumi kwa asilimia nane kwa miaka mitatu mfululizo ili tuweze kupunguza umaskini kwa nusu ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa uchumi wetu unachangiwa na sekta kadhaa. Sekta ya Kilimo inaongoza. Mchango wa Sekta ya Kilimo mwaka jana 2005 ulikuwa asilimia 45.6 tofauti na mwaka 2004 ambao ulikuwa asilimia 46.3. Kwa uchumi wowote unaokua, mchango wa Sekta ya Kilimo katika uchumi upaswa kupungua mwaka hadi mwaka kwani ukuaji wa sekta nyingine kutokana na kupanuka kwa uchumi hupunguza mchango wa Sekta ya Kilimo.

Hata hivyo, kwa Tanzania nadharia hii bado haifanyi kazi. Mchango wa Sekta ya Kilimo katika pato la Taifa unashuka kutokana na ukame na kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na chakula. Hii inaonyesha kuwa bado hatujafanya kazi sawasawa katika kuleta mapinduzi ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Madini ilikuwa kwa asilimia 15.7 mwaka 2005, mwaka 2004 sekta hii ilikuwa asilimia 15.4. Hata hivyo, ukuaji wa Sekta ya Madini hauendani na ukuaji wa ajira na kupungua kwa umaskini. Taarifa ya hali ya

umaskini nchini inaonyesha kuwa Sekta ya Madini inachangia ajira chini ya asilimia moja, yaani katika kila ajira 100 zinazotengenezwa nchini katika mwaka, Sekta ya Madini inachangia chini ya mtu mmoja katika ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inasababishwa na sababu moja kubwa, kwamba migodi ya madini inamilikiwa na wageni wachache. Serikali haijafanya juhudi kuimarisha wazawa walioko katika Sekta ya Madini na migodi pia haina mahusiano mazuri na sekta nyingine za uchumi, yaani *forward* na *backward linkages*. Ndio maana leo hii ni jambo la kawaida kwa migodi ya madini kununua hata nyanya na vitunguu kutoka Afrika ya Kusini. Sera mbaya ya madini isiyomjali Mtanzania maskini ndio chanzo cha tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utalii vilevile inao mchango wake katika uchumi wa nchi. Unakua, lakini mchango wake katika ajira ni mdogo. Watalii wanakuja Tanzania katika mbuga zetu, mlima wetu wa Kilimanjaro na fukwe zetu nzuri za Zanzibar, wakiwa wamelipa kila kitu huko kwao, yaani *package tourism*. Kuna ukwepaji wa kodi uliokithiri katika hoteli za kitalii, sera mbaya za sekta ya utalii ambazo hazimjali Mtanzania maskini ndio chanzo cha tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya hali ya umaskini nchini, ambayo Mheshimiwa Waziri hakuigusia katika hotuba yake, imeelezea hali ya umaskini kwa kila Wilaya ya Tanzania. Taarifa imetaja Wilaya ya kwanza mpaka ya mwisho kwa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa tu, nitaje Wilaya tatu tajiri ambazo wananchi wake wana uwezo wa kupata milo mitatu kila siku, yaani kwa kutumia kipimo cha *percentage of population of below basic needs poverty line* na Wilaya maskini zaidi kwa mwaka 2005. Wilaya tajiri ni Bukoba Mjini, Arusha Mjini na Mbeya Mjini, kati ya wananchi 100 Bukoba Mjini wananchi 11 tu ndio hawana uwezo wa mahitaji ya msingi. Arusha Mjini ni wananchi 12 na Mbeya Mjini ni watu 12 pia.

Napenda niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wanaotoka katika Wilaya hizi kwa Wilaya zao kufanikisha kuondoa umaskini.

Wilaya maskini zaidi ni Geita, Musoma Vijijini na Bunda. Wananchi 62 kati ya 100 wa Geita hawana uwezo wa mahitaji ya msingi. *Sixty two!* wananchi 64 Musoma na wananchi 68 Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ni muhimu sana kutolewa katika Bunge letu ili tuweze kujipima kwa ngazi ya umaskini wa Wilaya zetu ili iwe changamoto katika kuleta maendeleo. Taarifa ya hali ya umaskini, *Poverty and Human Development Report* ya mwaka 2005 ni ya Serikali, na inastahili kuletwa Bungeni na Waziri wa Mipango na pia iwe sehemu ya hotuba ya hali ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tujiulize maswali, ni kwanini Wilaya ya Geita yenye utajiri wa dhahabu lukuki yenye samaki wa Ziwa Victoria, yenye pamba, yenye ng’ombe na watu wenye nguvu inakuwa Wilaya maskini! Zaidi ya nusu ya wananchi wake hawana uwezo wa kula, kuvaa na kulala. Ni lazima tujiulize maswali

magumu yenye majibu sahihi. Wilaya ya Geita ni mfano tosha wa jinsi  asilimia zilivyo hazisaidii maendeleo ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili uchumi uweze kuwa na manufaa kwa Watanzania, ni lazima  Serikali kwa makusudi kabisa iamue kuweka sera rafiki kwa maskini, yaani *pro-poor policy*.  Sera rafiki kwa watu maskini ni zile zinazoelekea kuweka rasilimali katika sekta zinazokua na zinazoajiri watu wengi zaidi.

Kilimo ni sekta pekee inayoweza kuondoa umaskini nchini Tanzania, hivyo lazima maamuzi ya makusudi yafanywe kuwekeza rasilimali katika kilimo. Wataalamu wanasema kuwa iwapo tukiweza kufanya kilimo kikue kwa asilimia 10 kwa miaka mitatu mfululizo, umaskini nchini utapungua kwa asilimia 50 kabla ya muda wa mwisho wa malengo ya milenia, mushima wa kimataifa na kikanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeendelea kuwa mwanachama wa Mashirika ya kikanda ya kimataifa, Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Umoja wa Nchi Huru za Afrika, Ushirikiano wa Nchi za Afrika, *Caribbean* na *Pacific, ACP* na Tume ya Bahari ya Hindi. Malengo mbalimbali yanatufanya tujiunge na Mashirika haya ya kikanda na kimataifa ikiwemo biashara  na masuala ya usalama na misaada ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ilijitoa katika soko la pamoja kwa nchi ya Kusini mwa Afrika *COMESA* mwaka 2000. Inawezekana kabisa kuwa uamuzi huo ulikuwa muafaka wakati huo. Hata hivyo, tafiti mbalimbali zilizofanywa na wataalam wa biashara ya kimataifa na umoja wa wafanyabishara kama *Confederation of* Tanzania *Industries* zinaonyesha kuwa Tanzania inapata hasara kuwa nje ya *COMESA*.

Tunatambua umuhimu wa *SADC* kihistoria, lakini tutaishi mpaka lini ndani ya mfuko wa historia? Dunia ya sasa inaendeshwa kwa masuala ya kiuchumi, tulitarajia kuwa katika hotuba ya hali ya uchumi wa Tanzania Waziri mwenye dhamana ya uchumi angeweza kusema kitu kuhusu *COMESA* na madhara tunayopata kwa kutokuwa mwanachama wa *COMESA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa nchi zote za *ACP* ikiwemo Tanzania zimo katika mjadala kupitia makundi yao kwa kitu kinachoitwa *Economic Partnership Agreement* au *EPA*, *EPA* kwa lugha nyepesi ni umoja wa soko huria.  *EPA* inadhamiria kuondoa vikwazo vya biashara kati ya nchi za *ACP* na nchi za Jumuiya ya Ulaya. Mahusiano ya biashara yaliyopo hivi sasa ni ya upendeleo, yaani *non reciprocal* ambapo Tanzania anauza bidhaa zake zote isipokuwa silaha katika soko la *AU* bila kodi, yaani *Everything But Arms (EBA)*.

Mahusiano haya ya biashara yanawezeshwa na msamaha, yaani *WEVA* kutoka Shirika la Kimataifa *WTO*. Msamaha huu unaisha Desemba, 2007.  Kwa masikitiko makubwa, nimeshangazwa na hatua ya Serikali kuongeza juhudi katika mwaka 2006/2007 kutumia fursa ya soko la *EBA* ambalo limebakiza mwaka mmoja na nusu tu.

Inasikitisha kuwa wakati tunaomba kuwekeza juhudi katika eneo hilo, hata kuingia katika soko la **AGOA** bado ni tatizo.

Tanzania inajadili *EPA* katika nchi za *SADC* ambazo ziko nchi saba tu, lakini katika hizo nchi za *SADC* kuna nchi nne ambazo ziko *SAKU* na *Mozambique* na Angola zinatarajia kujiunga *SAKU*. Kwa hiyo, Tanzania kimsingi inajadili *EPA* ikiwa peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika rasimu ya makubaliano iliyowasilishwa Jijini Brasils Makao Makuu ya *AU* Afrika ya Kusini, sasa imeomba rasmi kuwa katika *SADC, EPA*, na kuzitaka nchi nyingine zote za *SADC, EPA* kuwa wanachama wa *SAKU Associate Members.* Hili Mheshimiwa Waziri hakuligusia kabisa. Bunge linapaswa kujua kuwa ndani ya mwaka mmoja na nusu, maana yake *EPA* tunaanza mwaka 2008, ndani ya mwaka mmoja na nusu ujao hatutakuwa na uhuru wa kupanga kodi zetu kwani Afrika Kusini itapanga kodi kwa niaba yetu kupitia *SAKU. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za Kenya na Uganda zinajadili *EPA* kupitia kundi la *EFA* ambalo ni wanachama wa *COMESA*, kitendo cha nchi wanachama Jumuiya ya Afrika Mashariki kujadili *EPA* katika makundi tofauti ni kitendo kinachoua uhuru wa forodha kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwani kitaalam nchi moja haiwezi kuwa mwanachama wa ushuru wa forodha mbili. *EPA* inapelekea makundi ya nchi kuwa na ushuru wa forodha. Sisi kama nchi tukijua kabisa madhara, tumeamua kujiweka katika ushuru wa forodha na Afrika Kusini badala ya ushuru wetu wa forodha na Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango maalum ya kiuchumi na kijamii, Serikali imeendelea kutengeneza mikakati mbalimbali ya kuendeleza nchi. Tulikuwa na *PRSP*, sasa MKUKUTA, MKURABITA na neno jipya kabisa MKUMBITA. *PRSP* haikueleweka na wala matokeo yake hatujajulishwa. Tukatengeneza MKUKUTA. MKUKUTA ni mpango mzuri sana, umeshirikisha jamii nzima, Mashirika yasiyo ya kiserikali, Vyama vya Siasa, Vyama vya Wafanyakazi na wataalam mbalimbali. Namshukuru Mwenyezi Mungu pia kwamba hata mimi nilishiriki katika kutengeneza MKUKUTA kupitia Asasi ya vijana ya *TYVA*. Sasa MKUKUTA haujaeleweka, imekuja MKURABITA. Huu hujaeleweka kabisa, kwani wenyewe haukuwa shirikishi, ni mambo ya Desoto. Juzi tumeletewa MKUMBITA, hii misamiati haiwezi kuleta maendeleo, tunachanganya tu wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, MKUKUTA ndio dira ya kutuongoza kukuza uchumi na hatimaye kupunguza umaskini, kazi iwe ni kuufanya MKUKUTA utekelezeke hata kwa mtu mmoja mmoja. Maeneo matatu ya MKUKUTA, Ukuaji Uchumi na Upunguzaji wa Umaskini wa kipato, Uboreshaji wa Maisha na Ustawi wa Jamii na Utawala Bora na Uwajibikaji yanapaswa kujulikana kama Azimio la Arusha lilivyojulikana na kuimbwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* umefanya kazi nzuri sana. Napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mkurugenzi Mkuu wa *TASAF,* Ndugu Dr. Likwelile kwa kazi nzuri inayofanywa na *TASAF*. Hata hivyo, kuna

watu wanataka kuharibu kazi nzuri ya *TASAF*, miradi ya *TASAF* sio ya kisiasa, ni miradi ya wananchi wote. Wanasiasa wanaopitapita huko Vijijini kudanganya wananchi kuwa wajiunge katika makundi ili wapate mikopo kutokana na itikadi za Vyama, wanakosea fedha za *TASAF*, ni miradi ya kijamii, ni marufuku kwa wanasiasa kupita jumuiya zao kuwagawa wananchi kivyama.

Ni jukumu la Serikali ya Kijiji au Halmashauri ya Mtaa kuratibu upatikanaji wa miradi ya *TASAF*, Mkutano Mkuu wa Kijiji au Mtaa ndio chombo cha mwisho chenye jukumu la kupitisha miradi na wala sio kundi la wanasiasa pale Kijijini au kwa Sheha.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma limeleta lawama kubwa kutoka kwa wananchi. Baadhi ya lawama zimeanza kujidhihirisha. Bunge litakumbuka kelele zilizopigwa kuhusu *TANESCO* na *NET GROUP SOLUTION*. *NET GROUP SOLUTION* tunawafukuza, lakini walioingia Mkataba huu wamenona, wameshiba, Taifa linaangamia, Wizara ya Fedha inatoa mabilioni kila mwezi kama ruzuku kwa *TANESCO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hebu tujiulize, nani anatumia umeme kule Kalizi, Nyalubanda, Kakunga, Nyamuoza, Kigale, Tankabwimba hakuna umeme! Umeme unatumika na watu wa *middle class*, mabilioni ya fedha yanatumika kwa matajiri tu. Watu maskini wangeweza kujengewa mashule, Zahanati, barabara Vijijini na kadhalika. Lakini fedha zote zinakwenda *TANESCO*, ruzuku ya mwezi mmoja kwa *TANESCO* ni sawasawa na gharama za barabara moja ya kiwango cha lami kati ya Mwandiga na Manyovu. Hivyo, rasilimali za nchi zinakwenda kwa wenye nacho, lakini walioingia Mkataba wa *NET GROUP* ni Watanzania, tunawajua au hatuwajui.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulibinafsisha Mashirika yetu ya Ndege *ATS* na vilevile Benki ya Biashara *NBC* na sasa inaitwa *ATCL* na Benki ya Biashara inaitwa *NBC Limited*. Tulitarajia kuwa, ubinafsishaji ungeweza kutuletea nafuu, tulitarajia kupata ndege zaidi lakini matokeo yake Makaburu wakachukua ndege kutoka kwao na kuikodisha kwa Kampuni yetu na sio makampuni yao ya *South African Air Ways*.

Njia za ndani za ndege zimekufa, ndege za *DAS8* zilikodishwa kutoka Afrika Kusini wakati tungeweza kukodisha kutoka ndege ya Serikali ya *F28*. Leo *ATC* haiendi Tabora, Dodoma, Shinyanga wala Kigoma. Mfumo mzima wa tiketi upo Afrika Kusini. Kodi inayotumika sasa ya 0183 ambayo ipo katika tiketi ya *ATC* ni ya Afrika Kusini na si yetu ile ya 0197. *NBC* nayo ina vituko vya ajabu hata ukitaka *Bank Statement Balance* ni lazima kwanza ipatikane kutoka Afrika Kusini, siku mtandao haupo shughuli zote za Benki zinasimama. Hata kitabu cha Benki tu ni lazima kusubiri wiki mbili kutoka Afrika Kusini.

Hakuna duniani nchi ya aina hii! Tumepata hasara, hakuna hatua zinazochuliwa, wahusika ni matajiri sasa, wengine wana majumba hata Pretoria, mali ya umma haina mwenyewe, nchi inapukutika, tunalaumu wageni wakati sisi ndio tunaofuja nchi. Tunawajua, historia inaandika, watoto wetu watatuhukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekodisha uwanja wa *KIA* kwa dola 1000 kwa mwaka, uwanja hauendelezwi, mwekezaji kadanganya nchi. Mwekezaji *KANTICO* amekuwa tajiri mno kwani kila siku anapata dola 5000 kutoka *KLM* peke yake inaposhuka tu pale *KIA*. Kila unaponunua tiketi kwenda Arusha au Moshi kuna fedha unampa mwekezaji huyu. Sasa ameanza kukodisha ardhi kwa Watanzania wanaolima pale, kwa eka Sh. 20,000/=, tuko kimya. Rasilimali zetu zinaliwa, wachache wanatajirika, haya hatuyaoni. Wabunge wameomba waone Mkataba wa *KIA*, Serikali haitaki, nini kinafichwa? Kambi ya Upinzani inaomba maelezo ya kina kuhusu kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TIC* bado ina changamoto kubwa. Ni lazima tutumie pesa nyingi kujitangaza. Kuna ushindani mkubwa katika kila nchi kujitangaza. Wengine hata Majimbo hujitangaza, lazima tuchangamke sasa katika ulimwengu huu wa ushindani, kama tunataka wawekezaji wa maana ni lazima tujitangaze.

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi na malengo ya mipango ya muda wa kati wa bajeti 2006/2007/2008/2009. Kwa aya mbili napitia misingi ya malengo mapana kama ilivyowasilishwa na Waziri na pia mpango wenyewe na kisha natoa mapendekezo ya mpango wa muda wa kati ili kukuza uchumi wetu na kuondoa umaskini ambao umetufukarishia wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uchumi wa mwaka jana 2005 si sawa na wa mwaka huu 2006, wakati huu. Wakati Mheshimiwa Waziri mwaka jana anasema hali ya uchumi mwezi Juni, alikuwa anaongea katika mazingira tofauti ya kiuchumi. Hivyo, misingi ya malengo mapana ya mpango na bajeti pia yalikuwa tofauti. Haiwezi kuwa tofauti sana, lakini haiwezi kuwa sawa kwa kila kitu. Hivyo, Mheshimiwa Waziri mwaka huu amefanya kunakili misingi ile ile ya mwaka jana kana kwamba hali ni sawa. Ni lazima tuwe makini.

Moja ya misingi ambayo nilitarajia Mheshimiwa Waziri angeitaja ni pamoja na kutoendelea kupanda kwa bei za mafuta, utabiri wa hali ya hewa na kudhibitiwa kwa mfumuko wa bei ambao unatishia kutengamaza uchumi mkuu, yaani *macro economic stability*. Pia, kutafsiriwa kwa MKUKUTA kivitendo katika kila Halmashauri ya Wilaya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika malengo ya uchumi kwa jumla, Waziri pia amerudia malengo yale yale aliyoyataja Waziri Kigoda bila kuzingatia hali ya sasa kwa mfano Waziri mwaka jana 2005 alitarajia uchumi kukua kwa asilimia 63 mwaka 2007 na Mheshimiwa Waziri mwaka huu pia hivyo hivyo. Hata hivyo, hili ni jambo ambalo haliwezekani, kwani mwaka huu uchumi utakuwa kwa asilimia 7.9 tofauti na alivyokadiria Kigoda mwaka jana kuwa uchumi ungekuwa asilimia saba.

Vilevile, kwa upande wa kasi ya kupanda bei, matarajio ya Waziri sio sahihi, kwani hayazingatii hali ya uchumi ya sasa. Ni vyema sasa tuweke malengo yetu katika hali halisi na Mawaziri waepuke kunakili hotuba za miaka ya nyuma ili kuepuka makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya kufikia malengo ya MKUKUTA, kama nilivyosema hapo awali…..

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kuhusu utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Nilitaka nimwachie Mheshimiwa Mbunge mpaka amalize hotuba yake, lakini nimeona ni vizuri nikasema hapa kuhusu utaratibu, Kanuni ya 50(1) ambayo inasema, "Ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni, kwa sababu hiyo Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni atawajibika kuwa na hakika kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu."

Sasa Mheshimiwa Mbunge wakati anaongea, amesema kuna watu wana majumba Pretoria waliohusika na mkataba. Sasa kufuatana na kanuni hiyo, mimi namhitaji atoe uthibitisho ama afute kauli yake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, una uwezo wa kuthibitisha au unafuta maneno haya? Kama unaweza kuthibitisha tutakupa muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafuta kauli yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mitatu wataalam wa umaskini wanasema, iwapo Sekta ya Kilimo ikikua kwa wastani wa asilimia 10, umaskini utapungua kwa asilimia 50. Kwa hiyo, tunapendekeza masuala yafuatayo yafanyike ili kuweza kukuza uchumi wetu.

Kwanza kuongeza uzalishaji kwa mkulima mdogo. Mkulima mdogo aweze kuzalisha zaidi katika ekari alizonazo hata kwa sasa. Kwa kuwa hatuna uwezo wa kupandisha bei mkakati wetu uwe ni wingi wa mazao, yaani *volume* badala ya bei *prices*.

Pili, kuongeza uzalishaji, ipo chini ya uwezo wetu; kupanga, ipo nje ya uwezo wetu.

Tatu, kila Halmashauri ya Wilaya iweke mpango kutafsiri lengo hili la kuongeza uzalishaji. Pia, tunapendekeza kugawa nchi katika kanda za umwagiliaji. Hatuwezi kumsaidia mkulima kama ataendelea kutegemea mvua, maji ya Ziwa Victoria yasitumike kwa kunywa tu, bali yatumike kwa kilimo katika Mikoa ya Shinyanga na hatimaye yafike Singida.

Maji ya ziwa Tanganyika yafike Tabora na mito yote mikubwa itumike kwa umwagiliziaji. Dhana ya sasa ya umwagiliziaji katika mabonde ipanuke zaidi, tufikishe

mifereji ya maji Vijijini ili uzalishaji uongezeke. Mpango wa kufikisha maji ya kumwagilia Vijijini ni ghali sana, lakini inawezekana kama inavyopendekezwa hapa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapendekeza kuongeza Maafisa Ugani Vijijini kwa kuwasomesha wahitimu wa Kidato cha Nne katika kila Kijiji ili wawe Maafisa Ugani Wasaidizi kutokana na aina ya kilimo katika Wilaya husika. Halmashauri za Wilaya ziweke mipango hii. Vilevile, tunapendekeza kuifanya Sekta ya Madini kutumika kutumikia Sekta ya Kilimo, Sekta ya Madini ndio sekta inayokua sana, lakini inachangia kidogo katika pato la Taifa. Sekta ya Madini haina mahusiano mazuri na sekta nyingine *strong forward and backward linkages,* hivyo faida ya sekta hii haiwezi kuwafikia wananchi kwani wamiliki wa madini ni wachache na mchakato wa madini ni wa mashine za kisasa. Hivyo ajira zinazotengenezwa ni kidogo sana.

Tunashauri kwamba Sera na Sheria za Madini zibadilike na kuifanya Serikali ikusanye mapato mengi zaidi katika madini. Kwa mfano mrahaba kufikia japo asilimia 10 ya mauzo ya madini, fedha za Sekta ya Madini ziendeleze Sekta ya Kilimo, Taifa liamue makusudi kabisa kuwa katika mrahaba wa asilimia tatu, itengwe mahususi kwa ajili ya kuendeleza kilimo na asilimia hiyo iweze kuendeleza Sekta ya Madini ikilenga zaidi wachimbaji wa kati na wadogo kwa lengo la kuwafanya Watanzania wafaidi rasilimali ya maendeleo. Pia tunapendekeza kufanya Sekta ya Utalii kuitumikia Sekta ya Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imeteuliwa kupata msaada kupitia Shirika la *Millenium Challenge Coorparation* linaloendesha mradi wa *Millenium Challenge Account*. Nchi imepatiwa jumla ya dola milioni 11 ili kuimarisha juhudi za kupambana na rushwa kama sehemu ya kufikia vigezo ya kupata msaada huu.

Hata hivyo, tumeshuhudia misaada mingi ya kimataifa kuishia maneno yaleyale ya nchi, matokeo yake *impact* haionekani. Kwa kuwa tumechagua maeneo ya miundombinu, nishati na maji kama maeneo ya kuelekeza msaada wa *MCC* wa jumla ya Dola milioni 700, yaani Shilingi bilioni 840. Basi msaada huu uelekezwe katika Mikoa ya pembezoni mwa nchi ili kuifungua na kuifanya ishiriki katika kukuza uchumi wa nchi. Mikoa hiyo ni Kigoma, Tabora, Rukwa, Ruvuma, Pwani na Pemba, yaani Kaskazini na Kusini Pemba. Tukifanya hivi tutaona dhahiri matokeo ya msaada huu kutoka Marekani na tunapendekeza sekta zibakie hizo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa nchi yetu inamkataba na msaada na Nchi ya Jumuiya ya Ulaya wenye thamani ya *EURO* milioni 355, yaani Shilingi bilioni 532, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Ulaya *EDEF* 19. Mkataba huu unaisha Desemba, 2007. Kupitia mkataba huu tumepata msaada wa miundombinu kama barabara ya Tinde Isaka, *Mandela Road,* Morogoro, Dodoma na ukarabati wa Bandari ya Zanzibar. Hata hivyo, kwa sasa tupo katika mjadala wa mkataba mpya ambao tumepangiwa kupata jumla ya *EURO* milioni 444 ambayo ni sawasawa na Shilingi bilioni 666. Bado hatujaamua vipaumbele vyetu viwe wapi, lakini tunapendekeza pia misaada hii ya kimataifa iende kwenye maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya jumla kwa kumalizia hotuba yangu, Kambi ya Upinzani inapendekeza masuala yafuatayo:-

Miradi ya kilimo nchini iwekwe chini ya utaratibu mmoja badala ya sasa ambayo Wizara ya Kilimo na Chakula haina uratibu wa miradi yote. Miradi ya kilimo imezagaa Wizara nyingi. Hii haifai, kwani msimamizi wa sera ya kilimo ni Wizara ya Kilimo, utaratibu wa sekta unasaidia sana kuhakikisha rasilimali za kilimo zinatumika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna uvujaji mkubwa wa mapato ya Serikali ama kwa Serikali kupoteza mapato au kwa watumishi wa Serikali kufuja fedha za umma. Tafiti zinaonyesha kuwa ufujaji mkubwa unatokea katika Serikali za Mitaa na hasa kwa Sekta za Elimu na Afya. Utafiti wa *LEPOA* unaonyesha kuwa kufujwa kwa fedha kunasababishwa hasa na fedha kutopelekwa katika shughuli zinazotoa huduma kwa jamii na badala yake fedha nyingi hupelekwa katika shughuli kama za utawala, masurufu ya safari na warsha.

Pia, sehemu kubwa kubwa ya fedha za umma zinakwenda kwa Maafisa wa Serikali na hata viongozi kama *allowance*. Waziri Kivuli wa Fedha anasoma mpango wa kupata mapato kutoka katika matumizi hayo, *allowances* muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasema sasa Tanzania ijiunge na *COMESA* ili wafanyabiashara wafaidike na unafuu wa kodi kwa bidhaa wanazouza nje katika *COMESA*. Hatuwezi kuendelea kuvumilia hasara tunayopata kuwa nje ya *COMESA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka Tanzania sasa ijadili mashirikiano mapya ya biashara na nchi za Jumuiya ya Ulaya kupitia kundi la *ESA* ili kuifanya Jumuiya ya Afrika Mashariki na pia kupata faida katika soko kubwa la nchi za *ESA*. Uamuzi huu pia utatuweka katika nafasi nzuri ya kushika masoko ya bidhaa katika kilimo katika nchi za Burundi, Rwanda na Mashariki ya *Congo DRC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kwamba iwapo mipango hii tunaliyoiainisha itafanyiwa kazi, matokeo ya ukuaji wa uchumi yataonekana kwa mwananchi mmoja mmoja Kijijini na Mijini. Hili ndio lengo la MKUKUTA, hili ndio lengo letu sote, kumwinua Mtanzania kiuchumi .

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. HAMADI RASHID MOHAMED (MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba upokee shukrani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2006/2007 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1) toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwa kauli moja, kunikubali kuwa niendelee kuwaongoza katika Bunge lako Tukufu. Nawaahidi kutumia ujuzi na uzoefu mdogo nilionao kuwaongoza kwa uadilifu mkubwa, nikiamini kuwa chini ya Uongozi wako Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wa Upinzani na Wabunge wote kwa pamoja tutasaidiana katika kuwatumikia Watanzania kwa lengo kuu la kuwaondolea umasikini uliokithiri, maradhi na ujinga pamoja na kujenga utaifa wetu wa dhati. Mwenyezi Mungu aziweke pamoja na kuzibariki nia zetu katika kutekeleza azma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba nikishukuru Chama Changu na Wapiga Kura wa Jimbo la Wawi kwa kunipa kura nyingi katika Uchaguzi uliopita na hadi leo kuwa ni mmoja wa Viongozi wao. Nawaahidi, kwa uwezo wa Mola sitawaangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 14.06.2006 Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alifanya mazungumzo na Wabunge wa CCM na hatimaye Wabunge wa Upinzani. Katika Kikao hicho, pamoja na mambo mengine mengi, Rais aliendelea kutoa ahadi yake ya kuumaliza mpasuko wa kisiasa ulioko Zanzibar na kusema, “Tumeishaanza, siyo rahisi sana lakini tutaumaliza.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani itaendelea kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais katika kuutafutia ufumbuzi mpasuko wa kisiasa wa Zanzibar pamoja na kero za Muungano, ila Kambi ya Upinzani ingelipenda kuweka bayana kwamba imani ya Watanzania hasa wa upande wa Zanzibar ni ndogo sana kutokana na ahadi kama hizo kutolewa na Rais aliyemtangulia na pia kutokutekelezwa kikamilifu kwa muafaka kati ya CCM na *CUF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais mwenyewe ameahidi kutembea kwenye maeneo yake, sisi Kambi ya Upinzani tunawaomba Watanzania wote wawe na imani na kauli ya Rais na sisi tunaahidi kuzidi kufuatilia utekelezaji wake huku tukielewa kuwa muda wa subira nao unazidi kuyoyoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzo huu aliouonyesha Rais Kikwete kukutana na Kambi ya Upinzani Bungeni kwa mazungumzo yanayohusu mustakabali wa Taifa letu, hayana budi kupongezwa na kuungwa mkono na wale wote wanaofahamu kuwa mdau wetu wote ni Mtanzania wa kawaida.

Tunamwomba Mheshimiwa Rais pia asiishie kukutana na Wabunge pekee, lakini pia akutane na wadau wote wa Siasa katika nchi yetu wakiwemo viongozi wa Vyama vya Siasa. Kitendo hicho cha Rais, kinadhihirisha wazi nia yake ya kujenga umoja wa Taifa letu, kuondoa ubaguzi kwa madhumini ya kupanua uwanja wa kidemokrasia na kumpa huduma Mtanzania bila kujali itikadi yake ya kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Zakhia Hamdan Meghji, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu pamoja na Manaibu wake, pamoja na Wakuu wa Vitengo na asasi zilizochini yao kwa kazi nzito ya maandalizi ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii fupi kuwakumbusha Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu kuwa, tokea nchi yetu ipate Uhuru, yaani Tanganyika mwaka 1961 kukawa na *Republic of Tanganyika* na baadaye Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964, kukawa na *People's Republic of Zanzibar* na hatimaye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi yetu imeongozwa na *TANU* na *ASP* na Hatimaye CCM.

Hivyo mafanikio na mapungufu yote ya maendeleo ya Nchi yetu yametokana na Uongozi na Sera za CCM, ambayo ni mrithi wa *TANU* na *ASP*.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu sote kujiuliza, katika kipindi chote cha uongozi wa aina moja; Je, Mtanzania wa kawaida maisha yake yameboreka kwamba sasa anaweza akapata angalau milo miwili bila ya wasiwasi? Anaweza akasomesha watoto wake na watoto wakasoma vizuri na hatimaye wakapata ajira? Anayo miliki ya ardhi kama ile alioachiwa na babu yake ambayo hawezi kunyang'anywa kwa tangazo la Redio? Anaweza kujiajiri kwa kupasua kokoto huku akiwa amechukua mkopo kwenye *SACCOS* yake akitegemea kusomesha watoto wake hatimaye anapigwa *stop* bila ya hata kupewa muda wa kujitetea kama walivyopewa muda wa kujirekebisha wala rushwa?

Je, anaweza kupata matibabu bila ya kulipia gharama kubwa? Anaweza kupata bei muafaka ya mazao yake kwa kuuza anakotaka kama ilivyokuwa kabla ya Uhuru na Mapinduzi? Je, hata anayefanya kazi amepata mshahara unaokidhi mahitaji yake? Tungeliweza kuuliza maswali zaidi, lakini nadhani imeeleweka tunataka kusema nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokumbushana haya, hatusemi kwamba Tanzania hakuna maendeleo au mabadiliko, lakini je, maendeleo hayo ni endelevu kiasi cha kumhakikishia Mtanzania kwamba baada ya Sera ya Kilimo ni Uhai ya Mwaka 1976. Je, tunajitosheleza kwa chakula cha kutosha na hata ukame ukitokea tuna chakula cha akiba? Au bado tunaendelea kuhemea chakula? Tuliwahi kuwa na hekta 450,000 za umwagiliaji, sasa zipo 260,000 tu, hayo ni maendeleo endelevu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu alituambia kupanga ni kuchagua. Je, kununua ndege kwa Shilingi bilioni 42 inayoweza kutua katika viwanja visivyozidi vitano katika nchi nzima na hasa kushindwa kutua Dodoma ambayo ni Makao Makuu ya nchi na Makao ya Bunge kwenye shughuli nyingi za kiserikali na za kibunge, ndege inayotumia wastani wa Shilingi milioni sita kwa saa ya kuruka na kuacha kuwatengenezea barabara wananchi wa Kusini ambao ni wazalishaji wakubwa wa Korosho na Muhogo. Au kuacha kujenga Zahanati zenye kuwanufaisha wananchi walio wengi, ni matumizi mazuri ya raslimali chache tulizonazo? Au ndio ule msemo wa kiswahili kwamba punda afe lakini mzigo ufike? Au kwa lugha tuliyoambiwa Bungeni kwamba hata Watanzania wakila nyasi lakini ndege lazima inunuliwe*? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni machache tu. Katika tathmini ya utekelezaji wa sera za kitaifa zinazosimamiwa na Chama Tawala kuna uuzaji wa hisa asilimia 25 ya mgodi wa almasi wa Mwadui kwa Dola za Marekani 184,521 tu, sawa na karibu Shilingi

za kitanzania milioni 200, fedha ambazo hata *PSRC* walishindwa kuthibitisha kama zilipokelewa na kama hiyo haitoshi kuwaruhusu wamiliki wakuu wa mgodi huo kutokulipa kodi hata tone hadi hii leo na hata gawio la hiyo asilimia 25 iliyobaki haijawahi kutolewa.

Tungependa kufahamu wakati wa kujibu hoja zetu, Mheshimiwa Waziri awaeleze Watanzania ni sababu zipi za Msingi zinamfanya Mheshimiwa Rais asiitumie Ndege hiyo mahususi iliyogharimiwa kwa fedha nyingi za Watanzania na bado Rais wetu anapanda lifti wakati Bunge lako Tukufu liliambiwa Rais wetu anahitaji kusafiri kwa raha mustarehe na bila kupata uchovu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nigusie kidogo kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine Serikali ililiambia Bunge kuwa ilikuwa inakusanya Shilingi trilioni 1.774, sawa na Shilingi bilioni 145 kwa mwezi. Hizi ni fedha nyingi japokuwa kama baadhi ya mianya ingezibwa na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na matumizi Serikali ingalipunguza kwa kiasi kikubwa bajeti tegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara na Idara sita tulizochambua, tumebaini kuna upungufu wa makusanyo wa mapato yasiopungua Shilingi bilioni nane, kinyume na kifungu cha kumi cha Sheria ya Fedha. Aidha, Shilingi bilioni 2.5 Wizara ya Mambo ya Nje imeshindwa kuziingiza *BOT* kutokana na mauzo ya *Visa* kinyume na *Circular* Na. 6 ya Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, upotevu wa fedha, Mfuko Mkuu wa Hazina Shilingi bilioni 1.8, *Police Force* Shilingi milioni 132, Kilimo Shilingi milioni 122 na Maliasili Shilingi milioni 155.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** *Yes*, kifungu cha 50, namsubiri akae chini.

Kifungu cha 50 (1) kinasema: "Ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni. Kwa sababu hiyo, Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni anawajibika kuwa na uhakika kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na siyo mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu." Sasa Mheshimiwa Mbunge anayesema, kasema pale katika ukurasa wa sita wa hotuba yake kwamba:

"Tungependa kufahamu wakati wa kujibu hoja zetu, Mheshimiwa Waziri awaeleze Watanzania ni sababu zipi za msingi zilizomfanya Rais asitumie ndege hiyo

mahsusi iliyogharamiwa kwa fedha nyingi za Watanzania na bado Rais wetu anapanda lifti wakati wa Bunge lako Tukufu liliambiwa Rais wetu anahitaji kusafiri kwa raha mustarehe na bila kupata uchovu.”

Sasa athibitishe hiyo lifti aliyoomba na kupata Rais wetu ni lini na wapi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge nilifikiri unakaa kwanza. *Ruling* ya Spika.

Mheshimiwa Mbunge ni kweli kifungu hiki kinasema hivyo. Kama unao ushahidi wa huyo Rais kuomba lifti tungefurahi kusikia, sijui ni lifti ya kwenda wapi!

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni tafsiri. Kwetu sisi tulipoambiwa Rais amenunuliwa ndege maalum, anapokuwa amepanda ndege nyingine tunachukulia kwamba ni lifti kwa maana kwamba imeachwa hasa ile ndege ya kupanda.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Hapana!

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hilo ni tatizo la tafsiri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WZIRI MKUU:** Sio sahihi kwa sababu Serikali ina ndege nyingi. Afute usemi wake ama atuambie aliomba lifti lini na wapi? Serikali ina ndege nyingi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani tafadhali uwe *brief,* maana yake kama ilikuwa lifti, ilikuwa ni lifti ya ndege ya nani? Lini na wapi? *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuondoa usemi. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa endelea na hoja zako.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, upotevu wa fedha Mfuko Mkuu wa Hazina. Hii ndiyo tathmini ya uwezo wa Serikali katika kusimamia mapato na matumizi ya Taifa letu. Kambi ya Upinzani kabla ya kuridhia Bajeti ya mwaka 2006/2007 inataka maelezo ya kina, juu ya upotevu huu na hatua zinazochukuliwa kwa wahusika kutoa fedha za wavuja jasho na kuepukana na bajeti tegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano pamoja na kuwa na sheria nzuri ya manunuzi, lakini Serikali imekiuka kwa makusudi na kuingia Mkataba na Kampuni ya Alex Stewart Asseyers kuchambua dhahabu inayozalishwa na kusafirishwa na Makampuni ya Madini Tanzania kwa gharama ya asilimia 1.9 ya mrahaba kutoka kwenye mrahaba wa asilimia tatu iliyopata Serikali. Hivyo, Serikali inapata asilimia 1.1 tu ya dhahabu yote inayosafirishwa nje. Hii ni biashara kichaa.

Mkataba wa Kampuni hii umeongezewa muda hadi mwaka 2007 na hivi asubuhi Naibu Waziri wa Nishati na Madini ametuthibitishia na wakati huohuo itakuwa imekusanya si chini ya *USD* milioni 65 maana katika kipindi hiki, tayari itakuwa imekusanya Dola milioni 30, fedha ambayo ingeweza kusaidia katika utoaji wa huduma za jamii kama Elimu na Miundombinu. Aidha, Serikali imeongeza Mkataba wa *Container Terminal TICS* kwa muda usiopungua miaka 10 zaidi bila ya kufuata utaratibu wa Sheria ya Manunuzi, yaani *Public Procurement Act*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani na Watanzania kwa ujumla tunahitaji maelezo ya kina katika eneo hili na hasa katika utaratibu mzima wa kuvunja ile sheria ya *Procurement Act*.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa kila mwaka kelele zinapigwa kuhusu misamaha ya kodi, bado hali haijawa nzuri. Zaidi ya asilimia 22.5 ya mapato hutolewa kama misamaha. Ni lazima tuandae utaratibu kwa mwaka huu kupunguza angalau asilimia 12 ya misamaha hiyo ili kupunguza Rushwa na bajeti tegemezi. Lakini pia kuwa na utaratibu ulio wazi zaidi wa kutoa misamaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2006/2007, kwa uchambuzi wetu, mfumo mzima wa Bajeti una mapungufu makubwa. Kwanza hauwashirikishi Wabunge katika maandalizi ya kupanga vipaumbele pamoja na kuwa Wabunge wanaishi Vijijini, wanakaa karibu kabisa na wananchi na ndiyo wenye kujua vipaumbele katika maeneo yao. Hili limesemwa vizuri na Mwenyekiti wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwetu mafungu ya Bajeti yanachukuliwa kwa ujumla tu na hivyo kuwafanya Wabunge kutokufahamu kwa kina matumizi ya mafungu hayo. Hii ni tofauti na nchi nyingine nyingi kama Zambia na Mauritius zinazofuata mfumo kama wa kwetu wa *CPA* ambapo hata mshahara wa Rais unaonyeshwa, Ziara za Rais zinajulikana katika kipindi cha mwaka mmoja ni ziara ngapi. Aidha, ziara zote za Mawaziri, Wabunge na Watumishi wote zinaorodheshwa na hivyo kuifanya kazi ya Wabunge ya kuisimamia Serikali kuwa rahisi lakini pia kuondoa mianya yote ya matumizi hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utaratibu wa Bajeti zetu za nyuma kuwa na mapungufu, Bajeti ya mwaka huu imefumbwafumbwa mno kiasi huwezi kujua ni kiasi gani cha punguzo kimeathiri mapato au ongezeko limemuongezea mzigo kiasi gani mlaji. Kwa mfano Bajeti ya 2005/06 ilionyesha wazi hatua inayochukuliwa na nyongeza au punguzo la mapato. Tazama Ukurasa wa 62 wa hotuba hiyo ya mwaka jana 2005.

Kinyume na Bajeti ya Mwaka huu, mfano halisi ni ukurasa wa 47 ambapo Waziri anataja hatua zilizochukuliwa kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa ya mafuta ya petroli. Lakini anataja tu viwango vipya bila kutaja vya zamani. Mwananchi wa kawaida au hata Mbunge ambaye hajachambua kwa makini hawezi kamwe kugundua madhara ya bajeti hii na ataendelea kuisifu kama baadhi ya watu walivyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe, ukurasa wa 46, kifungu 43 (1) Waziri haelezi kwa hatua hii atakayochukua itaipatia mapato ya ziada kiasi gani Serikali. Hivyo hivyo kwa kifungu cha (11) nacho haelezi kwa kuondoa msamaha wa kodi katika magari madogo utapunguza kiasi gani cha mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wakati tunakubaliana na kufutwa kwa *VAT* asilimia 20 kwenye bidhaa ya Petroli, haieleweki ni vipi Serikali ifute kodi ya thamani ya asilimia 20 kwenye bei ya mafuta ya petroli kodi ambayo ndio tegemeo kubwa ya Serikali halafu isiathiri mapato ya Serikali. Hiki ni kitendawili kinahitaji kutenguliwa. Wabunge na wananchi tunastahili kujua jinsi pengo hili litakavyozibwa ili isirudi kwa mlango wa nyuma kama ilivyotokea pia huko nyuma. Ni vyema pia Waziri akatueleza ni kiasi gani kilikuwa kinakusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila bajeti inayowasilishwa na Waziri wa Fedha, huzungumzia upanuzi wa wigo wa kodi, lakini kila mwaka tunashuhudia bidhaa zinazoongezwa kodi ni zile zile, vinywaji baridi, pombe na sigara. Bado serikali haijawa na maeneo mapana ya kukusanya kodi.

Aidha, Serikali haijawahi kueleza, kwa mfano ni vipi mkulima wa tumbaku atafaidika kama sigara ikiongezwa kodi ambayo inalipwa na mvutaji, lakini kiwanda kinachouza sigara hakimwongezei mkulima bei ya tumbaku yake. Ni vyema Serikali mbali na kupanua wigo wa kodi, lakini kwa maeneo ambayo mkulima anauza bidhaa zake kwenye viwanda ukatafutwa utaratibu wa kumwongezea bei. Utaratibu wa sasa ni wa kumnyonya mkulima wa kawaida sawa kama Mataifa yaliyoendelea yanavyotupangia

bei kwa bidhaa zinazotokana na mali ghafi ya kwetu. Sisi lazima tuonyeshe njia ili tuweze kudai haki zetu kwenye soko la kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalaumu soko la nje, lakini hata sisi wenyewe hapa ndani mfano mzuri ni soko la karafuu. Mkulima wa karafuu soko la nje ni Dola 3,500 kwa tani, wakati mkulima analipwa Dola 1,250 kwa tani. Katika kuongeza uwezo wa Wakulima iwe ni pamoja na kuuza walau wanakotaka, Serikali kuandaa mazingira mazuri ya soko huria kuepuka uholela, kupunguza kodi zinazopunguza uwezo wa mkulima, kuvunja hujuma za wafanyabiashara wakubwa wa mazao, yaani *cartel*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukurasa wa 31 wa kitabu cha bajeti kinaonyesha matumizi ya Shilingi bilioni 641 na Shilingi milioni 766 kwa ajili ya maendeleo kwa fedha zinazotokana na mapato ya ndani. Kati ya hizo, Shilingi bilioni 219,240 zimetengwa kwa miradi maalum ya kuzalisha umeme wa gesi na ukarabati wa miundombinu ya kusambazia umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa *TANESCO* kutokana na mikataba bomu inalipa *IPTL na SONGAs* jumla ya *USD* milioni 15.4 kwa mwezi kati ya mapato yake ya *USD* milioni 24 kwa mwezi. Hadi sasa *TANESCO* inadaiwa *USD* milioni 40 na *IPTL* na *SONGAs* kutokana na mikataba ya kuwaumiza Watanzania mbali na ziada ya *USD* milioni 60 ambazo Bunge hili mwaka jana 2005 liliwapatia. Hivi sasa *TANESCO* wanaiomba tena Serikali ruzuku ya *USD* milioni 200 ambazo Waziri anaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu umuhimu wa nishati katika maendeleo yetu. Lakini sisi Kambi ya Upinzani tunadhani kuwa hii mipango ya zimamoto haitamaliza matatizo ya *TANESCO*. Wakati umefika wa kupata *corporate plan* ya *TANESCO*, ili tuelewe hasa ni kiasi gani na kwa muda gani Serikali na Watanzania wataendelea kuliendesha Shirika la *TANESCO* nje ya gharama za umeme zinazopanda kila leo.

Kwa mujibu wa Sera ya Ubinafsishaji, tuliambiwa kuwa *NET GROUP SOLUTION* wamekuja kulinenepesha Shirika hilo ili litakapobinafsishwa liwe na bei nzuri. Je, limenenepa au kukonda kwa kiasi gani? Ili kuwalinda watumia umeme na kutoa kibali cha kutoa idhini ya fedha kwa Shirika linalofanya biashara, tunaitaka Serikali itoe kwa Bunge hili tathmini ya kina ya athari kwa uchumi wetu unaosababishwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili hili liende pia kwenye *Air Tanzania.* Serikali katika bajeti hii imetenga Shilingi bilioni 15 ili kutaka kuipatia *Air Tanzania.* Tunaomba *Cooperate plan* ya *Air Tanzania* ili Watanzania tusiendelee tu kutoa pesa ambazo hazipo katika mipango rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 32, Waziri ameelezea mgao wa fedha kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Shilingi bilioni 21,196 ambazo ni asilimia 4.5 kwa misaada kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais kwa kuelewa vyema matakwa ya Katiba, sura ya saba inayozungumzia kuweko kwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja na ambayo itachangiwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachokubaliwa na Tume ambayo katika Bunge la mwaka jana 2005 tuliahidiwa kuwa katika Bajeti hii *formula* itakuwa tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake wakati akilihutubia Bunge ukurasa wa 17 alisema, ninanukuu: "Nitaangalia upya mchango wa Serikali ya Muungano katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Zanzibar." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie:-

(a) Hii Shilingi bilioni 21,169 inatokana na misaada ya kiasi gani na ongezeko alilosema Rais katika hotuba yake ya Bungeni ni kiasi gani?

(b) Pia, Mheshimiwa Waziri atufafanulie: Je, mgao huu hauingiliani na ule wa Benki Kuu wa faida ambao pia unatumia *formula* isiyo sahihi ya asilimia 4.5 badala ya asilimia 11.02?

(c) Aidha, Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili, ni lini Tume ya pamoja ya fedha itakamilisha utaratibu wa mgao wa mapato na matumizi ya Muungano?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Serikali kwa kuzingatia mahitaji ya msingi ya Elimu, Afya na Maji. Elimu imetengewa asilimia 19 ukilinganisha na asilimia 16.1 ya bajeti iliyopita. Haidhuru, kuna haja ya kuangalia mfumko wa bei na mserereko wa Shilingi. Ni matumaini ya Kambi ya Upinzani kuwa fedha zitatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mkopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu bado ni kitendawili, kila wakati kumekuwa na maamuzi ya zimamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa mfuko huo hauna usimamizi mzuri na inawezekana kuna ubadhirifu mkubwa wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tunashauri mfuko huu ukabidhiwe kwa Benki itakayoshinda zabuni ya kuuendesha badala ya utaratibu wa sasa baada ya masharti ya Wazabuni kukubaliwa na wanataaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo. Katika Bajeti ya Waziri wa Fedha, ukurasa wa 31 mpaka 32 Waziri hakuweza kubainisha ni kiasi gani cha fedha kimetengwa mahususi kwa kilimo kama vile alivyofanya kwa Nishati, badala yake amechukulia tu kwamba kilimo kina uhusiano na Wizara nyingi. Ni vyema Mheshimiwa Waziri akakumbuka kuwa Serikali iliahidi katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za *SADC* kuwa kilimo kitapewa asilimia 10 ya Bajeti ya nchi mwanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti hii, Kilimo kimepewa asilimia 3.2 ambayo ni chini ya ile ya mwaka jana ya asilimia 3.9. Mfumuko wa bei ni asilimia tano ya Shilingi na Shilingi inazidi kuserereka. Kambi ya Upinzani inaona hii ni hali ya hatari kwa Sekta nzima ya Kilimo ambayo mchango wake ni asilimia 45.6 katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakulima wa Tanzania wamekuwa kama watoto wa kambo. Wakati wa Azimio la Arusha, ilitamkwa kwamba, njia kuu za uchumi zitamilikiwa na Umma kwa kupitia Mashirika ya Umma na Vyama vya Ushirika. Wakati huo Ushirika Tanzania ulikuwa unaongoza Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ulipoonekana una nguvu, ulitaifishwa na hata Benki yao na raslimali zao zilitaifishwa, wakulima wakarudi nyuma kuwa omba omba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatimaye ikaundwa Jumuiya ya Ushirika chini ya Chama. Mimi nilikuwa mmoja wa Viongozi, nilikuwa Naibu Katibu Mkuu, siasa ikaingilia Ushirika, hadi leo haujasimama sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Vyama vya Kuweka na Kukopa *SACCOS* vimeanza kujikongoja, kama chombo mbadala baada ya Wakulima kutaifishwa Benki yao. Vyama hivi, baadhi yake vimeanza kufanikiwa. Kwa mfano, Kibaigwa, Gairo, Wawi, Mikumi, Soko Kuu *Morogoro SACCOS*; *Mshikamano SACCOS Bank* na Mtibwa *Outgrowers Association SACCOS.* Nina hakika mafanikio yaliyofikiwa mnayafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama hivi vimeanza kupata matatizo ya Kisera, vimeanza kutakiwa kuchangia mbio za mwenge, makaribisho yasiyozingatia Bajeti za Vyama, riba kubwa zinazotozwa na Mabenki, Semina zinazoshinikizwa na Maafisa wa Ushirika bila kujali Bajeti za Vyama.

Pia, kanuni ya 39(4) ya 2004 ya Vyama vya Ushirika, kama ilivyonukuliwa na Mrajis wa Vyama aya 5.3 ya Waraka FA.65/105/01/65 wa tarehe 16 Mei, 2005 ina tatizo. Kanuni hii inataja Kamati ya Uchaguzi yenye mamlaka ya Kuchuja majina ya Wagombea. Hii ni *Political affiliation* nyingine kama ile ya Washirika. Hii ni kupunguza nguvu za wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inashauri kwamba ni vyema sheria itamke wazi kuwa Vyama vya Ushirika ni mali ya wanachama na maamuzi ni yao, Maaofisa wa Ushirika kazi yao ni kuvilea, kuvikagua na kutatua migogoro. Siasa zisiingilie Vyama vya Ushirika.

Serikali iendelee kutoa Elimu kwa wanachama kujiunga zaidi na hadi sasa ni asilimia 0.9 Watanzania waliojiunga na *M.F.I.*, yaani *Micro Finance Institution* kuongeza mitaji zaidi ili *SACCOS* zipunguze utegemezi wa mabenki ambayo baadhi yao yanatoza riba ya asilimia 15.

Kwa *SACCOS* zinazofanya vizuri Serikali itoe ruzuku ya kutosha, *Substantial Grant* au *Revolving Fund* na *formula* iwe ni mtaji wa wanachama, Akiba, Amana na Hisa mara mbili, hii itaondoa utegemezi na riba itaweza kushuka.

Serikali igharimie Semina na Vyama visimamie mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi na Makarani wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu inaweza kuvisimamia vyombo vya fedha ili zisaidie kuzilea *SACCOS*. Hakuna njia kwa uchumi kukua kwa kasi kama Benki Kuu itashindwa kusimamia riba na mserereko wa thamani ya fedha yetu. Hivyo, mipango yote ya kuondoa umasikini itakuwa ni nadharia tu. Urari wa biashara utaendelea kuwa nakisi, hasa kwa vile mauzo yetu nje ni kidogo kuliko tunavyoagizishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inarudia wito wake wa miaka zaidi ya minne sasa, hatuwezi kamwe kumkomboa Mtanzania na jembe la mkono. Tuliomba Serikali ianzishe Vituo vya Trekta kwenye Kanda mbalimbali, wananchi wakodishiwe Trekta. Kama walivyoanzisha Mapdre Benedictini Mtwara lakini walikatishwa tamaa na Serikali kwa kuweka Kodi kwenye ukodishaji huo wa trekta. Kama alivyopendekeza pia Padre Benedictini aliyeko Lushoto kuwa sehemu ya *Fuel levy* inayopatikana itumike katika kusaidia mradi huo wa ukodishaji, mpango ambao tuliuwasilisha kwa Waziri wa Kilimo aliyepita, lakini haukufanyiwa kazi.

Tunaitaka Serikali kama imedhamiria na inaitambua Sekta ya Kilimo kama uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania, haraka iwezekanavyo tuanzishe utaratibu huo. Kwani nchi yenye mabonde makubwa kama Bonde la Rufiji, Bonde la Ruvuma, Bonde la Malagarasi na mengine mengi yanaweza kutukomboa katika janga la njaa. Japan ambayo ni ndogo sana lakini leo inatugawia chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha Shilingi bilioni 318 badala ya 682 zilizotengwa 2005/2006 hadi kufikia Shilingi trilioni moja na milioni nne 4 kwa ajili ya mishahara, ajira ya Waalimu, afya, Wahasibu na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichambua upungufu wa watumishi katika Sekta ya Elimu, Afya, Uhasibu, wakaguzi na watumishi wengine, ni dhahiri kiwango cha mshahara kitakachoongezwa kitakuwa ni kidogo mno. Kwani sehemu kubwa ya fedha hizi zitatatumika kwa mishahara inayotokana na ajira mpya katika sekta hizo na siyo kuwa itatumika katika kuboresha tu mishahara kama wengi walivyoelewa.

Ukiangalia gharama za mfanyakazi, kodi ya nyumba, usafiri, umeme, maji, kusomesha watoto, chakula na kadhalika ni dhahiri kitakachoongezwa hakitoshi, ukitilia maanani kuwa Rais Kikwete aliahidi kutoa ajira zisizopungua 200 kwa kila mwaka yaani aliahidi milioni moja kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona wazi kuwa bila kuathiri Bajeti, Serikali ina uwezo wa kuwalipa wafanyakazi kima cha chini cha TSh.300,000/= kwa mwezi bila ya kuathiri bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia fungu la matumizi ya *Employment Allowances* mara nyingi fungu hili huzidi fungu la mishahara halisi ya wafanyakazi. Mathalan, katika *Program No.10, Vote 30* Ofisi ya Rais, kifungu kidogo cha 1001 mishahara ni shilingi 373,760,000 na Watumishi wasio na *Pension* ni 60,915,000 wakati *Employment Allowance* ni 921,996.000.

Cha kusikitisha ni kuwa *Employment Allowance* huwanufaisha tu viongozi wa ngazi za juu ambao pia wana huduma za ziada mathalan nyumba, usafiri, simu, umeme, maji, *furniture* na kadhalika. Lakini watumishi wa chini ambao hawanufaiki na chochote hawapati kitu. Hali hii iko karibu, hivyo katika Wizara zote mfumo huu hautendi haki, hauna tija wala motisha kwa watumishi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hesabu za harakaharaka, kwa Wizara sita nilizoangalia, *Employment Allowance* imechukua takriban asilimia 3.7 ya jumla ya matumizi yote ya Serikali ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiogopa ushauri huu wa kuunganisha *Employment Allowances* kwenye mshahara, au hata kuchukua asilimia hamsini tu (50) yake na kuiweka kwenye mshahara wa watumishi wote kwa uwiano wa sifa zao, ambao tumekuwa tukiutoa kila mwaka kwa kukwepa kulipa kiinua mgongo kikubwa mfanyakazi anapostaafu, bila ya kuangalia manufaa yafuatayo:-

Kwanza hakutakuwa na kada ya wafanyakazi ambao hawalipi kodi. Sasa hivi tuna viwango vya wafanyakazi wanaopata kiwango cha mshahara wa Shilingi 60 mpaka 80 hawalipi kodi. Kundi hili litaondoka kwa utaratibu huu.

Pili, Mifuko ya pensheni itapata wanachama zaidi kwa sababu watu wengi watakuwa wamepata kazi ya kuajiriwa.

Tatu, Kodi ya Serikali ambayo ni ya uhakika *Pay As You Earn* itapanda maradufu kwani *Employment Allowance* hivi sasa haitozwi kodi.

Nne, wafanyakazi watakuwa na kipato kitakachowapa moyo kufanya kazi, hivyo kuongeza ufanisi kazini na mengine mengi ambayo ni pamoja na kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Uwezeshaji, tunampongeza Waziri kwa kuainisha mipango ya uwezeshaji ikiwa ni pamoja na *SACCOS* ambazo tayari tumekwishaziongezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Dhamana. Mbali na kwamba unahitaji kuboreshwa kwa kuondolewa urasimu wake, bali pia unahitaji kupanuliwa kwa kuwa na sera inayosema: “Kila Kinachoweza Kutuingizia Fedha za Kigeni Kithaminiwe.” Yaani hivi sasa kuna mazao fulani tu ndiyo yanadhaminiwa. Kama tunataka kweli kuongeza

mapato yetu ya fedha za kigeni, basi kila Mtanzania anayeweza kusafirisha nje bidhaa yake iweze kudhaminiwa. Hiyo nafikiri ndiyo itatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wigo wa kuzalisha umeme, tunaweza tu kujitosheleza kwa umeme kama tutakuwa na *program* maalum ya kujua hasa tunahitaji kuwekeza kiasi gani cha mradi wa umeme kupitia *TANESCO*, pili ni nishati itokanayo na jua, upepo, mawimbi ya bahari, mimea, mbegu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya nishati ya mafuta kwa nchi yetu yanaendelea kuwa makubwa sana kutokana na umuhimu wake katika mzunguko mzima wa uchumi wa nchi yetu. Kutokana na tafiti zilizofanywa, inakisiwa kuwa mahitaji hayo ya nishati ya mafuta kwa kipindi cha miaka mitano ijayo mpaka 2010 yatakuwa tani za ujazo milioni 2.37. Wakati mahitaji kwa mwaka yanakisiwa kuwa ni tani milioni 1.2 na kati ya hizo, Sekta ya Usafirishaji inatumia 40%, Sekta ya Viwanda inatumia 25%, Sekta ya Kilimo inatumia 10%, Sekta ya Biashara 5% na matumizi ya nyumbani 10% na matumizi mengine 10%.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati ya mafuta itokanayo na mazao ya kilimo katika nchi yetu bado ni mpya kwa Watanzania walio wengi japokuwa nishati hii inaweza kuzalishwa na kuongeza kipato kwa Taifa na wananchi wake kwa kuzingatia kuwa mazao yanayozalisha nishati hii yanazalishwa takribani eneo zima la nchi yetu. Mazao hayo ni mawese, nazi, korosho, pamba, miwa na jatropha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Soko la Dunia la *ethanol* bidhaa inayopatikana kabla ya kupata nishati ya *biofuel* inapanda kati ya 2%-3% kwa mwaka. Matumizi ya *ethanol* katika Soko la Dunia inategemea kupanda hadi kufikia lita milioni 41.5 kwa mwaka huu wa 2006. *Ethanol* inapatikana katika mazao yote niliyoyataja hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna viwanda vinne vikubwa vya sukari na mabaki baada ya kuzalisha sukari (*bagasse*) na kwa ujumla viwanda vyetu vina uwezo wa kuzalisha karibu tani 500,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia teknolojia kutoka Ufaransa, Mauritus, wanaozalisha wastani wa tani 650,000 za sukari, wanazalisha umeme wa asilimia 45 ya mahitaji yao kutokana na mabaki ya miwa. Hivi sisi tumeshindwa kujifunza hata kutoka nchi za *SADC* ambazo sisi ni wanachama wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Vitambulisho, sheria ya kuanzisha vitambulisho ilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka 1987 karibu sasa miaka 19.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoshauri katika hili ni kwamba Idara ambazo zinatumia vitambulisho, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Uhamiaji, Polisi, *TRA* na kadhalika zianzishe Mfuko wa Pamoja ili gharama hizi ziweze kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya nyumba, tunaipongeza Serikali hatimaye imesikiliza kilio cha Wabunge cha kudai Benki ya Maendeleo, ambayo itatoa mikopo ya muda mrefu katika kilimo, ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri *T.I.B* mbali na kupewa milioni 50, lakini Benki Kuu iwakopeshe kwa riba isiyozidi asilimia mbili kama bilioni 100 ili kuwa na mtaji wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki za Biashara, Benki hizi bado zinatoza *commission* kubwa, *commissio*n ya asilimia moja kwa mtu anayeomba mkopo, akiomba bilioni moja inamtaka alipe Shilingi milioni 10. Uukichukua na riba anazolipa mtu huyo hawezi kuchukua mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, riba kwa mikopo ni ya juu sana inafika hadi 25% wakati mfumuko wa bei ni chini ya asilimia saba ya riba ya mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba vilevile Benki Kuu ndiyo chanzo cha kuwa na riba kubwa. Hivi sasa *Commercial rate* ya Benki Kuu kuwakopesha mabenki mengine ni asilimia 17. Tunashauri kwamba asilimia hii iteremke ili mabenki mengine yaweze kutoa mikopo kwa riba ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri Mifuko ya Hifadhi za Jamii nayo iundiwe chombo cha kuratibu kwani mifuko hii sasa inatoa mikopo kama vyombo vya fedha wakati haimo katika mfumo wa vyombo vya fedha. Kwa hiyo, ni vizuri vikawekewa utaratibu ili visitoe mikopo na kunufaisha wachache badala ya kunufaisha wafanyakazi wanaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa madini kwa Taifa letu bado ni kitendawili. Makampuni mengi ukishawauzia mgodi huo, sio tena mali ya Watanzania. Ndio maana wawekezaji hao huuza migodi hiyo bila hata kuiarifu Serikali, maana wanaona ni mali yao. Kilicho chetu ni mrahaba na kidogo huduma tunazotoa ambazo hivi sasa kampuni ya nje ndiyo yanakuja kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ule mrahaba mdogo tuliokuwa tunaupata wa asilimia tatu, sasa hivi asilimia 1.9% ya mrahaba huu inapewa Kampuni ambayo inatufanyia *(assey)* kama tulivyoambiwa hivi sasa asubuhi ambayo tunamwomba Mheshimiwa Waziri atupatie maelezo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kumalizia, naomba Waziri atuelezee mambo yafuatayo:-

Moja, ubia wa Benki Kuu katika mradi wa *Mwananchi Gold Co.Ltd.* Wana hisa ngapi, ni akina nani, na mtaji wao ni kiasi gani?

Pili, Benki Kuu kama *Regulator* anaruhusiwa kuingia kwenye hisa?

Tatu, Kampuni ya Dhahabu ya MEREMETA ilianzishwa kwa lengo la kukisaidia kiwanda cha Nyumbu. Je, Lengo hilo bado liko au halipo na sasa hivi kampuni hii inamilikiwa na nani na Serikali ina hisa ngapi ?

Nne, chombo ambacho kingeweza kuwasaidia wachimbaji wadogo na wa kati ni *STAMICO*. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa *STAMICO* ichukuliwe kama *SIDO* kwa kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo na wa kati, kwani hao ndio watakaotuonyesha faida ya kuwa na raslimali za madini na sio makampuni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za Serikali za kuhifadhi mazingira, Serikali imeongeza ushuru kwenye mifuko ya *plastic* kutoka asilimia 15% hadi 120%. Katika ahadi zilizotolewa wakati wa Kampeni za kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anakunywa maziwa. Je, kwa kuongeza kodi hii, yale maziwa tunayonunua kwenye paketi na maji tunayokunywa kwenye paketi hayataathirika na hivyo kuendeleza kipindupindu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pamoja na kupiga kelele muda mrefu kuhusu haki za Walemavu, kwa mara nyingine imesikitishwa kuona kuwa hadi leo Bajeti haina mtazamo maalum kwa ajili ya Walemavu. Hata ndani ya Bunge letu, japo ujenzi kwa kiasi fulani umezingatia mahitaji ya Walemavu, lakini mahitaji mengi ya walemavu hayajazingatiwa, mathalani *Braille machine*, maalum vya kusomea, kuelewa alama mbalimbali kama za vyombo vya mawasiliano.

Pamoja na hayo, Serikali yetu hadi leo haijaridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu maslahi yao, yaani *International Standard Rules on the Equalization of Opportunities to persons with disabilities* wa Umoja wa Mataifa, *No.48* wa 1996. Kambi ya Upinzani inahimiza Serikali ichukue hatua ya haraka kuridhia Mkataba huo na kuingiza katika utekelezaji ili Watanzania hao wapate haki zao hususan kama tunavyopata sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, pamoja na wananchi kutokutupa kura za kutosha au kama walitupa lakini hazikuonekana, bado tutaendelea kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima wa mpango wa Serikali na Chama kilichoko madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Tunangoja maelezo ili tuweze kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaanza wachangiaji Wabunge wengine. Ataanza Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, atafutiwa na Mheshimiwa Mgana Msindai. Nadhani Mheshimiwa Omar Kwaang’w atakuwa wa tatu.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutumia nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuweza kushirikiana na wenzangu katika kuchangia hoja hii ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji pamoja na ya Waziri wa Fedha.

Kwanza kabisa ningependa kutumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Spika na wewe kwamba kwa kweli siyo jengo tu humu tulimo, lakini wewe mwenyewe na Mheshimiwa Spika, mmewezesha Ukumbi huu kuwa na mandhari inayofanana na Awamu ya Nne pamoja na Bunge hili la karne ya 21. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa kutumia nafasi hii kumshukuru Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Waziri wa Fedha kwa hotuba zao nzuri ambazo kwa mimi binafsi na nina hakika Waheshimiwa Wabunge wengi tumezielewa.

Vilevile ningependa kusema kuwa bajeti hii kwa sisi Waheshimiwa Wabunge wa CCM nimeamini kwamba imezingatia kwa uhalisi kabisa sera za Chama chetu pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya 2005. Labda mimi niwatoe wasiwasi baadhi ya watu hasa wanaofikiri kwamba mambo haya hayawezekani. Bajeti hii imetolewa kwa misingi ile ile ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Kwa hiyo, wale waliozoea kubabaisha kwa kutokufanya kazi waanze kujiandaa kwa sababu miguu yao itavunjika maana *speed* haitakuwa ndogo. *(Makofi)*

Mimi naamini Waheshimiwa Wabunge sisi tutakuwa wa kwanza kuhakikisha kwamba bajeti hii inatekelezwa. Katika hili, mimi naomba niseme bila kuona haya kwamba suala la kuleta maendeleo ya nchi hii haiwezekani tukamuachia mtu mmoja anaitwa Rais. Ni kazi ya kila mmoja wetu, kila Mtanzania na hasa Viongozi. Ndugu zangu pia Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani wanawajibu wa kuleta maendeleo katika Majimbo yao na ninawashauri ili wafanye vizuri wakasome Ilani ya CCM itawasaidia. *(Makofi)*

Pili, ningeomba tusifute historia. Kwa mfano, mimi nimpongeze kwanza ndugu yangu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, tulikuwa wote pamoja Bungeni. Kwanza, *Afro Shiraz* na *TANU* na baadaye CCM. Yote haya tunayoyaona hapa yanatokana na kazi nzuri zilizofanywa na Vyama vile na yeye anastahili kujipongeza kwa kazi hiyo, maana haifai kujiondoa katika historia.

Kama tulifanya hovyo, mimi ninaomba mtakapopanga watu waliofanya hovyo mniweke na mimi mstari mmoja na waliowahi kufanya hovyo. Kama tulifanya vizuri naomba mtupongeze na ndugu yangu Hamad Rashid Mohamed asijitoe. Kwa sababu tungefanyaje hapa bila kuwa na mwanzo ule? Hatuwezi kujitoa kwa mema na mazuri yaliyofanyika siku za nyuma. Kama mlivyosikia, yeye yenyewe alishapata kuwa Katibu Mkuu wa *CUT* na ni mafanikio makubwa kwa historia yake na atakapoandika historia hawezi kujiondoa katika jambo hili. Kwa hiyo, niliona niseme jambo hili ili wote tuelewane. *(Makofi)*

Vilevile, kuna maelezo yamesemwa hapa kuhusu ndege, watu wazima tutarudiaje kila Bunge jambo lile lile? Kila Bunge tukikutana ugomvi ni ndege tu, wagonjwa wa mambo yaliyopita. Ndege ilishanunuliwa, hivi tutarudisha ndege Marekani tukadai fedha!? Sisi ni watu wazima hapa Bungeni, watu wanaotusikia watatushangaa kweli!

Maana sisi Waheshimiwa Wabunge tulikuwepo na hata ndugu yangu alikuwepo, tulishakubaliana na tulikuwa wote kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi ulishapitisha ndege imenunuliwa. Hivi inawezekanaje leo badala ya kuzungumza mambo ya kwenda mbele tunaanza kubishana juu ya ndege!

Halafu pia ningependa niseme kwa ajili ya wanaotusikiliza tu, Mbunge ukisema jambo humu ndani, kanuni zikasema kwamba umekosea au umesema uongo, hata ukifuta bado ni uongo. Kwa sababu watu wameshasikia. Sasa haifai watu wazima mmekuja huku mmejiandaa kusema uongo, mnapata fedheha ya bure mbele ya Bunge. Kwa hiyo, nataka niseme hata kwa watu wazoefu. *(Makofi)*

Pili, nataka niseme rasmi kwa baadhi, labda ambao hawakuwa wamepata habari.......

**NAIBU SPIKA:** Ni kwamba ukisema unafuta, unathibitisha kwamba ulikuwa ni uongo kweli.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tena naomba radhi, uliposimama ningekaa, nilikuwa sijakuona. Nakuomba radhi.

Kwa hiyo, nataka niseme ndugu zangu kwamba katika Bara la Afrika lote mwaka 2004 yalifanyika mashindano ya vyombo vinavyoshughulikia uwekezaji kama hiki cha kwetu *Tanzania Investment Centre*.

Kwa Bara lote la Afrika zilichujwa nchi 11 zikabakia tatu. Zilipokwenda kwenye mchujo wa mwisho, Tanzania kwa chombo chake hiki cha Tanzania *Investment Centre* ambacho *Executive Boss* wetu alikuwa ni Mheshimiwa Spika wetu wa sasa, ndiye alipata zawadi ya kwanza katika Afrika nzima. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba tupongezane. Mambo haya mema hayawezi kuwa ya Serikali peke yake bila sisi wote. Sifa ya nchi haiwezi kuwa sifa ya CCM, inakuwa ya nchi na nchi ni Vyama vyote. Kwa hiyo, naomba sifa hii tuibebe wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, ningependa niseme mambo mawili pia. Moja, ambalo ni kubwa kwangu siwezi kulisahau ni kuwa mimi ni miongoni mwenu waliochaguliwa kuwa Wabunge wa mwaka 2005. Ninaomba niwashukuru wananchi wa Kwela kwa kunichagua kuwa Mbunge wao tena. Nitakuwa natimiza kipindi cha miongo mitatu katika Jimbo hilo. *(Makofi)*

Lakini vilevile, ningependa kutumia nafasi hii vilevile, kuwashukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa imani yake juu yangu. *(Makofi)*

Baada ya hayo, ningependa nitoe mapendekezo moja kwa moja bila kuchelewa. La kwanza, haya yote yaliyo katika Ilani, nataka nirudie sasa nilisema nitaeleza. Mimi naamini yatatekelezwa kwa sababu mbili. Moja, sisi Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM tulipokwenda kuomba kura tulikuwa tunatembea na Ilani. Kwa hiyo, tutaisaidia

Serikali yetu kwenda kutafsiri kwa vitendo kwa wananchi waliotuchagua maana kazi ya kuleta maendeleo hatuwezi kumuachia Rais peke yake wala Waziri Mkuu peke yake.

Lakini nataka nieleze wale tuliokuwepo zamani. Zamani ilikuwa kwa mfano tunasema tutakuwa na sherehe ya kumbukumbu labda ya jambo fulani kwa miaka miwili katika Mkoa fulani, majengo yote haya, kwa mfano kiwanja hiki cha Dodoma kilijengwa kwa ajili ya sherehe na kazi ile ya kujenga kile kiwanja ilifanyika miezi sita tu.

Juzi Waziri Mkuu wetu hakufanya majaribio, alidhamiria akasema anataka watoto waliobaki kutokwenda Shule za Sekondari wajenge madarasa mapya watoto waende Shule za Sekondari. Zaidi ya asilimia 50 ya wanafunzi waliobaki wamejengewa madarasa na wanakwenda Shule za Sekondari. Watu ni wale wale! Kinachotakiwa ni kuwa na mipango na usimamizi mzuri.

Nataka niseme hasa kwa watu wa Serikali wa Mikoani wajihadhari sana. Sitaki kukufuru kwa Mwenyezi Mungu, mimi nilifanya kazi na Marehemu Moringe Sokoine, kuna wakati Marehemu Moringe Sokoine alikuwa ananipigia simu usiku saa saba, naamka naanza kuzungumza naye kwa muda wa saa mbili usiku.

Sasa nataka niwajulisheni ninavyomfahamu Edward Ngoyai Lowassa. Watendaji wa Serikali jiandeni! Mtajuta kweli mkifanya ubabaishaji. Kwa hiyo, mimi naamini yatafanywa haya.

**MBUNGE FULANI:** Kweli kabisa!!

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Maana mimi nimeishi naye na tumefanya kazi pamoja. Mambo ya simu za usiku yanaanza kurudi, jiandeni watekelezaji. Lakini ili tufike huko, ushauri wangu kwa Serikali, naomba nchi ichorwe kwa Kanda za Maendeleo ili malengo yawekwe.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waziri Mkuu, naomba msikubali Mikoa hata Wizara kuendesha maendeleo kwa hotuba. Kama tuna mpango na Ilani ipo na sera zipo, Mikoa yote itakiwe kutengeneza mipango yao ya maendeleo kwa kutumia *profiles* zao walizonazo, kwa sababu kila Mkoa una utajiri wake tofauti na Mkoa mwingine. Sasa Mikoa yote ilitakiwa siku nyingi itayarishe *profiles* zake, mambo yanayowezekana katika Mikoa yao. Sasa yale yatengenezewe mipango na programu za utekelezaji ili kila Mkoa uwajibike kueleza wamefanya nini katika kutekeleza Ilani isiwe mambo ya jumlajumla. Huo ndio ushauri wangu.

Vilevile, tukichora Kanda za nchi tutaweza kutafsiri kwa usahihi nani wataitosheleza nchi kwa chakula. Kwa mfano, Rukwa, Ruvuma, Iringa na Mbeya tuko tayari kulisha nchi na kuuza nje. Kwa kweli nikisema juu ya Morogoro nitakuwa nakufuru maana niliishi huko. Morogoro ndiyo iweze kulisha nchi peke yake. Lakini, sitaki kusema zaidi nyie wenyewe mnaelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachosema ni kuwa sasa tubanane kwa malengo, watu wawajibike, lakini tuchore Kanda. Kwa mfano, kama nilivyosema Mikoa ile minne ili twende tuwakaribishe viongozi wetu, tuwe nanyi tupange mipango na mbolea na pembejeo zinazotolewa wazitoe kwa malengo hayo isiwe bila hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, napendekeza kwamba uwezeshaji wa wananchi uwe kwa Wizara zote. Wizara zote zitengeneze sheria na kanuni ya namna ya kuwawezesha wananchi.

Tatu, tulipitisha sheria ya uwezeshaji kwa kuchukua hisa 21 za Benki ya *NMB* ziende kwa wananchi. Iko hapa sheria, inasema Serikali itakuwa na hisa 30, wawekezaji watakuwa na hisa 49 na wananchi watakuwa na hisa 21. Naomba Serikali muanze kuziuza hisa za *NMB* sasa. Ama moja kwa moja, ama tuitumie *Unit Trust* ifanye kazi ya kuuza hisa kwa sababu hakuna kuchelewa. Hisa hizi ni za wananchi na ni haki yao, iko ndani ya Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninatoa ushauri kwamba Wizara yenyewe ya Nishati na Madini wawe na maeneo ambayo yametambuliwa yana dhahabu ili sasa inapotokea kuna mwekezaji Serikali imwelekeze mahali pa kwenda kuwekeza ili kuondoa ugomvi huu. Kwa sababu hata taarifa ambayo ndugu yangu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati wa Madini alisema hapa juzi Bungeni, mimi sikubaliani. Alisema kwamba Wizara ina watu wanaofuatilia jiolojia, ripoti zinazotolewa na *investors,* siyo kweli.

Mimi ninao ushahidi kwamba mnadanganywa Wizara na nina *documents* za kuonyesha kwamba mnadanganywa. Wale wawekezaji wa madini wote wanakuwa na taarifa mbili. Moja ni ya kwao na nyingine siyo yenu wanabana ile yenye mali sahihi wanawaletea ya kawaida tu na wanasema hawawezi kuleta kwenu ya siri kwa sababu ya *confidentiality* , wana mashaka watu wenu wanaweza kuuza hizo habari kwa watu wengine. Mimi nina ushahidi na mkitaka niwaletee makampuni ambayo yamewadanganya ninayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mkitaka usahihi, maeneo ya madini yawe ya Serikali ili Serikali ndio ielekeze watu kwenda kuwekeza. Pili, mimi nashauri toka sasa Serikali iwe inaingia hisa. Siwezi kusemea migodi iliyokwishaanza, Serikali inajua jinsi itakavyofanya. Lakini kwa migodi ijayo mimi naomba Serikali yenyewe iwe na hisa, tusiwaachie hawa utajiri wa nchi. Wao wana teknolojia, wana fedha na sisi tuna dhahabu, basi tuungane. Sisi tuna dhahabu na wao wana pesa, twende pamoja 50 kwa 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nimekuta kule Botswana wanajenga mgodi mkubwa sana wa Almasi, wao ni 50 na *De beers* ni 50. Kwa hiyo, ndiyo namna ya kuweza kwenda pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu vilevile, nataka kuishauri Serikali na mimi nina hakika tutafanya vizuri sana, na wananchi wana imani kubwa sana na Serikali ya

Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wana imani kubwa na hii bajeti imedhihirisha kabisa. *(Makofi)*

Sasa ni lazima vilevile tuwe na mianya ya kubana matumizi. Mimi nina hakika kwamba Serikalini sasa magari ni mengi kuliko mahitaji na magari, yanaleta gharama kubwa. Mimi naomba turudie utaratibu wa zamani. Magari yote ya Serikali yawe kwenye *pool*. Kila Wizara iwe na *pool*. Watu wa kupewa magari ya Serikali wawe ni wenye *entitlement* ya kupewa gari kwamba ajira ya Waziri ni kupewa gari, ajira ya Katibu Mkuu wa Wizara ni kupewa gari. Sasa wale wengine waende wakapewe gari kwenye *pool*. Leo ukiona kwa mfano, watu wanatoka Dar es Salaam kuja Dodoma, mtu mmoja anapanda gari moja na anatoka Wizara hiyo hiyo na mwingine kutoka Wizara hiyo hiyo naye anapanda gari lake. Kwa hiyo, magari yatakuja 10 kutoka Wizara moja na kila gari amepanda mtu mmoja. Sasa haiwezekani mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani mimi nilipokuwa nafanya kazi, tulikuwa tunapanga ratiba tunampelekea Mkuu wa Wilaya. Kwa hiyo, Mkuu wa Wilaya anaagiza anasema Idara fulani na Idara fulani mtakwenda eneo fulani wote. Kwa hiyo, Maofisa wanne, watano mnasafiri kwa gari moja kwenda kufanya kazi ya wananchi, kwa sababu sisi wote shabaha ni wananchi. Lakini leo kila mtu anataka kwenda na gari lake, tena gari lenyewe ni shangingi wala siyo gari ndogo ndogo. Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali itusaidie namna ya kubana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ningependa niseme kuhusu takwimu. Mimi narudia kuhusu takwimu. Naomba Serikali ijitahidi kuleta takwimu ambazo zinaonyesha tulikotoka na tunakokwenda. Kwa mfano, takwimu alizoleta Mheshimiwa Waziri mimi nimezipenda, lakini mimi ningependa ziwe zinalinganishwa.

Kwa mfano, kama tunasema tulipanda miti milioni tano, sasa tuseme lengo lilikuwa ni miti mingapi? Tusilinganishe na miti iliyopandwa mwaka jana, hapana. Tulinganishe lengo la miti ya kupanda na iliyopandwa siyo kulinganisha na iliyopandwa kipindi kilichopita. Maana hata ile ukisema ilipandwa miti milioni tano, hautuambii kabla ya kupandwa miti milioni tano lengo lilikuwa kupandwa miti mingapi kwanza. Kwa hiyo, tuwe na malengo ili kipimio kilinganishe lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie bajeti ya mwaka huu. Nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali pale ilipoona wenzetu wanasema uongo wakasahihisha. Nawapongeza sana. Kama mwenzangu alivyosema hapa Bungeni siyo mahali pa kusema uongo. Kwa hiyo, kote kwa wenzetu Wapinzani na sisi Chama Tawala tujiangalie tusiseme uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wenzetu wa *TRA*, pamoja na shida kubwa wanayoipata lakini kila mwaka wamekuwa

wanavuka malengo na wao ndiyo wanatuwezesha tunaongea mambo haya. Niwapongeze sana, waendelee na juhudi hizo ili mapato yetu yaongezeke zaidi. Lakini ningewaomba wanisaidie kitu kimoja na waende wakakifanyie kazi.

Ukienda kwenye maduka mengi unataka kununua *TV* au kitu kingine unaambiwa kama hutaki risiti bei yake ni 300,000/=, lakini kama unataka risiti bei yake ni 400,000/=, hivi hizi bidhaa huwa zinaingiaingiaje? Kwa hiyo, nawaomba waende wakalifanyie kazi, lazima kuna dosari mahali waisahihishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hiyo, sasa nirudie kwenye kitabu chenyewe na ninaomba twende ukurasa wa 41. Naipongeza sana Serikali kwa kurudisha ushuru wa asilimia 10 kwa ajili ya mbegu za mafuta na kwa ajili ya mafuta ya wenzetu yanayotoka nje. Kwa kweli kurudisha huo ushuru wakulima wa alizeti, wakulima wa mawese watafaidika kwa sababu watapata bei nzuri na ninaomba hilo Serikali isije ikalifuta tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, mimi nimeshangaa sana kuona mafuta ya ndege yamefutiwa kodi, lakini mafuta ya taa ambayo wananchi wengi wanayatumia hayakufutiwa kodi. Hivi ni wananchi wangapi hapa Tanzania wanapanda ndege? Ndege zenyewe zina migogoro, viwanja vibovu.

Kwa hiyo, mimi ningeiomba Serikali itafute njia nyingine ifute kodi kwenye mafuta ya taa na hiki chanzo ikitafute katika eneo lingine. Sasa hivi tunalinda mazingira yetu, wananchi wanasumbuliwa wakichoma mkaa, lakini wakipata mafuta ya taa kwa bei nafuu itawasaidia zaidi. Kwa hiyo, hilo mimi naiomba Serikali iliangalie ili kuwasaidia wananchi wake. *(Makofi)*

La pili, nashukuru kupunguza kodi kwenye gesi na hiyo ni kwa ajili ya wenzetu wa Mijini. Kule Iramba Mashariki au Monduli hii kitu haiwasaidii kwa sababu gesi haiwezi kwenda kwenye nyumba ya tembe au nyumba ya nyasi, italeta maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa na hii nimeisema kwa makusudi sijaona bei ya bati na bei ya saruji ipunguzwe. Wananchi wetu wanajitahidi Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya nishati ya mafuta kwa nchi yetu yanaendelea kuwa makubwa sana kutokana na umuhimu wake katika mzunguko mzima wa uchumi wa nchi yetu. Kutokana na tafiti zilizofanywa, inakisiwa kuwa mahitaji hayo ya nishati ya mafuta kwa kipindi cha miaka mitano ijayo mpaka 2010 yatakuwa tani za ujazo milioni 2.37. Wakati mahitaji kwa mwaka yanakisiwa kuwa ni tani milioni 1.2 na kati ya hizo, Sekta ya Usafirishaji inatumia 40%, Sekta ya Viwanda inatumia 25%, Sekta ya Kilimo inatumia 10%, Sekta ya Biashara 5% na matumizi ya nyumbani 10% na matumizi mengine 10%.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati ya mafuta itokanayo na mazao ya kilimo katika nchi yetu bado ni mpya kwa Watanzania walio wengi japokuwa nishati hii inaweza kuzalishwa na kuongeza kipato kwa Taifa na wananchi wake kwa kuzingatia kuwa mazao yanayozalisha nishati hii yanazalishwa takribani eneo zima la nchi yetu. Mazao hayo ni mawese, nazi, korosho, pamba, miwa na jatropha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Soko la Dunia la *ethanol* bidhaa inayopatikana kabla ya kupata nishati ya *biofuel* inapanda kati ya 2%-3% kwa mwaka. Matumizi ya *ethanol* katika Soko la Dunia inategemea kupanda hadi kufikia lita milioni 41.5 kwa mwaka huu wa 2006. *Ethanol* inapatikana katika mazao yote niliyoyataja hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna viwanda vinne vikubwa vya sukari na mabaki baada ya kuzalisha sukari (*bagasse*) na kwa ujumla viwanda vyetu vina uwezo wa kuzalisha karibu tani 500,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia teknolojia kutoka Ufaransa, Mauritus, wanaozalisha wastani wa tani 650,000 za sukari, wanazalisha umeme wa asilimia 45 ya mahitaji yao kutokana na mabaki ya miwa. Hivi sisi tumeshindwa kujifunza hata kutoka nchi za *SADC* ambazo sisi ni wanachama wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Vitambulisho, sheria ya kuanzisha vitambulisho ilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka 1987 karibu sasa miaka 19.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoshauri katika hili ni kwamba Idara ambazo zinatumia vitambulisho, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Uhamiaji, Polisi, *TRA* na kadhalika zianzishe Mfuko wa Pamoja ili gharama hizi ziweze kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya nyumba, tunaipongeza Serikali hatimaye imesikiliza kilio cha Wabunge cha kudai Benki ya Maendeleo, ambayo itatoa mikopo ya muda mrefu katika kilimo, ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri *T.I.B* mbali na kupewa milioni 50, lakini Benki Kuu iwakopeshe kwa riba isiyozidi asilimia mbili kama bilioni 100 ili kuwa na mtaji wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki za Biashara, Benki hizi bado zinatoza *commission* kubwa, *commissio*n ya asilimia moja kwa mtu anayeomba mkopo, akiomba bilioni moja inamtaka alipe Shilingi milioni 10. Uukichukua na riba anazolipa mtu huyo hawezi kuchukua mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, riba kwa mikopo ni ya juu sana inafika hadi 25% wakati mfumuko wa bei ni chini ya asilimia saba ya riba ya mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba vilevile Benki Kuu ndiyo chanzo cha kuwa na riba kubwa. Hivi sasa *Commercial rate* ya Benki Kuu kuwakopesha mabenki mengine ni asilimia 17. Tunashauri kwamba asilimia hii iteremke ili mabenki mengine yaweze kutoa mikopo kwa riba ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri Mifuko ya Hifadhi za Jamii nayo iundiwe chombo cha kuratibu kwani mifuko hii sasa inatoa mikopo kama vyombo vya fedha wakati haimo katika mfumo wa vyombo vya fedha. Kwa hiyo, ni vizuri vikawekewa

utaratibu ili visitoe mikopo na kunufaisha wachache badala ya kunufaisha wafanyakazi wanaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa madini kwa Taifa letu bado ni kitendawili. Makampuni mengi ukishawauzia mgodi huo, sio tena mali ya Watanzania. Ndio maana wawekezaji hao huuza migodi hiyo bila hata kuiarifu Serikali, maana wanaona ni mali yao. Kilicho chetu ni mrahaba na kidogo huduma tunazotoa ambazo hivi sasa kampuni ya nje ndiyo yanakuja kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ule mrahaba mdogo tuliokuwa tunaupata wa asilimia tatu, sasa hivi asilimia 1.9% ya mrahaba huu inapewa Kampuni ambayo inatufanyia *(assey)* kama tulivyoambiwa hivi sasa asubuhi ambayo tunamwomba Mheshimiwa Waziri atupatie maelezo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kumalizia, naomba Waziri atuelezee mambo yafuatayo:-

Moja, ubia wa Benki Kuu katika mradi wa *Mwananchi Gold Co.Ltd.* Wana hisa ngapi, ni akina nani, na mtaji wao ni kiasi gani?

Pili, Benki Kuu kama *Regulator* anaruhusiwa kuingia kwenye hisa?

Tatu, Kampuni ya Dhahabu ya MEREMETA ilianzishwa kwa lengo la kukisaidia kiwanda cha Nyumbu. Je, Lengo hilo bado liko au halipo na sasa hivi kampuni hii inamilikiwa na nani na Serikali ina hisa ngapi ?

Nne, chombo ambacho kingeweza kuwasaidia wachimbaji wadogo na wa kati ni *STAMICO*. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa *STAMICO* ichukuliwe kama *SIDO* kwa kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo na wa kati, kwani hao ndio watakaotuonyesha faida ya kuwa na raslimali za madini na sio makampuni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za Serikali za kuhifadhi mazingira, Serikali imeongeza ushuru kwenye mifuko ya *plastic* kutoka asilimia 15% hadi 120%. Katika ahadi zilizotolewa wakati wa Kampeni za kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anakunywa maziwa. Je, kwa kuongeza kodi hii, yale maziwa tunayonunua kwenye paketi na maji tunayokunywa kwenye paketi hayataathirika na hivyo kuendeleza kipindupindu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pamoja na kupiga kelele muda mrefu kuhusu haki za Walemavu, kwa mara nyingine imesikitishwa kuona kuwa hadi leo Bajeti haina mtazamo maalum kwa ajili ya Walemavu. Hata ndani ya Bunge letu, japo ujenzi kwa kiasi fulani umezingatia mahitaji ya Walemavu, lakini mahitaji mengi ya walemavu hayajazingatiwa, mathalani *Braille machine*, maalum vya kusomea, kuelewa alama mbalimbali kama za vyombo vya mawasiliano.

Pamoja na hayo, Serikali yetu hadi leo haijaridhia Mkataba wa Kimataifa unaohusu maslahi yao, yaani *International Standard Rules on the Equalization of Opportunities to persons with disabilities* wa Umoja wa Mataifa, *No.48* wa 1996. Kambi ya Upinzani inahimiza Serikali ichukue hatua ya haraka kuridhia Mkataba huo na kuingiza katika utekelezaji ili Watanzania hao wapate haki zao hususan kama tunavyopata sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, pamoja na wananchi kutokutupa kura za kutosha au kama walitupa lakini hazikuonekana, bado tutaendelea kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima wa mpango wa Serikali na Chama kilichoko madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Tunangoja maelezo ili tuweze kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaanza wachangiaji Wabunge wengine. Ataanza Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, atafutiwa na Mheshimiwa Mgana Msindai. Nadhani Mheshimiwa Omar Kwaang'w atakuwa wa tatu.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutumia nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuweza kushirikiana na wenzangu katika kuchangia hoja hii ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji pamoja na ya Waziri wa Fedha.

Kwanza kabisa ningependa kutumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Spika na wewe kwamba kwa kweli siyo jengo tu humu tulimo, lakini wewe mwenyewe na Mheshimiwa Spika, mmewezesha Ukumbi huu kuwa na mandhari inayofanana na Awamu ya Nne pamoja na Bunge hili la karne ya 21. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa kutumia nafasi hii kumshukuru Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Waziri wa Fedha kwa hotuba zao nzuri ambazo kwa mimi binafsi na nina hakika Waheshimiwa Wabunge wengi tumezielewa.

Vilevile ningependa kusema kuwa bajeti hii kwa sisi Waheshimiwa Wabunge wa CCM nimeamini kwamba imezingatia kwa uhalisi kabisa sera za Chama chetu pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya 2005. Labda mimi niwatoe wasiwasi baadhi ya watu hasa wanaofikiri kwamba mambo haya hayawezekani. Bajeti hii imetolewa kwa misingi ile ile ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Kwa hiyo, wale waliozoea kubabaisha kwa kutokufanya kazi waanze kujiandaa kwa sababu miguu yao itavunjika maana *speed* haitakuwa ndogo. *(Makofi)*

Mimi naamini Waheshimiwa Wabunge sisi tutakuwa wa kwanza kuhakikisha kwamba bajeti hii inatekelezwa. Katika hili, mimi naomba niseme bila kuona haya kwamba suala la kuleta maendeleo ya nchi hii haiwezekani tukamuachia mtu mmoja anaitwa Rais. Ni kazi ya kila mmoja wetu, kila Mtanzania na hasa Viongozi. Ndugu zangu pia Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani wanawajibu wa kuleta maendeleo katika

Majimbo yao na ninawashauri ili wafanye vizuri wakasome Ilani ya CCM itawasaidia. *(Makofi)*

Pili, ningeomba tusifute historia. Kwa mfano, mimi nimpongeze kwanza ndugu yangu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, tulikuwa wote pamoja Bungeni. Kwanza, *Afro Shiraz* na *TANU* na baadaye CCM. Yote haya tunayoyaona hapa yanatokana na kazi nzuri zilizofanywa na Vyama vile na yeye anastahili kujipongeza kwa kazi hiyo, maana haifai kujiondoa katika historia.

Kama tulifanya hovyo, mimi ninaomba mtakapopanga watu waliofanya hovyo mniweke na mimi mstari mmoja na waliowahi kufanya hovyo. Kama tulifanya vizuri naomba mtupongeze na ndugu yangu Hamad Rashid Mohamed asijitoe. Kwa sababu tungefanyaje hapa bila kuwa na mwanzo ule? Hatuwezi kujitoa kwa mema na mazuri yaliyofanyika siku za nyuma. Kama mlivyosikia, yeye yenyewe alishapata kuwa Katibu Mkuu wa *CUT* na ni mafanikio makubwa kwa historia yake na atakapoandika historia hawezi kujiondoa katika jambo hili. Kwa hiyo, niliona niseme jambo hili ili wote tuelewane. *(Makofi)*

Vilevile, kuna maelezo yamesemwa hapa kuhusu ndege, watu wazima tutarudiaje kila Bunge jambo lile lile? Kila Bunge tukikutana ugomvi ni ndege tu, wagonjwa wa mambo yaliyopita. Ndege ilishanunuliwa, hivi tutarudisha ndege Marekani tukadai fedha!? Sisi ni watu wazima hapa Bungeni, watu wanaotusikia watatushangaa kweli!

Maana sisi Waheshimiwa Wabunge tulikuwepo na hata ndugu yangu alikuwepo, tulishakubaliana na tulikuwa wote kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi ulishapitisha ndege imenunuliwa. Hivi inawezekanaje leo badala ya kuzungumza mambo ya kwenda mbele tunaanza kubishana juu ya ndege!

Halafu pia ningependa niseme kwa ajili ya wanaotusikiliza tu, Mbunge ukisema jambo humu ndani, kanuni zikasema kwamba umekosea au umesema uongo, hata ukifuta bado ni uongo. Kwa sababu watu wameshasikia. Sasa haifai watu wazima mmekuja huku mmejiandaa kusema uongo, mnapata fedheha ya bure mbele ya Bunge. Kwa hiyo, nataka niseme hata kwa watu wazoefu. *(Makofi)*

Pili, nataka niseme rasmi kwa baadhi, labda ambao hawakuwa wamepata habari.......

**NAIBU SPIKA:** Ni kwamba ukisema unafuta, unathibitisha kwamba ulikuwa ni uongo kweli.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tena naomba radhi, uliposimama ningekaa, nilikuwa sijakuona. Nakuomba radhi.

Kwa hiyo, nataka niseme ndugu zangu kwamba katika Bara la Afrika lote mwaka 2004 yalifanyika mashindano ya vyombo vinavyoshughulikia uwekezaji kama hiki cha kwetu *Tanzania Investment Centre*.

Kwa Bara lote la Afrika zilichujwa nchi 11 zikabakia tatu. Zilipokwenda kwenye mchujo wa mwisho, Tanzania kwa chombo chake hiki cha Tanzania *Investment Centre* ambacho *Executive Boss* wetu alikuwa ni Mheshimiwa Spika wetu wa sasa, ndiye alipata zawadi ya kwanza katika Afrika nzima. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba tupongezane. Mambo haya mema hayawezi kuwa ya Serikali peke yake bila sisi wote. Sifa ya nchi haiwezi kuwa sifa ya CCM, inakuwa ya nchi na nchi ni Vyama vyote. Kwa hiyo, naomba sifa hii tuibebe wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, ningependa niseme mambo mawili pia. Moja, ambalo ni kubwa kwangu siwezi kulisahau ni kuwa mimi ni miongoni mwenu waliochaguliwa kuwa Wabunge wa mwaka 2005. Ninaomba niwashukuru wananchi wa Kwela kwa kunichagua kuwa Mbunge wao tena. Nitakuwa natimiza kipindi cha miongo mitatu katika Jimbo hilo. *(Makofi)*

Lakini vilevile, ningependa kutumia nafasi hii vilevile, kuwashukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa imani yake juu yangu. *(Makofi)*

Baada ya hayo, ningependa nitoe mapendekezo moja kwa moja bila kuchelewa. La kwanza, haya yote yaliyo katika Ilani, nataka nirudie sasa nilisema nitaeleza. Mimi naamini yatatekelezwa kwa sababu mbili. Moja, sisi Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM tulipokwenda kuomba kura tulikuwa tunatembea na Ilani. Kwa hiyo, tutaisaidia Serikali yetu kwenda kutafsiri kwa vitendo kwa wananchi waliotuchagua maana kazi ya kuleta maendeleo hatuwezi kumuachia Rais peke yake wala Waziri Mkuu peke yake.

Lakini nataka nieleze wale tuliokuwepo zamani. Zamani ilikuwa kwa mfano tunasema tutakuwa na sherehe ya kumbukumbu labda ya jambo fulani kwa miaka miwili katika Mkoa fulani, majengo yote haya, kwa mfano kiwanja hiki cha Dodoma kilijengwa kwa ajili ya sherehe na kazi ile ya kujenga kile kiwanja ilifanyika miezi sita tu.

Juzi Waziri Mkuu wetu hakufanya majaribio, alidhamiria akasema anataka watoto waliobaki kutokwenda Shule za Sekondari wajenge madarasa mapya watoto waende Shule za Sekondari. Zaidi ya asilimia 50 ya wanafunzi waliobaki wamejengewa madarasa na wanakwenda Shule za Sekondari. Watu ni wale wale! Kinachotakiwa ni kuwa na mipango na usimamizi mzuri.

Nataka niseme hasa kwa watu wa Serikali wa Mikoani wajihadhari sana. Sitaki kukufuru kwa Mwenyezi Mungu, mimi nilifanya kazi na Marehemu Moringe Sokoine, kuna wakati Marehemu Moringe Sokoine alikuwa ananipigia simu usiku saa saba, naamka naanza kuzungumza naye kwa muda wa saa mbili usiku.

Sasa nataka niwajulisheni ninavyomfahamu Edward Ngoyai Lowassa. Watendaji wa Serikali jiandeni! Mtajuta kweli mkifanya ubabaishaji. Kwa hiyo, mimi naamini yatafanywa haya.

**MBUNGE FULANI:** Kweli kabisa!!

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Maana mimi nimeishi naye na tumefanya kazi pamoja. Mambo ya simu za usiku yanaanza kurudi, jiandeni watekelezaji. Lakini ili tufike huko, ushauri wangu kwa Serikali, naomba nchi ichorwe kwa Kanda za Maendeleo ili malengo yawekwe.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waziri Mkuu, naomba msikubali Mikoa hata Wizara kuendesha maendeleo kwa hotuba. Kama tuna mpango na Ilani ipo na sera zipo, Mikoa yote itakiwe kutengeneza mipango yao ya maendeleo kwa kutumia *profiles* zao walizonazo, kwa sababu kila Mkoa una utajiri wake tofauti na Mkoa mwingine. Sasa Mikoa yote ilitakiwa siku nyingi itayarishe *profiles* zake, mambo yanayowezekana katika Mikoa yao. Sasa yale yatengenezewe mipango na programu za utekelezaji ili kila Mkoa uwajibike kueleza wamefanya nini katika kutekeleza Ilani isiwe mambo ya jumlajumla. Huo ndio ushauri wangu.

Vilevile, tukichora Kanda za nchi tutaweza kutafsiri kwa usahihi nani wataitosheleza nchi kwa chakula. Kwa mfano, Rukwa, Ruvuma, Iringa na Mbeya tuko tayari kulisha nchi na kuuza nje. Kwa kweli nikisema juu ya Morogoro nitakuwa nakufuru maana niliishi huko. Morogoro ndiyo iweze kulisha nchi peke yake. Lakini, sitaki kusema zaidi nyie wenyewe mnaelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachosema ni kuwa sasa tubanane kwa malengo, watu wawajibike, lakini tuchore Kanda. Kwa mfano, kama nilivyosema Mikoa ile minne ili twende tuwakaribishe viongozi wetu, tuwe nanyi tupange mipango na mbolea na pembejeo zinazotolewa wazitoe kwa malengo hayo isiwe bila hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, napendekeza kwamba uwezeshaji wa wananchi uwe kwa Wizara zote. Wizara zote zitengeneze sheria na kanuni ya namna ya kuwawezesha wananchi.

Tatu, tulipitisha sheria ya uwezeshaji kwa kuchukua hisa 21 za Benki ya *NMB* ziende kwa wananchi. Iko hapa sheria, inasema Serikali itakuwa na hisa 30, wawekezaji watakuwa na hisa 49 na wananchi watakuwa na hisa 21. Naomba Serikali muanze kuziuza hisa za *NMB* sasa. Ama moja kwa moja, ama tuitumie *Unit Trust* ifanye kazi ya kuuza hisa kwa sababu hakuna kuchelewa. Hisa hizi ni za wananchi na ni haki yao, iko ndani ya Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninatoa ushauri kwamba Wizara yenyewe ya Nishati na Madini wawe na maeneo ambayo yametambuliwa yana dhahabu ili sasa inapotokea kuna mwekezaji Serikali imwelekeze mahali pa kwenda kuwekeza ili

kuondoa ugomvi huu. Kwa sababu hata taarifa ambayo ndugu yangu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati wa Madini alisema hapa juzi Bungeni, mimi sikubaliani. Alisema kwamba Wizara ina watu wanaofuatilia jiolojia, ripoti zinazotolewa na *investors*, siyo kweli.

Mimi ninao ushahidi kwamba mnadanganywa Wizara na nina *documents* za kuonyesha kwamba mnadanganywa. Wale wawekezaji wa madini wote wanakuwa na taarifa mbili. Moja ni ya kwao na nyingine siyo yenu wanabana ile yenye mali sahihi wanawaletea ya kawaida tu na wanasema hawawezi kuleta kwenu ya siri kwa sababu ya *confidentiality* , wana mashaka watu wenu wanaweza kuuza hizo habari kwa watu wengine. Mimi nina ushahidi na mkitaka niwaletee makampuni ambayo yamewadanganya ninayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mkitaka usahihi, maeneo ya madini yawe ya Serikali ili Serikali ndio ielekeze watu kwenda kuwekeza. Pili, mimi nashauri toka sasa Serikali iwe inaingia hisa. Siwezi kusemea migodi iliyokwishaanza, Serikali inajua jinsi itakavyofanya. Lakini kwa migodi ijayo mimi naomba Serikali yenyewe iwe na hisa, tusiwaachie hawa utajiri wa nchi. Wao wana teknolojia, wana fedha na sisi tuna dhahabu, basi tuungane. Sisi tuna dhahabu na wao wana pesa, twende pamoja 50 kwa 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nimekuta kule Botswana wanajenga mgodi mkubwa sana wa Almasi, wao ni 50 na *De beers* ni 50. Kwa hiyo, ndiyo namna ya kuweza kwenda pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu vilevile, nataka kuishauri Serikali na mimi nina hakika tutafanya vizuri sana, na wananchi wana imani kubwa sana na Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wana imani kubwa na hii bajeti imedhihirisha kabisa. *(Makofi)*

Sasa ni lazima vilevile tuwe na mianya ya kubana matumizi. Mimi nina hakika kwamba Serikalini sasa magari ni mengi kuliko mahitaji na magari, yanaleta gharama kubwa. Mimi naomba turudie utaratibu wa zamani. Magari yote ya Serikali yawe kwenye *pool.* Kila Wizara iwe na *pool.* Watu wa kupewa magari ya Serikali wawe ni wenye *entitlement* ya kupewa gari kwamba ajira ya Waziri ni kupewa gari, ajira ya Katibu Mkuu wa Wizara ni kupewa gari. Sasa wale wengine waende wakapewe gari kwenye *pool.* Leo ukiona kwa mfano, watu wanatoka Dar es Salaam kuja Dodoma, mtu mmoja anapanda gari moja na anatoka Wizara hiyo hiyo na mwingine kutoka Wizara hiyo hiyo naye anapanda gari lake. Kwa hiyo, magari yatakuja 10 kutoka Wizara moja na kila gari amepanda mtu mmoja. Sasa haiwezekani mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani mimi nilipokuwa nafanya kazi, tulikuwa tunapanga ratiba tunampelekea Mkuu wa Wilaya. Kwa hiyo, Mkuu wa Wilaya anaagiza anasema Idara fulani na Idara fulani mtakwenda eneo fulani wote. Kwa hiyo, Maofisa wanne, watano mnasafiri kwa gari moja kwenda kufanya kazi ya wananchi, kwa sababu sisi wote shabaha ni wananchi. Lakini leo kila mtu anataka kwenda na gari lake, tena

gari lenyewe ni shangingi wala siyo gari ndogo ndogo. Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali itusaidie namna ya kubana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ningependa niseme kuhusu takwimu. Mimi narudia kuhusu takwimu. Naomba Serikali ijitahidi kuleta takwimu ambazo zinaonyesha tulikotoka na tunakokwenda. Kwa mfano, takwimu alizoleta Mheshimiwa Waziri mimi nimezipenda, lakini mimi ningependa ziwe zinalinganishwa.

Kwa mfano, kama tunasema tulipanda miti milioni tano, sasa tuseme lengo lilikuwa ni miti mingapi? Tusilinganishe na miti iliyopandwa mwaka jana, hapana. Tulinganishe lengo la miti ya kupanda na iliyopandwa siyo kulinganisha na iliyopandwa kipindi kilichopita. Maana hata ile ukisema ilipandwa miti milioni tano, hautuambii kabla ya kupandwa miti milioni tano lengo lilikuwa kupandwa miti mingapi kwanza. Kwa hiyo, tuwe na malengo ili kipimio kilinganishe lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie bajeti ya mwaka huu. Nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali pale ilipoona wenzetu wanasema uongo wakasahihisha. Nawapongeza sana. Kama mwenzangu alivyosema hapa Bungeni siyo mahali pa kusema uongo. Kwa hiyo, kote kwa wenzetu Wapinzani na sisi Chama Tawala tujiangalie tusiseme uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wenzetu wa *TRA*, pamoja na shida kubwa wanayoipata lakini kila mwaka wamekuwa wanavuka malengo na wao ndiyo wanatuwezesha tunaongea mambo haya. Niwapongeze sana, waendelee na juhudi hizo ili mapato yetu yaongezeke zaidi. Lakini ningewaomba wanisaidie kitu kimoja na waende wakakifanyie kazi.

Ukienda kwenye maduka mengi unataka kununua *TV* au kitu kingine unaambiwa kama hutaki risiti bei yake ni 300,000/=, lakini kama unataka risiti bei yake ni 400,000/=, hivi hizi bidhaa huwa zinaingiaingiaje? Kwa hiyo, nawaomba waende wakalifanyie kazi, lazima kuna dosari mahali waisahihishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hiyo, sasa nirudie kwenye kitabu chenyewe na ninaomba twende ukurasa wa 41. Naipongeza sana Serikali kwa kurudisha ushuru wa asilimia 10 kwa ajili ya mbegu za mafuta na kwa ajili ya mafuta ya wenzetu yanayotoka nje. Kwa kweli kurudisha huo ushuru wakulima wa alizeti, wakulima wa mawese watafaidika kwa sababu watapata bei nzuri na ninaomba hilo Serikali isije ikalifuta tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, mimi nimeshangaa sana kuona mafuta ya ndege yamefutiwa kodi, lakini mafuta ya taa ambayo wananchi wengi wanayatumia hayakufutiwa kodi. Hivi ni wananchi wangapi hapa Tanzania wanapanda ndege? Ndege zenyewe zina migogoro, viwanja vibovu.

Kwa hiyo, mimi ningeiomba Serikali itafute njia nyingine ifute kodi kwenye mafuta ya taa na hiki chanzo ikitafute katika eneo lingine. Sasa hivi tunalinda mazingira yetu, wananchi wanasumbuliwa wakichoma mkaa, lakini wakipata mafuta ya taa kwa bei nafuu itawasaidia zaidi. Kwa hiyo, hilo mimi naiomba Serikali iliangalie ili kuwasaidia wananchi wake. *(Makofi)*

La pili, nashukuru kupunguza kodi kwenye gesi na hiyo ni kwa ajili ya wenzetu wa Mijini. Kule Iramba Mashariki au Monduli hii kitu haiwasaidii kwa sababu gesi haiwezi kwenda kwenye nyumba ya tembe au nyumba ya nyasi, italeta maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa na hii nimeisema kwa makusudi sijaona bei ya bati na bei ya saruji ipunguzwe. Wananchi wetu wanajitahidi sana sasa hivi kujinga nyumba za kisasa, lakini bei ya bati inazidi kupanda na bei ya saruji inazidi kupanda, Serikali inasemaje juu ya hilo na inataka wananchi wake waishi kwenye nyumba nzuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nitaligusia kwa haraka haraka kwa sababu yako mengi, ni upande wa wakulima. Bajeti imewataja wakulima lakini sioni kama watafaidika sana. Wakulima wetu walio wengi bado wanatumia jembe la mkono, tunaomba wasaidiwe waweze kuondokana na jembe la mkono waanze kutumia matrekta. Sasa hivi maeneo mengi wameanzisha *SACCOS*, mikopo iende kwenye *SACCOS* Vijijini kule ili wananchi wetu wapate mikopo. Hilo naliomba sana na lipewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwa wafugaji, Tanzania nafikiri ni ya tatu kwa kuwa na wingi wa mifugo hapa Afrika. Lakini tunataka wananchi wetu wapunguze mifugo yao. Mimi nafikiri la maana zaidi ilikuwa ni kutoa Elimu kwa wananchi na Serikali ilishasema itagawa *ranch* zilizopo kwenye *ranch* ndogo ndogo ili wafugaji wetu wafaidi.

Sasa mimi ningeomba hilo lianze mara moja. Mimi ninataarifa na nampongeza Ndugu yangu Mzindakaya amepata *ranch* kule na inakwenda vizuri, lakini kuna *ranch* ziko nyingi wananchi hawajafaidi. Taarifa ninazo za uhakika, kuna mkulima mmoja kapewa eneo la *ranch* kule Kagera na Morogoro, badala ya kufuga mifugo analima miwa. Sasa hiyo kweli inaendana na sera zetu kweli? Kwa hiyo, mimi nawaomba sana haya mambo yasahihishwe. Wakulima na wafugaji wetu wakishapata *ranch* ndogo ndogo waweke mifugo yao hakutakuwa na ugomvi tena kati ya wakulima na wafugaji, kwa sababu watakaa maeneo yao peke yao na watajitegemea.

Niipongeze sana Serikali kwa kuongeza kodi kwa mifuko ya plastiki. Kwa hilo niwapongeze sana, kwa kweli tunakwenda kwenye kulinda mazingira yetu. Nimesikia kuna watu wanapiga kelele kwamba tutakuwa tumepoteza ajira ya watu 5,000. Mimi niwaombe hao hao badala ya kutengeneza mifuko ya plastiki watengeneze mifuko ya karatasi ili hizi ajira 5,000 ziendelee kuwepo. Kwa kweli kwa mwendo huu Tanzania tunaweza tukarudi na mazingira yetu yakawa mazuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye bei ya sukari. Bei ya sukari bado ni mzigo mkubwa sana hapa kwetu. Tuna mashamba manne ya sukari, kuna Kilombero, Mtibwa, *TPC* na Kagera lakini bado sukari haionekani.

Sukari bei yake sasa hivi kule ninakotoka mimi ni zaidi ya Sh. 1,200/= kwa kilo. Sasa huyu mtu wa Kijijini kweli atamudu hiyo sukari? Kwa hiyo, mimi naomba sana tuangalie na katika haya mashamba manne shamba ambalo naona linajitahidi ni shamba la Kilombero. Haya mengine bado. Kwa hiyo, mimi nauliza, sukari inayotoka Brazil, Thailand bei ni ndogo kuliko sukari yetu hapa, ni kwa nini iwe hivi? Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie sana hilo.

Sasa hivi nikizungumzia upande wa maji, niipongeze sana Serikali na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu kipindi kile akiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, ulipoanza mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na Kahama, nampongeza sana wakati ule alikuwa bado Waziri na akaishauri Serikali. Sasa hivi ni Waziri Mkuu, tunaomba maji yatoke Kahama yakifika yaende Nzega, Igunga, Singida na kwingineko na maji ya Ziwa Tanganyika yatoke Kigoma, yaje Tabora na maeneo mengine na maji ya Ziwa Nyasa yaende Songea na kwingineko. Hiyo ndiyo itatuletea maendeleo zaidi, kazi imeanza nzuri lakini twende tujitahidi zaidi ili tuweze kusambaza haya maji.

Niipongeze Serikali kwa uamuzi wa kujenga Shule za Sekondari. Wananchi walipoambiwa, kwanza Shule za Msingi tumefanya kazi nzuri sana ni yakujivunia. Sasa hivi ni Shule za Sekondari. Mimi nashukuru kusema kwamba ninakotoka kila Kata sasa wana Shule ya Sekondari. Tatizo tulilonalo ni Waalimu na ninajua kabisa Serikali inajitahidi na ndiyo maana imeanzisha Vyuo vingi kidogo kuwa Vyuo Vikuu kwa ajili ya Walimu wa Sekondari.

Lakini mimi ningeishauri Serikali, vijana wote wanaomaliza *Form Six* wakapata daraja la tatu na kuja juu, wote wachukuliwe waende kwenye ualimu. Wale ambao hawatapata nafasi ya kuendelea, waende kwenye hiyo *crush program* ya mwaka mmoja waende kufundisha na kama anataka kujiendeleza atokee kule kazini kwake itusaidie, kwa sababu haipendezi kuwa na Shule nyingi Walimu hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwa haraka haraka, maana sitaki nigongewe kengele, bei ya mafuta ya taa nimeomba ifutwe na hata hivi ilivyopungua tuwe waangalifu, Serikali iwe karibu na wafanyabiashara wasio na nia njema. Sasa hivi wataanza kulangua mafuta ya taa mengi, wanakwenda kuchanganya na *petrol* au na mafuta mengine. Kwa hiyo na hapo Serikali lazima iwe macho sana kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwa upande wa watumishi, tumeshaambiwa kwamba watumishi wataongezewa mishahara. Lakini kuongezewa mishahara kwa watumishi wetu wa Serikali hakutakuwa na maana kama Serikali haitasimamia bei za vitu kama vyakula, nyumba za kupanga na kadhalika. Kwa sababu wameshasikia kwamba mishahara inaongezwa, huko nje nako wanajiandaa kutupokea kama mpira wa kona.

Kwa hiyo, mimi naomba sana Serikali iliangalie hilo ili kuwasaidia watumishi wake na kama wenzangu alivyosema, tumekuwa tunasema hapa Bungeni sasa hivi tunarudisha madaraka kwa wananchi, tutaka madaraka yarudi kwenye Halmashauri zetu. Lakini kwenye Halmashauri zetu ningeiomba Serikali ipitie upya kuangalia Watendeji walioko kwenye Halmashauli zetu za Wilaya. Kuna wengine hawawezi kwenda na kasi mpya ya sasa, wawekwe watumishi wenye uwezo wa kufanya kazi na wale ambao wanafanya kazi kwa moyo wakiitumikia nchi yao na sasa hivi mmechelewa kuwabadilisha Ma-*DC*, Wakurugenzi au kuwa-*confirm* hawa walipo, wale walishasimama, kazi zimesimama maana hajui hatima yake ya leo na kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, Serikali ina mpango wa kuingia mikataba na Halmashauri zetu ili kazi ziende vizuri. Mimi nigeliomba Serikali ili kufanikisha haya vitendea kazi viwepo kule Wilayani na la pili, fedha ziwe zinakwenda kwa wakati, la sivyo mambo hayatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja mia kwa mia. Naomba nikae ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Bajeti kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kabisa nataka niwapongeze Mawaziri wote wawili, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango kwa hotuba zao. Vilevile, niseme kwamba naunga mkono matarajio ambayo wameyaeleza na vilevile hatua za kibajeti. Kwa hiyo, naunga mkono Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze katika maeneo matatu, kwa ufupi na kwa haraka. Kwanza itakuwa angalizo la Bajeti ya 2005/2006 kipindi kilichopita na pili nitafanya angalizo kwenye matumizi ya Serikali kwa 2006/2007 ya sasa na tatu, nitafanya angalizo kwenye mipango ya maendeleo, hali ya uchumi na vilevile kugusia Mkoa wangu wa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nifanye angalizo kwenye Bajeti ya mwaka jana 2005/06 kwenye Sekta ya Elimu kwa ufupi kabisa. Mapambano ya MKUKUTA, chimbuko lake ni lazima iwe ni elimu. Hakuna njia nyingine fupi! Kwa mtu yeyote ambaye atakuwa amekwenda Shule, kwa vyovyote vile atajiuliza nimepata elimu, kwa nini nikumbatie umaskini?

Kwa hiyo, Sekta hii ndiyo ya kuiwekea uzito mkubwa. Sasa najaribu kuangalia angalizo, tumefanya vizuri kwenye mpango wa maendeleo ya Shule za Msingi *(MMEM),* kama ambavyo Waziri hapa asubuhi ametoa kauli yake na mimi naipongeza Serikali kwa mipango hiyo. Lakini sasa ni vizuri tugeukie kwenye Elimu ya Juu. Kwenye Bajeti, kwa sababu elimu ya juu ndiyo itakayotuhakikishia kwamba tutakuwa kwenye mstari wa

mbele katika MKUKUTA kwa sababu ndiyo inayotoa maarifa na vilevile maisha bora pamoja na mapato kupatikana kadri jamii inavyoelimika. Kwa hiyo, nilidhani tugeukie huko ili kwa kweli tusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika angalizo la Bajeti iliyopita, naangalia Bajeti ya MMEM. Katika Bajeti ya MMEM kumetokea upungufu katika miaka mitano iliyopita kwa asilimia karibu 19.2 na kwa mwaka 2003/2004 asimilia 34.6, ilikuwa ni upungufu mkubwa. Kwa upande wa fedha za Wahisani, vilevile kumeonekana upungufu mkubwa sana kumekuwa na asilimia 37.4 na 26.4. Mwaka 2003/2004 tulipata upungufu wa asilimia 54 kutokana na fedha ambazo zimeahidiwa na Wahisani na kwa wastani kwenye Bajeti ya MMEM upungufu ulitokea bilioni 341.7 kwa miaka hiyo.

Kwa upande wa fedha za Wahisani upungufu ulikuwa asilimia 33.3 ni kama bilioni 108. Kama tungelikuwa tunajiuliza kila mwaka hatua tunayopiga na kusema upungufu huu umetokana na nini na turekebishe, basi asilimia hizi zisingekuwa zinapanda juu sana na kupungua sana. Kwa hiyo, la kwanza kila mwaka tuwe tunafanya tathimini baada ya Bajeti kuona upungufu uko wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Elimu ya Juu, matumizi ya kawaida Shilingi bilioni 3.5 hawakupewa. Matumizi ya maendeleo Shilingi bilioni 5.2 hawakupewa na hii imeathiri sana kwa kweli hasa kwenye Vyuo Vikuu vya Mzumbe, SUA na Taasisi ya Mambo ya Bahari kule Zanzibar. Fedha hizi hazikufanya kazi kwa sababu hazikutolewa. Kwa hiyo, hakuna kazi kwa kweli imefanyika kwenye eneo hilo.

Kwa mwaka ujao, Bajeti ya Wizara ya Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu kuna upungufu wa Shilingi bilioni 4.5 kwenye matumizi ya kawaida. Tukubaliane kwamba kwa kweli athari moja ni kwamba azma ya udahili ambayo tumesema wanafunzi wanaoingia Vyuo Vikuu tuiongeze kutoka asilimia 0.27 kwenda mpaka asilimia 12.5, tutaanza vibaya kama upungufu huu utaendelea kuwa hivi. Kwa hiyo haitatusaidia sana.

Vilevile Vyuo Vikuu vishiriki vipya, cha Dar es saam, Mkwawa, pamoja na kile cha Ushirika, vitaathirika sana na ni vipya na vinatarajia kudahili wanafunzi karibu 4,000. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuongeza fedha kwenye eneo hili. Vilevile, kama tunavyofahamu, Serikali inataka kuweka azma ya kuongeza posho kwa ajili ya vijana wa Chuo Kikuu kutoka Sh. 2,500/= mpaka Sh.3,500/=. Hii ni ongezeko karibu bilioni 17. Kama Wazara hii haitaangaliwa, basi itakuwa tatizo, jambo hili litaleta shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mahali penye watu wengi, zipo gharama za maji, umeme, posho za Wahadhiri na mambo kama hayo. Kwa hiyo, nilitaka kufanya angalizo hilo kwamba kwa kweli jambo hilo lirekebishwe.

Vilevile katika uchambuzi, nimeona jambo moja. Chuo Kikuu kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara kilichopo Moshi chini ya *SUA*, wala hakionekani kabisa kwenye mipango hii na Mheshimiwa Rais amezindua Chuo hicho sio zamani, ni hivi karibuni. Wala hakina hata *item code,* hakionekani kabisa kwenye vitabu hivi. Kwa hiyo, ni muhimu sana jambo hilo kwa kweli tuliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, naomba niende sasa kwenye matumizi ya Serikali, hotuba ya Waziri wa Mipango, ukurasa wa 78, 79, Mheshimiwa Waziri amesema, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne hatuna budi kuwa makini zaidi katika kubainisha vipaumbele vyetu. Lakini ameendelea kusema kwamba, sasa ni vizuri tuangalie mambo mengine ambayo huenda tuyaahirishe kutokana na ufinyu wa Bajeti. Sasa mimi nasema tuahirishe haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia *Sub vote* 2600 -300 kasma ya *hospitality*. Kwenye kasma hii matumizi ni Shilingi bilioni 9.7. Hili ni eneo ambalo tunataka tuliahirishe. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Mipango, tuahirishe maeneo mengine. Sasa naomba kufanya angalizo kwamba, kasma hii ya *hospitality* Wizara nane zinatumia kati ya milioni tano na 30, Wizara na Taasisi tano zinatumia kati ya milioni 31na 70. Wizara nane zinatumia kati ya Shilingi milioni 71 na 100 na Wizara 11 na Taasisi zake zinatumia Shilingi milioni 101 mpaka 200 na Wizara tatu zinatumia Shilingi milioni 300 mpaka 400 na Wizara mbili zinatumia Shilingi milioni 400 mpaka 500, Wizara mbili zinatumia Shilingi milioni 500 mpaka bilioni moja na Wizara moja inatumia Shilingi bilioni 1.0 mpaka bilioni 1.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwenye eneo hili, naomba fungu hili lirekebishwe, itolewe asilimia 25 hivi nyingine zote tupeleke kwenye maendeleo, tubane matumizi. Vilevile fungu hili ndilo ambalo ubadhirifu unaweza ukatokea wakati wowote. Kwa sababu huwezi ku-*control,* fungu hili ni la viburudisho, chakula na nini. Ndiyo pale ambapo watu wanaweza wakaandika fedha usizotarajia na bila ya wewe kujua. Hili ndilo fungu la kupunguza kabisa na ikitokea hali mbaya ya ukame, fungu hili ndilo litumike. Msipunguze upande wa maendeleo, punguza eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika vilevile nimeona mianya kwenye matumizi ya Halmashauri za Wilaya. Bajeti za Halmashauri za Wilaya zinaonyesha watu wa upande wa uhasibu wanakwenda Wizarani Dar es Salaam, kila mwezi kufuata *warrant of fund* kwa ajili ya mishahara na mambo mengine. Hili ni ongezeko ambalo sio la lazima, fikiria Waweka Hazina wote wa nchi nzima kwenda Dar es Salaam kila mwezi au Watumishi wengine kuja Dodoma kila wakati, hii inaongeza sana matumizi ya fedha za Serikali, lini tutafanya maendeleo? Kwa hiyo, naomba sana hilo nalo lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni mipango ya maendeleo. Waziri wa Mipango kwenye kitabu chake cha hali ya uchumi 2005 kurasa 101 aya ya 147 amesema hivi, mgawanyo wa miradi iliyoandikishwa kimkoa inaonyesha kuwa Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kwa kupata miradi 339. Anamalizia kwa kusema Mikoa ya Singida na Manyara haikupata hata mradi mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo hapa ni kwamba Serikali imeamua kuijenga Dar es Salaam peke yake. Maana Mkoa wa pili unaofuatia katika kupata miradi baada ya hii 339 ya Dar es Salaam ni Mkoa wa Arusha ambao una miradi 79. Mingine kutoka pale ni Kilimanjaro miradi 29, Mwanza miradi 23. Mingine ni mmoja mmoja, Singida na Manyara haikupata hata mradi wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ndipo hoja ya kugawa Mkoa uliokuwa wa Arusha sasa inaonekana. Arusha inayo miradi 79, Manyara hakuna na Singida hakuna. Sasa Waziri wa Mipango hebu mipango ipangwe jamani msijenge tu Dar es Salaam, mjenge na huku kwingine, tunahitaji kupata na sisi. Sasa miradi 339, yote iko Dar es Salaam ndiyo imeandikishwa kule. Hilo ndilo angalizo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nilitaka niseme kuhusu manufaa ya kukua kwa uchumi kufikia asilimia 6.57, hayawezi kuonekana vizuri na mwananchi wa kawaida kwa sababu ya idadi ya watu. Tunagawana hiki kilichokua wakati ambapo na idadi yetu imekua, sasa mtuambie Serikali kwenye eneo hili la idadi ya watu tunafanya nini?

Tunakuwa tunaendelea, uchumi utakua vizuri lakini tutakapogawana ule uchumi kwamba hii iende kwenye Hospitali, kwenye nini, wananchi wa kawaida hawawezi kuona haya mafanikio kwa sababu idadi ya watu nayo inaongezeka kila siku. Sasa lazima kuna kitu cha kufanya kwenye hili eneo la idadi ya watu ili ukuaji wa uchumi uweze kuonekana kwa mtu mmoja mmoja. Kwa hiyo hili ni eneo ambalo nilidhani ni muhimu kwa kweli lifanyiwe kazi, kwamba sasa hivi tunayo mikono michache inayofanya kazi lakini midomo mingi sana, tunafanya nini? *(Makofi)*

Idadi kubwa ya vijana hawafanyi kazi, kama hatuna sheria ya kuhakikisha kwamba kila mtu nchini anafanya kazi ukiondoa wanafunzi, wazee na wale wasiojiweza, kwa kweli hata siku moja hatutatoka hapo. Tuhakikishe kwamba ni lazima kuwe na sheria ya kuhakikisha kwamba kila mtu anafanya kazi na kila mtu ale kwa jasho lake. Bila kufanya hivi hatutafika. Vijana wengi Mijini wako kwa marundo wanaendelea kutembeza biashara ndogo ndogo, soksi na pengine vitu vingi hata unaweza kukuta ni vya wizi. Lakini tunaangalia tu! Sasa tubadilishe basi hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, sasa nakwenda kwenye Mkoa. Mkoa wa Manyara hauna Hospitali ya Mkoa, Mkoa wa Manyara hauna mtandao mzuri wa barabara, hauunganishwi na Wilaya zake kwa barabara, Mkoa wa Manyara hauna Ofisi za Mkoa, sasa ndiyo zinajengwa, Mkoa wa Manyara Ofisi ya Halmashauri ya Mji mpya hakuna. Sasa tunaomba Serikali, najua Mkoa umeomba fedha kukamilisha Ofisi ya Mkoa, fedha zilizotengwa ni kidogo na Mheshimiwa Rais juzi alipokuwa kwenye ziara ya Mkoa wa Manyara alisema, basi jungu kuu halikosi ukoko, ataangalia. Tunaomba Ofisi zile zikamilike ili Mkoa uhamie kwenye Ofisi zake na tugeukie sasa kwenye Hospitali. Mkoa ambao hauna Hospitali kwa kweli ni Mkoa wa Manyara. Sasa fedha zilizotengwa ni kama za kuangalia tu kiwanja maana ni kidogo sana. Tunaomba azma hii, basi nayo kwa kweli iangaliwe.

Sasa kuna barabara ambayo inaunganisha Makao Makuu Babati, Simanjiro na Kiteto, barabara hii ni kilometa 250 na zaidi. Fedha iliyopangwa ni kidogo sana, milioni 800 tu. Tukiendelea na mtindo huo, barabara itajengwa kwa miaka 20 ili tufike Kiteto na Simanjiro. Sasa Mkoa unawasiliana vipi na Wilaya zake?

Tunaomba Serikali ihamasishe Mashirika kama *TANAPA*, Mashirika haya mengine, Serikali ikope itengeneze mradi maalum kwa ajili ya barabara hiyo, vinginevyo ule Mkoa haujaunganishwa na utapata matatizo makubwa sana ya mawasiliano. *TANAPA* ni mdau katika eneo lile, analo eneo pale, na mashirika haya mengine *PPF*, *NSSF* Serikali inaweza ikakopa ukatengenezwa mradi maalum barabara ile ikatengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasubiri kuona kwenye Bajeti utengenezaji wa barabara ya Minjingu - Babati kwenda Singida, na Minjingu - Babata kuja Dodoma. Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ajitayarishe kwa majibu kwa sababu tumechoka kusikia upembuzi yakinifu kwa miaka mingi iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki hauwezi ukatosha mchangiaji mwingine. Sasa naomba niwaeleze tu jambo moja. Tunapochangia hizi hotuba mbili ya Mipango na ya Fedha, tunazungumza tunayotaka kuzungumza. Hivyo hivyo tutakapokuja katika hotuba ya Waziri Mkuu tutazungumza yoyote yale tunayotaka kuzungumza. Kwa hiyo mnayozungumza sasa hivi ya Wizara nyingine, Mawaziri wanayachukua katika Wizara zao, ndiyo maana tuna wataalam wengi walioko hapa, ni kwa sababu ya ku-*capture* yale mnayoyazungumza kusudi watakapofika kwenye Wizara zao wajibu yale ambayo mmeyazungumza.

Maana nimeona kuna vi- *note* vya wasiwasi hapa vingi tu kwamba mimi nataka. Unapochangia Hotuba ya Waziri wa Fedha, Mipango na Waziri Mkuu mnazungumza chochote mnachotaka kuzungumza ili mradi hamsemi uongo au kutukana mtu. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, hilo ndilo mnatakiwa kufanya. Kwa hiyo, Mawaziri wanachukua katika yale mnayozungumza katika hotuba hizi tatu Mawaziri wanaohusika katika Wizara zao na watayatolea majibu. Maana wengine wanasema nifute huku niweke kwa Waziri Mkuu, kama upo basi upo.

Kwa hiyo, naomba msipate wasiwasi, halafu muandike kwa zile fomu zetu za kuomba. Nimesikia kwamba hazionekani, tutatafuta mahali ambapo mnaweza kuzipata kwa urahisi. Mkiniandikia vi-*note* hapa kama hivi hapa si anakwenda kuvi-*destroy* vyote hivi! Sasa mambo yenu muhimu mtaya-*destroy,* andikeni kwenye *form*. Wanaoandika kuhusu ushauri wowote naomba muandike majina maana mmoja ameandika hapa anasema kwa niaba ya watu wote. Mimi siamini kwamba mmejadiliana wakati gani ikawa kwa niaba ya watu wote. Kwa hiyo, muandike jina kabisa ionekane Mbunge fulani. Kwa hiyo, tutajibu kufuatana na namna hiyo.

Baada ya kusema hayo naomba tuahirishe Kikao mpaka saa 11 jioni.

*(Saa 6.56 mchana Bunge lilisimamishwa*

*mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, Rais ametoa ahadi nyingi tu nzuri ambazo Wabunge na Madiwani pia wanazizungumzia na ahadi hizo ambazo zimo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Ni vyema basi ikazitengea mafungu maalum ya fedha ili zitekelezwe ili wananchi waone kuwa Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi inatimiza ahadi yake ili kila Mtanzania awe na maisha bora.

Serikali Tunafahamu kwamba hali ya hewa imeathiri uchumi wetu kwa kiasi fulani, ambayo hivi sasa Serikali inajitahidi kwa uwezo wake kujaribu kuyaweka mambo yaende vizuri na mimi nina matumaini makubwa tutafika mahali mambo yote yata–*stabilize* na hali ya maisha itakuwa kama ilivyokuwa awali, ili tuweze kuendelea kuchangia yale mambo muhimu ambayo wananchi wanayahitaji katika maisha ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachosema ni kwamba, ili Serikali iendeshe shughuli zake vizuri, ni lazima iwe inapata mapato mazuri kwa kukusanya kodi mbalimbali katika nchi yetu. Yapo maeneo mengi ambayo yanahitaji kupewa kipaumbele na kuweka mikakati madhubuti ili makusanyo ya kodi yawe mazuri na hatimaye bajeti iwe nzuri na hali kadhalika tunaweza tukashughulikia kero za wananchi mbalimbali bila ya kuwa na matatizo makubwa na hatimaye tufike mahali tunaachana na kutegemea wafadhili katika Bajeti zetu. Hilo ni la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sekta nyingi ambazo zinaweza zikachangia Pato la Taifa, mimi nianze kuzungumzia migodi yetu ya dhahabu. Migodi ya dhahabu tumeianzisha siyo muda mrefu sana na tuna matumaini tutafika mahali migodi hii iweze kuchangia pato kubwa la Taifa kama ilivyo katika nchi mbalimbali zinazozalisha dhahabu. Lakini, kuna mapungufu mengi ambayo tunahitaji tuyatizame upya na Serikali izingatie kwamba hoja hapa katika migodi ya dhahabu ni jinsi gani tutapata *share* ya kutosha ili kukidhi Bajeti yetu ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri kuna jambo la kwanza ambalo linarudisha nyuma, ni ile *team* ambayo inafanya *negociation* ya mikataba kati ya Serikali na makampuni yanayokuja kuwekeza katika uchimbaji wa dhahabu. Aidha, *skills* za *negotiation* siyo nzuri. Vile vile, pengine kuna baadhi ya watu wanakuwa wanakosa uzalendo, wanashindwa kutambua kwamba hili ni jambo la msingi na hii ni rasilimali ya wananchi wetu na hatimaye kukubali kwa urahisi kuwapa nafasi kubwa wawekezaji bila kujitazama sisi wenyewe tunafika sehemu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Kamati ya Uchumi na Fedha imesema: “Nafikiri Serikali sasa hivi imekwishajifunza vya kutosha kwamba sasa tunaweza tukajua tumekosea wapi, turekebishe wapi.” Hatimaye sasa tunapopata wawekezaji wengine, basi tutizame vizuri. Tunazungumza nao kwa kiasi fulani na kuhakikisha kwamba Serikali inapata mapato ya kutosha katika migodi yetu.

Nami naungana na Mheshimiwa Rais kwa kusema kwamba, Mikataba ya Madini itazamwe upya ili kukidhi haja ambayo naizungumzia hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitoe mfano, Kahama *Gold Mine* ilikuwa inamilikiwa na *Sutone Resources*, wao wakauza *share* zao kwa *Barrics*. Naye *Barrics* sasa hivi ameingia mkataba na *Placerdom*. Leo asubuhi kulikuwa na swali kuhusu madini na mikataba na mimi niliuliza swali, hivi hii mikataba kunapofanyika *tansaction* za kuuza *share* kati ya Kampuni na Kampuni, hivi Serikali inapata kodi?

Mheshimiwa Waziri alijaribu kufafanua, lakini, inaonyesha wazi kwamba mikataba yetu iko dhaifu, haikuweza kueleza *specifically* maeneo kama haya. Migodi ipo kwetu Tanzania, lakini, yale makampuni yanapouza *share*, sisi tunabaki kutizama macho wanafanya *tansaction* zao, wanapeana pesa, lakini Serikali haipati hata senti tano. *It's not fair*. Sasa, huo ni upande mmoja , tutizame vizuri mikataba yetu. Hii inatokana kwa sababu Serikali haina *share* katika hii migodi. Nafahamu kwa sababu gani labda Serikali haina *share*, labda ni kwa sababu haina uwezo. Lakini tuweze kufika pahala basi, Serikali kwa jinsi yoyote, ni lazima iwe na *share* japo ya asilimia tano katika migodi yote ya dhahabu iliyopo hapa nchini

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo linaweza likatusaidia na maeneo mengine mbali mbali ambayo yanaonekena yana udhaifu katika kupata mapato katika migodi ya dhahabu pamoja na migodi mingine ya Almasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye Benki ya Tanzania, *BoT*. Sarafu yetu inashuka na haya ni mambo ya kitaalam unapozungumzia katika Bunge au Serikali inaposema uchumi unakua. Lakini Sarafu yetu inaanguka, wao wanaona chakula kinapanda bei, mafuta yanapanda bei, haelewi, uchumi unakua, sarafu inaanguka, chakula kiko juu. Sasa hili suala la biashara huria, mimi naiomba sana *Bank of Tanzania* ifike pahala iweze ku – *stabilize* hii *currency* yetu. Hatuwezi tukaiachia *currency* ijisawazishe yenyewe katika soko. Hatuna uchumi ambao ni mkubwa na mzuri sana kuweza tukafikia pahala kama huko.

Watu wengi watatumia *loopholes* hizi na sisi tutazidi kupoteza nguvu ya sarafu yetu. Sasa, naiomba sana *BoT* na sheria ambayo tumekwishaipitisha. Tumewapa nafasi kubwa sana wahakikishe kwamba wanafanya kila jitihada kwamba sarafu yetu inakuwa imara, maana yake nina wasiwasi sasa tutafika kama ile sarafu ya Zambia ilivyo. Ilikuwa ni Dola moja – Kwacha 2400, sasa hivi imeishafika 4000. Sasa tusifike huko. Inatuumiza sana. Inatuumiza katika bei za mafuta, inatuumiza katika kuagiza bidhaa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitu vingi vinaagiziwa kutoka nje kwa ajili ya matumizi ya wananchi hapa ndani, bei zao zinakuwa kubwa, wanaona ni gharama kubwa kununua na inafika mahala inatuumiza, lakini hii ni kazi ya *Bank of Tanzania* na hivi sasa tumewapa meno waweze kuitumia sheria vizuri na Wizara ya Fedha ijitahidi kuisimamia *Bank of Tanzania* kuhakikisha kwamba ina-*stabilize* uchumi wetu na hatimaye ili twende vizuri pamoja na haya matatizo ya ukame yakishamalizika, lakini tuone basi hali inakuwa ni nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie vile vile katika mpango mzima wa kuweza kuinua uchumi wa wananchi kwa maana ya kufanya biashara kwa kukopa pesa katika Mabenki. Yamezungumzwa hapa ni kwamba wewe ukienda kukopa pesa Benki, riba ni kubwa sana. Huwezi ukafanya biashara kwa riba kama hivyo. Nawe unaweka pesa yako Benki, mwananchi anaweka pesa Benki, anapewa riba ya asilimia 2.5, 3, haizidi. Hivi nani atafika mahali aseme mimi naweka pesa yangu Benki? Ndiyo maana wengi wanaamua kuweka fedha zao nje, kwa sababu vivutio vya Benki zetu, havivutii kwa wananchi wenyewe kuweka pesa Benki na hatimaye waweze kupata faida katia fedha zao. Wanashindwa kukopa kwa sababu wanajua riba ni kubwa, biashara ni ngumu, sarafu iko chini. Siyo rahisi kwa yule mwenye kipato cha chini kuweza kukopa na hatimaye akafanya biashara vizuri.

Sasa hivi Serikali nashukuru wameweka utaratibu wa kuwakopesha wafanyabiashara wadogo wadogo katika maeneo yetu. Lakini, pia itazame kwamba kuna mtu mmoja tu katika kila Benki ya *NMB* ambaye anasimamia masuala ya mikopo. Afisa yule, aende Vijijini, Afisa yule akae Ofisini, aratibu shughuli za mikopo, haiwezekani. Naiomba Wizara ya fedha ijaribu kuzungumza na *NMB* angalau kila Benki ya *NMB* katika Wilaya zetu, wawe na Maofisa angalau wawili, watatu kuweza kuratibu shughuli za mikopo ili kila mwananchi aweze kunufaika na mikopo ambayo tumeilenga kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika kero nyingine ambayo inaturudisha nyuma katika kupata mapato na watu kuwa na uzito wa kuleta bidhaa hapa kwa sababu ya kero za Bandarini na hasa katika suala la ushuru. Mimi nitoe mfano wa uagizaji wa magari.

Unapompa mtu nafasi ya kuamua yeye akisie gari hii ilipiwe ushuru wa kiasi gani, wengine watafaidika, wengine wataumia, kwa sababu umemuachia mtu binafsi amue kama yeye. Ni vyema sasa Serikali ikaweka utaratibu mzuri, kwa sababu inaeleweka kabisa kwamba gari za Kijapani zinajulikana kwa *CC* zake na mwaka ambao zimetengenezwa *(Manufacturing Year)*. Sasa, kutokana na vipengele hivi au vigezo hivi, iamuliwe kwa makusudi na katika Bajeti Waziri amesema kwamba sasa magari ambayo toka yametengenezwa mpaka miaka kumi, baada ya miaka kumi, usilete gari nchini.

Mimi ninaipongeza, kwa sababu inatugharimu pesa nyingi ya kununua *spare* kwa sababu ya magari mabovu yaliyopo nchini. Lakini, ndio uwezo wa wananchi kununua hayo magari ambayo wameona kule ni bei nafuu, lakini yakija huku nako, kigongo cha ushuru ni kikubwa sana. Basi, Serikali iweke utaratibu mzuri kwamba, gari ya mwaka fulani, yenye *CC* namba fulani au *CC* ya kiwango fulani, ushuru wake ni kiasi kadhaa, ili yule anayenunua gari anajua kwamba hii gari nikiipeleka nyumbani, ushuru wake ni kiasi fulani kwa sababu ya *CC* na mwaka uliotengeneza ile gari. Utaondoa matatizo ya mtu mmoja kukaa Ofisini na kuamua kwamba wewe ulipe kiasi gani. Hii kwa kweli inaleta mianya ya rushwa ambayo haki wakati mwingine haitendeki katika maamuzi ya kumuamulia mwananchi alipe kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nizungumzie *T-Scan*. *T-Scan* imeletwa hapa nchini kwa nia njema. Lakini inapofanya kazi zake mpaka watoe taarifa yule mteja au

yule aliyeleta bidhaa alipe kiasi gani, inaweza ikamchukua hata wiki tatu. Kwa hiyo, unamlazimisha yule mteja alipe *port charges* bila ya sababu. Haiwezekani *document* imekwishakaguliwa kontena au bidhaa aliyoleta itoke Mkoani kwa mfano Tanga iende Dar es salaam na hatimaye sasa Dar es salaam ndio waamue alipe kiasi gani, inachukua wiki tatu au wiki mbili wakati *storage charge* zikifika, Bandari wataendelea kutoza *storage charge*.

Kwa kweli tutakuwa hatumtendei haki huyu mwananchi ambaye anaagiza bidhaa. Haya yote ndiyo yanayo rudisha nyuma, kukosekana kwa mapato mengi na kwa urahisi wa watu kufanya biashara kwa furaha zaidi. Anafikiria akileta mzigo wake atapatikana na misukosuko kama hii. Kwa kweli inaipunguzia sifa nchi yetu kwa wawekezaji ambao wanataka kuja kuwekeza maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda uliobaki naona hautoshi, lakini nilikuwa na haya machache ya kuchangia. Naiomba sana Serikali itizame maeneo mengi ambayo bado ni kero katika mapato yetu ambayo ndiyo msingi wa Bajeti nzuri katika miaka ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa kupunguza gharama za gesi. Lakini, vile vile watazame na majiko ya gesi, yaingie bila ya ushuru ili kila mwananchi Kijijini sasa awe na utamaduni wa kutumia gesi na hatimaye tuweze kuhifadhi misitu yetu ili tuweze kuwa na angalau na hali nzuri ya mazingira, tuondokane na masuala ya ukame na ukataji wa miti hovyo ambao unatuletea athari.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru kwa kunipa nafasi na niseme naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Thomas Mwang'onda. Atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth B. Kahama. Waheshimiwa, mtaona kwamba sifuati orodha ile kule. Kitu ninachotaka kuwahakikishia ni kwamba kila atakayekuwa ameomba, ama ataongea katika hotuba hizi ama kwa Waziri Mkuu. Hamuwezi kukosa, tunapanga. Kwa mfano tokea asubuhi mmeongea ninyi akina-baba peke yenu. Sasa na jinsia itaingia. Lakini, Janeth B. Kahama yuko namba 13 huko. Kwa hiyo, mnaona tunaangalia, kwa mfano tukifuata orodha hii, utakuta watazungumza Morogoro wanne. Wamepangana Morogoro peke yao. Sasa, tunatafuta na mwingine, mikoa mingine. Kwa hiyo ndiyo maana tunafanya hivyo. Kwa hiyo watu wanauliza, mimi nilikuwa wa kwanza, aha! Kwa hiyo Mheshimiwa Thomas Mwang'onda yupo!

**MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii adimu ya kuweza kuchangia kwenye hoja ya Serikali kwa Wizara ya Fedha na ile ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Kwa kuwa ni mara ya kwanza, napata nafasi hii ya kuongea kwenye Bunge lako tukufu, nimeona kwanza ningeanza kuelekeza salaam zangu za pongezi kubwa kwa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupata ridhaa ya wananchi baada ya ushindi wa kishindo kwenye Uchaguzi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nipeleke salaam zangu za pongezi kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Edward Ngoyayi Lowassa kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Waziri Mkuu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi na wewe mwenyewe na Mheshimiwa Spika, mpokee salaam zangu za pongezi kwa kuchaguliwa kuwa viongozi wetu kwenye Bunge hili tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, salaam zangu za mwisho za pongezi, naomba nizipeleke kwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Uwezeshaji kwa hotuba zao nzuri, zilizokuwa za makini na zinazolenga katika kumkomboa mtanzania yule wa chini kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa napata nafasi leo kwa mara ya kwanza kuzungumza kwenye harma hii, nilidhani basi nitumie nafasi hii na mimi kumpelekea salaam zangu za shukrani, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua kati ya wananchi wale milioni 40 kuwa mmoja wa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya kuchangia, naomba niseme ninaunga mkono asilimia mia kwa mia hotuba za Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Nina kila sababu ya kufikia uamuzi huo. Yaliyomo kwenye Hotuba hizi yameonekana kumlenga yule Mtanzania wa kawaida wa chini kabisa. Nikiwa Mwanachama wa CCM na kiongozi wa CCM, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ambayo ndiyo imebeba zile ahadi zinazotufanya tuwe hapa na kuwa na Serikali tuliyonayo, zimepewa uzito mkubwa na hii inaonyesha kwamba Serikali iliyoko madarakani, kweli nia iliyo nayo ni kuhakikisha inatimiza yale yaliyoahidiwa wakati wa uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache tu na mimi kuleta mchango wangu kama Mjumbe wa Bunge lako hili Tukufu. La kwanza kabisa, ninataka kuongelea juu ya viwanda vyetu. Ni ukweli usiofichika kwamba nchi yetu uchumi wake hasa umelalia katika suala zima la kilimo. Kilimo ndiyo tunachokiita uti wa mgongo. Kinatuchangia pato letu la Taifa kwa asilimia 45.6, hii inafahamika wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama utakumbuka, Mei Mosi mwaka 1995, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wakati akihutubia wananchi kule Mbeya, wakati anaongelea suala la viwanda; alisema bila kusita kwamba nchi yetu kama nchi yetu ni nchi maskini, lakini nchi bila viwanda itakuwa ni ngumu sana kupata yale maendeleo. Wote tunafahamu nchi zile za *G7* wakati ule, sasa hivi *G8*, msingi mkubwa wa heshima zinazopata ni kuwa na viwanda. Ukiifuatilia hotuba ya Waziri wa Fedha, inaonyesha Serikali haikulala nyuma katika hili, nami naomba niipongeze. Wameainisha vizuri kwamba sasa wanaelekeza nguvu zao kwenye suala la *EPZ* na *SEZ* kuhakikisha kwamba tunakuwa na bidhaa zenye thamani na ubora tosha wa kuweza kuuzika nje na hata kuweza kupenya kwenye masoko kama vile *AGOA*, *Canadian Compact* na kadhalika.

Mimi naona ni ushauri tu katika kuleta suala la maboresho. Mapendekezo yangu; ninaelewa umuhimu wa *Free Market Economy*, lakini pamoja na uelewa huu lazima tukumbuke kwamba sisi ni nchi ya Dunia ya Tatu, bado ni nchi maskini. Sasa, tunapokuwa tunaiachia sekta binafsi moja kwa moja, ikatuandalie namna ya kuweza kuamua suala hili la viwanda linakwenda wapi, kidogo nina wasiwasi ile kasi inaweza ikasita. Pendekezo langu kubwa, tuangalie suala zima la uanzishwaji *System ya Establishment* au *ownership* – suala la namna ya miliki ya viwanda hivi. *CRDB* ni Benki moja ambayo imepata mafanikio makubwa sana, na hii yote imetokana na sera nzuri za Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, hebu tazama ule muundo wa umiliki wa zile hisa za *CRDB*. *CRDB* wanae mwekezaji kutoka nchi nchi za nje, lakini vile vile Serikali ina hisa mle, vile vile wananchi wana hisa mle ndani. Ninachosema, hawa jamaa zetu wa nchi za nje huwa wanavutika sana wanapoona kuna mkono wa Serikali katika uwekezaji wa aina yoyote ile *(any sort of investment*). Iwapo Serikali yetu, maana kutoka mwaka 2004 kwenda 2005, tumetoka kwenye ule ukuaji wa viwanda wa asilimia nane tumekwenda kwenye asilimia tisa. Mimi nasema tunaweza kwenda hadi 30, *Inshallah* Mungu akijalia kama tukifuata yaliyo muhimu. Lakini lazima tuwe waanzilishi wenyewe *self initiative* ya *Government* yetu. Tufike mahali tuseme kwa kutumia *Board of External Trade*, tufanye utafiti, tuweke mazingira ya kujua bidhaa gani zinaweza kuuzika.

China sasa hivi *is case in question*, wanakwenda vizuri sana. Watanzania wengi wengine Wabunge humu ndani, wamekuwa wakienda China na kununua vitu na kuvileta huku kwetu. Siri yao kubwa ni viwanda vya gharama nafuu kabisa. Sasa hivi wanapenya soko la dunia vizuri sana. Mimi nasema tukiweza kutumia *BET* tukafanya *RND (research and developement)*, utafiti na uendelezaji wa soko, tutafikia hatua ya kuweza kupata wawekezaji wa kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, katika namna hiyo tutakuwa tunajenga mazingira ya kumwingiza mwananchi wa kawaida kabisa na akawa mmiliki wa viwanda hivi. Kwa maana hiyo mmilki wa nguvu kuu za uchumi ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza tuwe na viwanda ambavyo Serikali imewekeza hela zake kwanza, tutafute mwekezaji kutoka nchi za nje, tutengeneze mazingira ya hisa kuuzwa kwenye viwanda vya namna hii. Lakini yawe mazingira ambayo yatamruhusu mwananchi wa kawaida kabisa wa chini. Hata kama atakopeshwa hisa, kwa kuzingatia kwamba sisi ni nchi maskini, faida tutakazopata pato la Taifa litaongezeka, tutakuwa na viwanda vingi, tuapata ukuaji katika Sekta ya Viwanda, ajira itapatikana kwa wingi sana. Vile vile tutakuwa na wananchi ambao wameongezewa kipato na Serikali yao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali yetu katika kuhakikisha kwamba viwanda vinafanya kazi, mimi nilidhani hii iwe njia mojawapo ya kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri na kasi ya aliye juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la kodi ya ongezeko la thamani, *VAT*. Nchi ya Uingereza, *VAT* inatozwa asilimia 17.5. Tanzania nchi ambayo ni maskini, *VAT* ni asilimia 20. Kabla sijaendelea naomba niweke angalizo kwamba Serikali imeangalia sana hili. Hivi sasa Serikali imeweka msamaha kwenye *Mobile Health Clinics*, yale magari ambayo yanakuja yanafanya tiba za afya. Imeondoa kodi ile. Naomba niipongeze sana kwa hilo. Serikali imeangalia hata katika kuboresha matumizi ya gesi na kuachana na mkaa, imeondoa *VAT* kwenye masuala ya gesi. Naipongeza sana kwa hilo.

Lakini, ninadhani iko haja ya kurudi nyuma na kuangalia tena kwamba kama Uingereza ni nchi tajiri na inafanya vizuri kiuchumi, kodi ya ongezeko la thamani ni asilimia 17.5, kwa nini sisi tusifikie hapo au tukawa chini zaidi! Ninachojaribu kusema ni kwamba kuna kitu kinaitwa *volume business*, wale wawekezaji wa soda, *Coca Cola* na *Pepsi* wao kwenye *volume businness* wanachojali siyo faida kubwa, wanachojali ni uwingi wa mauzo. Uwingi wa mauzo unapokuwa mkubwa nao wanapata faida kubwa. Serikali kwa kushusha *VAT* huko siku za usoni, nina hakika zile hisia za kukwepa kodi zitapungua na itahamasisha wananchi au wafanyabiashara kulipa kodi zaidi. Ningependa sana Serikali ikalipa hili umuhimu mkubwa ili basi pato la Serikali liweze kuongezeka na ile njia ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania ikazidi kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, nadhani muda unakimbia lakini nichangie suala la mfumko wa bei *(Inflation)*. Naweza kuwa na mtazamo labda *radical* kidogo. Ni kweli tumekuwa na mfumko wa bei, toka asilimia 4.3 mpaka asilimia 6.9. Mojawapo ya sababu hizo zimetajwa kwamba ni ukame, njaa, kukosa chakula. Lakini vile vile pia gharama za uzalishaji wa nishati, umeme nazo zilichangia. Najua ninao marafiki wengi ambao wanashiriki katika uuzaji wa mafuta. Lakini, mimi nasema iko haja ya kudhibiti *prices* za mafuta. Wale wenzetu wa *OPEC*, ule umoja wa wazalishaji wa mafuta Duniani, wale *Oil Producers*, huwa kuna wakati wanakaa pamoja na kuamua kushusha bei ile ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapoamua kushusha yale mafuta, sisi huku hayashuki. Sisi yakipanda, yanapanda tu. Matokeo yake sisi ni nchi maskini, gharama za maisha zinaendelea kupanda siku hadi siku. Ninasema kwa nia njema tu, tufike mahali tutengeneze Bodi maalum kwa ajili ya udhibiti huo, tukiangalia kweli tunaishi katika Uchumi wa Soko Huria *(Free Market Economy)*, tunatambua hilo.

Lakini, basi angalau wale wenzetu wa *OPEC* wanaposhusha na sisi tushushe ili tuweze kupata unafuu kwa nchi yetu ya Tanzania. Bei ya mafuta inakuwa kama fimbo vile ya kumpigia mwanafunzi au ng'ombe aweze kwenda katika namna ambayo mchungaji anataka. Tukifika hapo, dunia ikishusha bei ya mafuta, basi na sisi huku tutakuwa na hali ahueni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua muda unanikimbia lakini kwa ufupi sana ninataka nichangie suala la nishati. Mimi ninasema ipo haja ya kuangalia suala la nishati mbadala. Tunatumia umeme, sasa hivi tuna *SONGAs* na kadhalika. Hii inaweza ikaonekana ni ya gharama ya juu. Lakini, nadhani imefika wakati ambapo sasa nishati ya

umeme wa jua *(solar power)* hasa kwa wale wananchi wa hali ya chini wa Vijijini pamoja na ugharama wake, ni wakati umefika sasa wa kuifikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapowekeza kwenye umeme wa jua *(solar power)*, ni ukweli usiofichika, gharama yake ni kubwa siyo siri. Lakini ukiangalia *on a long time basis*, kuna faida kubwa, maana gharama inakuwa betri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo. Naunga mkono hoja ya Serikali. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuwa mwanamke wa kwanza leo kuchangia katika Bajeti katika ukumbi huu mpya, nakushukuru sana. Naomba kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyejalia ujenzi wa ukumbi huu umekamilika bila kuwa na matatizo na katika hali ya usalama wa sisi wote tumeweza kuwa huru. *(Makofi)*

Naomba kupongeza sana hotuba ya Bajeti ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne. Kwa kweli ni Bajeti nzuri sana ambayo imeletwa kwetu hapa na Waziri wa Fedha mwanamke wa kwanza baada ya miaka 45 tangu tumepata Uhuru na iliyotolewa kwa mara ya kwanza katika ukumbi huu mpya uliofunguliwa hivi juzi na Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 12 Juni, 2006. *(Makofi)*

Bajeti hii kusema kweli imejitahidi sana kutatua na kuzungumzia matatizo ya wananchi wa Tanzania kwa ujumla. Ingawa ni vigumu katika kipindi cha miezi 12 ukafanya maajabu ya kutimiza matatizo yote ya wananchi wa Tanzania.

Lakini hata hivyo imeanza vizuri katika awamu hii. Kiongozi Mkuu wa China marehemu *Chairman* Mao Zetung alikuwa na msemo ambao alisema safari ndefu huanzia hatua ya kwanza, kwa hiyo, mimi naamini hatua hii imetoka safari ndefu lakini iko njiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kutoa mchango wangu kwanza katika *page* ya 22 katika Kitabu cha Waziri wa Fedha, Bajeti imezungumzia kuwa asilimia 45.8 za fedha za kutekeleza MKUKUTA zimewekwa kwa ajili ya kukuza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hapo nishikilie eneo la *SACCOS* kwa kweli awamu ya tatu imejitahidi sana kuhamasisha na kuanzisha *SACCOS* nyingi nchini kote, hata Mheshimiwa wa Upinzani leo alizungumzia kuhusu suala hilo la *SACCOS*. *SACCOS* nyingi zimefaidika na zimeendelea vizuri. *SACCOS* hizi ambazo baina yao ni za wanawake, za vikundi vya vijana, wafanyabiashara mbalimbali, wakulima mbalimbali zimeweza kujikokota mpaka hapa zilipofika. Ingekuwa vema basi Serikali ingeendelea kuhamasisha katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kuhakikisha wengi wamejiunga na *SACCOS* hizi au wameanzisha *SACCOS*. *(Makofi)*

Lakini naomba vile vile kuwaomba Serikali iangalie katika kuwasaidia wana *SACCOS* hawa waweze kupata mafunzo ya kutosha ya biashara kuhakikisha

wanapochukua mikopo au kuweka waweze kufanya biashara bila kupata hasara. Kwa hiyo, tunaomba Serikali isaidie katika eneo la mafunzo ya biashara na maeneo ya mafunzo ya kuweka na kukopa. Vile vile tunaomba Serikali iangalie suala zima la kusaidia vikundi hivi vipate angalau fedha au mikopo ya kutosha kuweza kuanza *SACCOS* kununua vifaa na hata kujenga ujenzi wanaotumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba katika *page* inayofuata hapo juu ya 23 naomba kununukuu; “kwa ujumla Bajeti hii imetenga asilimia 26 ya mapato ya ndani kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.” Halafu ukiruka mstari wa pili inasema; “lengo ni kutenga mtandao mzuri wa miundombinu.” Hapo kwenye miundombinu mimi leo naomba kwa kweli niache mengine yote lakini nijikite katika eneo zima la usafiri katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam ni Jiji la wote tuliopo hapa. Hata kama Dar es Salaam imetengewa kiasi gani cha jambo lolote tukubali, tusikubali ni kuwa sisi wote wengi wetu tunaishi Dar es Salaam au tunapita Dar es Salaam kufanya shughuli zetu. Utaratibu mzima wa usafiri kwa wananchi wa Jiji la Dar es Salaam ni kero kubwa sana jamani tena kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa daladala wa Dar es Salaam ni usumbufu mkubwa sana kwa abiria wote wa Dar es Salaam. Abiria hao wakiwemo wafanyakazi, wafanyabiashara na hata watoto wa shule kiasi kwamba wafanyakazi wengi wanachelewa sana kufika maofisini na wanalaumiwa wakifika ofisini na pia wanachelewa kurudi majumbani kwao. Usumbufu huu unadhoofisha tija kwa sababu unaongeza badala ya kusaidia kupunguza umaskini kwa ajili ya usumbufu huu wa usafiri wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina pendekezo langu moja, mimi naona unatakiwa mfumo mpya kabisa wa usafiri. Tukirudi kama ule wa mwaka 1960 ambapo tulikuwa na *UTC* ungeliweza kusaidia. Lakini tunaomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwasaidia wenye daladala wajiunge, waunde kampuni moja kubwa ambayo pia ikiwezekana watafutiwe mbia ambaye mbia huyo ana uwezo na uhakika na utalaam wa ujuzi wa kuendesha shughuli ya huduma za usafiri katika miji mikubwa kama Dar es Salaam. Bila mbia huyo na bila hivyo kwa kweli mpango uliofanywa sasa hivi mimi nasema ni wa muda tu hatutafika mbali sana. Tunachohitaji kwa kweli ni *strategic joint venture partner* ambayo ni kitu cha muhimu sana. *(Makofi)*

Mfano mzuri ni *OC transport* ya Mji wa Ottawa Canada ambao wao hawana *underground system*, hawana *train* hizi, wanategemea mabasi, lakini basi zinakuja zinapita kila mahali na ni mfano mzuri duniani. Nadhani Mheshimiwa Bernard Membe kama yupo hapa atakumbuka yeye aliishi Ottawa ni mfumo mzuri duniani. Namwona amesimama, ahsante sana Mheshimiwa Bernard Membe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nikizungumzia tatizo la msongamano wa magari ya Dar es Salaam, nasema haliwezi likatatuliwa kwa njia yoyote sasa hivi, ukisema uongeze barabara inamaanisha unavunja nyumba na hiyo unamaanisha ni

gharama. Ukisema uweke boti, maboti kutoka Kunduchi kuja mjini ni gharama. Ukisema uweke jambo lolote *fly over* ni gharama zaidi. Ukisema uweke *commuting trans* yote ni gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu kwa Serikali yetu ni Serikali yetu kuhamia Dodoma. Serikali yetu ihamie Dodoma kama ilivyokuwa imepangwa toka zamani. Vinginevyo kama sivyo baada ya miaka mitano Jiji la Dar es Salaam halitakalika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi kwenye matatizo sugu ya Ziwa Victoria nilikozaliwa, *airport* ya Mwanza, *airport* ya Bukoba, ni lini *airport* hizi kwa kweli zitaitwa zikawa *airport* bila matatizo aina yoyote? *Airport* ya Mwanza inajitahidi lakini bado kuna kasoro, wafanyabiashara wote wa mazao kama ndizi zinatoka kule, zinatoka Ziwani, Kagera, Mwanza, Mara kuna mboga, kuna matunda yote yanakosa soko kwa sababu hakuna kiwanja cha kuaminika na cha uhakika. Soko kuu la ndizi, mboga, matunda na kadhalika liko *Middle East* na wote mnajua. Lakini cha kusikitisha ndugu zetu wa Uganda ndiyo wanaofaidika na soko hilo peke yao. Sisi Tanzania hatufaidiki, hatumo kabisa na tunalima. Halafu Waganda wenyewe wananunua ndizi kutoka Bukoba, Karagwe, lakini hatufaidiki sisi, wanafaidika wao. Kwa hiyo, baada ya hayo naomba Serikali ifikirie kuhusu suala la Kiwanja cha Ndege cha Bukoba kiwe cha *International* na pia cha Mwanza kifike kiwango cha kuwa *International* kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba baada ya hapo kabla ya kengele kulia mara ya pili, naomba nizungumzie kidogo mikakati ya uchumi wa kilimo, naunga mkono kuhusu sera ya kilimo ya umwagiliaji maji. Hiyo haina mjadala kabisa kwangu. Ni jambo zuri sana na tuendelee nalo. Lakini tuwe na *strategy* ambayo inaendana na karne ya 21 na *strategy* ambayo inaendana na soko la karne ya 21 hapo tutafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hivyo kwa sababu kuna mazao ya kilimo ambayo ni mazao ya biashara. Zao moja naomba nilitamke ni zao la muhimu sana antimisia. Zao la antimisianadhani kuna nchi kama mbili tu duniani mojawapo ikiwa Tanzania ambapo linalimwa na linaweza kuota. antimisia inatengeneza dawa ya *Malaria* ambayo kama tunajua *Malaria* inaua zaidi Ukimwi. Katika Tanzania Mkoa wa Mara ndiyo peke yake wameanza kulima zao hili la antimisia. Naomba basi Serikali ijitahidi inavyoweza kuhamasisha Mikoa ile yenye neema kama ya Mkoa wa Mara ambao wanaweza kulima zao hilo. Lakini kuna mazao mengine pia ambayo yanaweza yakawa mazao ya kuuza nje, *amarula* wengine wenu mnakunywa hapa ni kinywaji kizuri sana, *amarula* inatengeneza chai katika nchi za Afrika Kusini, *amarula* pia inatengeneza dawa na vipodozi. *(Makofi)*

Lakini kuna mazao mengine kama *jet rover* ambayo tunaambiwa inatengeneza dizeli na huku dizeli inatoka nje na kumbe nyumbani tunaweza kuwa nayo. Kuna mlonge, alofa yote hiyo ni lazima Serikali iangalie kuhamasisha wananchi waanza sasa kulima mazao ambayo yatatuletea faida.

Lakini iko haja pia ya kutoa kipaumbele kwenye mazao ambayo bado hatujajitosheleza kama miwa, sukari bado haijatutosha, kwa hiyo, hatujatoshelezwa na zao la miwa hata kidogo. Kwa hiyo, naomba tuweke mkazo katika eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kidogo kabla sijamaliza nigusie Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Serikali bado nasikitika sana haijaweka mkazo na kuona umuhimu kabisa wa Wizara hii. Tanzania sasa tuna taabu sana ya umeme, lakini tunahitaji kuingia na sisi katika karne hii ya *nuclear power. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii moja kwa moja. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN AHMED SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo. Awali ya yote na mimi niungane na wenzangu kwa kumpongeza sana Mama Zakia Meghji na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa kwa hotuba nzuri na yenye mwelekeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Waziri Mkuu Ndugu yetu Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya kwa faida ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo naomba nimalizie pongezi zangu za dhati kabisa kwa wenzetu wanaokusanya mapato katika nchi yetu, *TRA*. *TRA* inafanya kazi kubwa na nzito, mwaka huu tumejionea wenyewe nchi yetu imeingia katika tatizo kubwa la njaa, lakini *TRA* kwa kuongozwa na Ndugu Kitilya wameendelea kuvuka malengo, wameendelea kufikia malengo na wanaendelea kufanya kazi nzuri kwa wakati mgumu pamoja na kwamba sisi wafanyabiashara tunaendelea kulalamika lakini kwa kweli *TRA* wanaendelea kufanya kazi nzuri na mimi naendelea kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Mimi naomba kushauri Serikali katika maeneo yafuatayo, kwanza nianze na eneo la mafuta, wenzangu wamelizungumzia na mimi naona nichangie kidogo. Mafuta bado ni tatizo katika Taifa letu na bado zipo juhudi zinaendelea kufanywa lakini bado mimi naishauri Serikali wakati nachangia hotuba ya Rais Bungeni nilishauri Serikali kwa upande mafuta ingeunda chombo maalum, mafuta ni kitu nyeti kwa Taifa lolote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tumekuwa na utaratibu wa kusema kwamba ni soko huria. Mafuta yanapanda, yanashuka, yanakwenda kulia yanakwenda kushoto, juhudi zinaendelea kufanyika lakini bado hazijazaa matunda. Hapa kuna mambo mawili, aidha, Serikali idhibiti bei kwa kupanga bei ya mafuta kwa maana ya *control price* kwa mafuta au Serikali iunde chombo maalum kufuatilia mafuta, tokea yanapotoka mpaka yanakoingia na jinsi yanavyolipiwa ushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukiwa na *control price* ya mafuta itasaidia sana kuelewa kwamba sasa hivi soko linakwendaje. Lakini bado lipo tatizo pale juhudi zimefanywa kufunga *flow meter, flow meter* zile zinaonekana bado ni tatizo. *Pressure* ya kusukuma mafuta kwa kutuma *flow meter* ni ndogo. Sasa hivi inaonekana Serikali tena

inaingia gharama ya kufunga *air valve* pale bandarini. Sasa leo *flow meters,* kesho *air valve* keshokutwa sijui kitu gani, hii yote inafanyika kwa sababu hatuna chombo maalum cha kusimamia, kuangalia tatizo hili litakwisha vipi. Zoezi la *air valve* litakapofika inawezekana tukapata tatizo la wiki au siku kumi au siku kumi tano la kushusha mafuta bandarini. Hapo sasa tatizo litajitokeza na nchi inaweza ikaingia katika tatizo kubwa. Wakati wowote nafikiri suala la kufungwa kwa *air valve* litakuwepo maana ni lazima hatuweze kulikwepa hilo. Sasa naomba Serikali iliangalie suala hili kwa umakini zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumza ni barabara. Mvua hizi zilizonyesha barabara zetu vijijini zimeharibika kabisa, lakini Serikali ina utaratibu maalum kwa Manispaa za Miji kuwapa fedha za kununua magari ya zimamoto. Hivi karibuni tumeshuhudia magari ya zimamoto zaidi ya arobaini yamenunuliwa kwa ajili ya Manispaa. Hivi kwa nini Serikali isifanye utaratibu wa kuwanunulia Halmashauri za Wilaya greda kwa ajili ya kuchonga barabara? Ikiwa Manispaa wananunuliwa magari ya zimamoto sisi kule vijijini tunahitaji magreda kwa ajili ya kuchonga barabara zetu. Halmashauri hatuna uwezo wa kununua greda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo gari moja la zimamoto ni shilingi milioni 350 na kuendelea. Naishauri Serikali iangalie uwezekano wa kutupatia mafungu maalum Halmashauri tuweze kununua greda ambazo zitachonga barabara zetu kwa maeneo ambayo tunaona yameathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Manispaa wapewe magari ya zimamoto sisi vijijini tupewe magreda. Hata ikiwezekana kutusimamisha mafungu ya barabara kwa muda bora iwe hivyo lakini baada ya hapo tupewe magreda yatakayotusaidia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili la barabara lipo suala la barabara ya kutoka Korogwe - Handeni - Mziha - Turiani - Mvomero mpaka Mikumi ni ahadi ya Mheshimiwa Rais lakini naishukuru Wizara ya Miundombinu, juzi wakati wanajibu swali la Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, wamesema barabara hii tayari iko katika mipango ya awali. Mimi naiombea Serikali kila kheri na baraka mipango ya awali hiyo iendelee hadi ikamilishe ahadi yake ya kuwekwa lami kwa barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie kwenye kilimo, Mkoa wa Morogoro, umejaliwa, una mito mingi na una maji mengi. Serikali kama Serikali bado haijatambua umuhimu wa kutumia Mkoa wa Morogoro kama sehemu ya akiba ya chakula kwa Taifa letu. Katika Wilaya ya Mvomero, tuna mabonde mengi ya umwagiliaji, kazi tunazofanya ni kutokana na uwezo wa Halmashauri na wananchi wenyewe. Lakini tukipata nguvu na msukumo wa Serikali Kuu, Mkoa wa Morogoro, tunaweza tukalisha Mikoa zaidi ya mitano au zaidi ya hapo. Tunaiomba Serikali ije ikae na Wabunge wa Mkoa wa Morogoro, ifanye tathimini ili na sisi tuweze kueleza yale maeneo ambayo tunaweza tukashirikiana na Serikali Kuu kwa kuweza kusaidiana nayo katika maeneo ambayo tunahitaji msaada. *(Makofi)*

Lakini katika hilo la kilimo kuna suala la ruzuku ya mbolea mimi naomba kuiuliza Serikali hivi hii ruzuku ya mbolea nani anajua inapatikana wapi na kwa bei gani? Tunaambiwa mbolea za ruzuku zipo na zinapatikana, hivi mkulima atatambuaje kwamba duka lile linauzwa mbolea ya ruzuku? Mbolea inauzwa shilingi 18,000/=, 20,000/=, 25,000/= lakini anayefaidika ni yule muuzaji siyo mkulima. Hakuna chombo chochote kinachoweza kufuatilia kwamba mbolea ya ruzuku Mkoa fulani huko inakotoka inatoka kwa beni gani na mkulima inamfikia kwa bei gani. Wabunge hatuelimishwi, Madiwani ukiwauliza hawana taarifa, inaonekana ni suala la watalaam. Sasa naomba Serikali itusaidie, aidha kutupa maeneo ambayo yanaweza yakatusaidia katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningeishauri *TRA* waliangalie ili waongeze mapato yao ni suala la ushuru wa mafuta ya taa pamoja na *Jet A - 1.*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mafuta ya ndege hayana kodi, lakini mafuta haya ya ndege yanatumika kama mafuta ya taa. Kwa sababu hayana kodi inawezekana ujanja ukatumika ili watu wakayaleta kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri *TRA* wale wenye uwezo wa kuleta mafuta haya ya *Jet*, kwanza wayalipie kodi, baada ya kutumika wapewe *refund* na *TRA* la sivyo kutakuwepo na udanganyifu mkubwa katika eneo hili na Serikali itakosa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumza ni mifuko ya jamii ya *NSSF* na *PPF*. Mifuko hii inaonekana ina mitaji mikubwa na inatoa mikopo mikubwa kwa watu wenye uwezo mkubwa. Mimi ushauri wangu kwa mifuko hii na kwa Serikali, ni kuwa wafanyabiashara wakubwa wana uwezo wa kukopa mabenki na wana dhamana zinazotambulika, lakini watumishi wa Serikali au watumishi ambao wako katika taasisi mbalimbali hawana uwezo wa kupata mikopo kwa sababu hawana dhamana. Badala ya kutoa bilioni kumi kwa mfanyabiashara mmoja ni vema basi tukatoa bilioni 10 kwa watumishi 1,000 kila mmoja akakopeshwa milioni 10 fedha za Tanzania ili watumishi hawa wajenge nyumba bora na wakalipa. Lakini leo mifuko hii haiwanufaishi wanaokatwa, inawanufaisha matajiri wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mdogo, *TRA* wapo watumishi 3,500 watumishi 3500 ukiwapo milioni 10 ni bilioni 35, bilioni 35 hizi utakuta mifuko hii imeshakopesha watu wengi. Sasa mimi naishauri Serikali mifuko hii sasa iondokane na dhana ya kukopesha wafanyabiasahra wakubwa na badala yake ikopeshe watumishi, wajenge nyumba bora wawe na maisha bora katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona wenzetu kwenye Bajeti wametuletea suala la kuongeza *airtime* kwenye simu. Mimi hiyo sikatai, nakubaliana nayo, lakini ninachotaka ili wakusanye zaidi mimi ningeishauri Serikali wakati wanakusanya *airtime* kwa asilimi 7 basi waondoe *VAT* kwenye simu zenyewe ili simu ziletwe kwa wingi, wao *TRA* wakusanye *airtime* kwa wingi. *(Makofi)*

Sasa hivi simu ukileta *peace 5, peace 6* unalipa *VAT 20%* sasa kwa sababu wao wanataka ku-*base* zaidi kwenye *airtime* basi haya madude haya yaje kwa wingi ili wao wakusanye zaidi *airtime* na Serikali ipate mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la kuwasaidia wananchi wetu katika eneo la kujenga nyumba bora. Naishauri Serikali kwa Bajeti ya mwakani, safari hii tumechelewa kwa sababu tutaharibu mwelekeo mzima wa Bajeti. Huko mbele Serikali iondoe *VAT* katika *cement* na mabati. *Cement* na mabati ni sehemu kubwa inayosaidia watu kujenga nyumba bora. Lakini maeneo haya mawili yanabeba mzigo mkubwa. Kila siku bei ya *cement* inapanda, Serikali iangalie uwezekano wa kuondoa *VAT* katika *cement* na bati kwa siku zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na suala la umeme, umeme umeahidiwa katika Majimbo yetu Sumve na Mvomero. Lakini bado miradi yote miwili imesimama, kule Sumve kuna mradi wa umeme unaokwenda Malya, kule Mvomero kuna mradi wa umeme unaokwenda Mngeta, miradi hii miwili namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie ili miradi ile ikamilike. Mradi wa Mngeta umeanza mwaka 2004 umefikia katika .... Serikali imeshatumia zaidi ya shilingi milioni 200 mradi haujakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, wafanye ziara katika Wilaya ya Mvomero wafike eneo la Mngeta wakague mradi huu. Mvomero iko barabarani, ni barabara hii hii ya Dodoma naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake yeyote atakayepata muda hata kama ni Jumamosi na Jumapili tukaangalie ni jinsi gani *TANESCO* imeshapoteza mamilioni ya fedha lakini bado mradi haujakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kabla sijamaliza nitamke naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

La mwisho naona muda unaruhusu, la mwisho wenzetu wa *TRA* wanaendelea kukusanya kodi, lipo eneo ambalo wanatakiwa wakusanye kodi katika kodi za majengo, *rental income*. Inaonekana majengo mengi yanajengwa katika Jiji la Dar es Salaam na wanaojenga majengo yale wanapata misamaha kupitia *TIC* lakini bado kodi ni kubwa na sina hakika kodi zinazolipwa hizo chache kama zinalipiwa 15% ya kodi inayotakiwa kulipa *TRA*. *TRA* inatakiwa itenge kitengo maalum kwa kujua kwamba je, mapato haya nayo yanaingiaje na yanasaidia vipi na yanalipwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Labda na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kuwa hai na kuniwezesha mimi kusimama leo hii ikiwa ni siku ya mwanzo ya michango ambayo inatolewa kwenye hizi hotuba mbili ambazo zimetolewa na Mawaziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji pamoja na Waziri wa Fedha. Vile vile napenda kuchukua nafasi hii, kutoa pongezi kwa Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Spika, pamoja na wewe

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kazi nzuri pamoja na mazingira mazuri ambayo tunaanza kuyafanyia kazi hivi sasa. *(Makofi)*

Vile vile nichukue nafasi hii kuzisifu hotuba mbili ambazo zimesomwa hapa na Mawaziri wetu kwamba kweli zina lengo la kuondoa umaskini. Ile nia ya kuondoa umaskini inaonekana humu ndani ya hizi hotuba. Kwa hiyo, kwa hilo nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yaliyomo katika vitabu hivi ni mazuri pamoja na hotuba nyingine ambazo zimetangulia kueleza vinginevyo na wasiwasi wao. Lakini nadhani Wabunge wengi ambao wamechangia walichangia zile sehemu ambazo zilikuwa zinatia mashaka kidogo ili kuzidi kuboresha. Hotuba zao zimekuwa nzuri sana na kwa hilo tunazidi kuendelea kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wale wachache ambao watakuwa wanapenda kurekebisha baadhi ya maeneo ili utendaji wa Serikali hii uweze kwenda vizuri sana. Mwanzo wa utendaji wa kazi wa Serikali unaonekana ni mzuri sana, nia ya viongozi wote wawili au wote ambao wapo katika Serikali Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, inaonekana ni kweli wanakusudia kuwafanyia mema wananchi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda nizungumzie kipengele fulani ambacho kidogo kimekuwa na usumbufu pamoja na kwamba watu wamekuwa wanakipigia kelele sana lakini imeonekana kwamba kinaangukia sijui tuseme hakisikiki au hajitokezi mtu akajaribu kuweka vizuri hiki. Pamoja na sifa ambazo tumekuwa tukitoa hapa kukipa kitengo ambacho kinahusiana na ukusanyaji wa kodi cha *TRA* pale pana tatizo kubwa sana ambalo lisipoangaliwa linaweza likachafua hii hali ya hewa nzuri ambayo tunaanza nayo katika kuendesha utawala katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wananchi hasa kutoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano kuhusiana na unyanyasaji ambao unafanywa na maafisa katika kitengo hiki cha *TRA*. Nina uhakika kwamba wengi wameshalisikia hili kwa sababu wengi wameshalizungumza hata wananchi wenyewe kabla ya sisi viongozi kuanza kulizungumza wamekuwa wakilizungumza kwa sauti kubwa sana lakini matokeo yake hayaonekani na *TRA* wamekuwa wakiendelea na vitendo hivi. *(Makofi)*

Mimi nitatoa baadhi ya mifano, mimi mwenyewe nimewahi kufika *TRA* wakati nikiwa katika shughuli za Kamati na kuuliza baadhi ya maswali lakini majibu yamekuwa hayaridhishi. Kuna suala hili linalohusiana na suala la usajili wa magari ZNZ. Gari lililosajiliwa Zanzibar, gari lolote linaloingia Tanzania ikiwa ni pamoja na Zanzibar kodi ile inakusanywa na *TRA*. Hata huko Zanzibar kipo kitengo cha *TRA* ambacho kinafanya kazi hiyo hiyo. Kwa hiyo, gari wewe linunue popote lakini mandhari unaliingiza Tanzania kodi ile inachukuliwa na *TRA* na wala siyo bodi ya mapato ya Zanzibar. Lakini la kusikitisha utakapochukua uamuzi kwamba gari hii sasa naisajili kwa namba za Zanzibar hapa ndipo linapoanza tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo linatokea ukishasajili kwa namba za Zanzibar ukasema sasa baada ya matumizi yako labda mtu anataka kulileta gari sasa Tanzania Bara hapo unaanza kukutana na usumbufu. Barabarani unaweza kukuta magari yamepangana labda mawili yanatoka Afrika Kusini kuna moja la Kenya, moja la Uganda lakini lile la Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano litasimamishwa na usumbufu unaanzia hapo. *(Makofi)*

Mimi niliwauliza *TRA* kwa nini mnafanya hivi? Nikapata jibu kwamba ahaa unajua maafisa wetu, sasa najibiwa maafisa wetu ili maafisa wa *TRA* walioko Zanzibar wana-*collide* na wananchi Zanzibar kwenye mapato kwenye ile kodi inayolipiwa yale magari.

Mimi nikawauliza jamani *collation* hii lakini hamwoni kama ni suala lenu la ndani kwa sababu Ofisi ya *TRA* iliyoko Zanzibar ni ile ile ya Jamhuri ya Muungano? Kama kuna *collation, collation* hao maafisa wenu mmewachukulia hatua gani ambao wameshiriki kwenye suala hili? Kwa sababu Zanzibar ziko gari nyingi sana namba za Zanzibar za magari sasa hivi ziko kwenye 50,000 ZNZ 50000 na zinaendelea. Magari mengi sana ikiwa Maafisa wa *TRA* wameweza ku-*collide* na namba yote hiyo, ni mapato kiasi gani yamekwishapotea hapa na mnawachukulia hatua gani na nikataka kujua ni nani na nani ambao wamechukuliwa hatua kutokana na hii *collation* sikupata jibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikaja nikauliza tena kuna afisa mmoja alikuja wakati tuko Bagamoyo akatoa mwongozo mzuri sana wa *TRA* kausoma na mimi niliusifu. Lakini tulipokuja tena kwenye suala hili kwa nini mnawakamata wananchi, mnawasumbua humu njiani kuhusiana na tatizo lenu la ndani kwa sababu ilikuwa ninyi kwanza mjisafishe ninyi wenyewe *(in house cleaning)* kwanza kabla hamjaanza kuwasumbua watu nje.Kwa nini hamuwachukulii hatua? Walahi jibu hakuwa nalo, wanatuambia sisi tutawakamata tu. Utayakamata vipi magari ya watu, kwa tatizo lako wewe? Wewe unafanya kosa halafu unaenda kumvamia mtu mwingine. Isitoshe hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nendeni na Zanzibar mkachukue ile hatua kasimamisheni kule. Kwa sababu wapo watu magari wanaendesha magari kule, kodi kiasi gani zimepotea?

Mheshimiwa Naibu Spika, haikuishia hapo tu, mimi nitarudi nyuma zaidi kidogo labda nilipozungumza kwenye Kamati yule kiongozi wa *TRA* hakunielewa au alinisahau. Kipindi kilichopita nilikuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar na katika watu aliokuja kuzungumza nao mimi nilikuwa mmoja wao, tumekaa ofisini tukazungumza kuhusu usajili wa magari. Tukalizungumza vizuri na nilikubaliana sana na wazo lake kwamba hili wazo ni zuri lakini kwa sababu sisi tumekuwa na utaratibu wetu tungeomba basi kwa upande wa Zanzibar tutengewe fungu katika baadhi ya hizi namba wala hatutaki nyingi namba zote zitakazoanza *T100 ZAA* tupewe sisi kule Zanzibar. Tukawa tumeshauriana katika mazingira kama hayo sijui imeishia wapi? Nimeona kimya, kimya mpaka nimekuja kustukizia magari yanakamatwa huku Bara. Halafu isitoshe *timing* yenyewe mtu kavizia mpaka Uchaguzi Mkuu umekwisha kwa sababu alijua wangeanza kulifanya kabla ya uchaguzi asingefanikiwa. Lakini sasa hivi tumaliza

uchaguzi ndiyo mtu anakuja kulifanya hili kwamba wananchi baada ya miaka mitatu watasahau.

Sasa tunafanya kazi vipi jamani. Kazi tunazifanya vizuri tuzifanye kwa uhakika. Juzi niliuliza swali mimi tarehe 13 Juni, 2006 kuhusiana na suala la mafuta ya ndege *Jet A-1.* Mimi niliuliza lile swali. Baadaye nikauliza swali la nyongeza hapa nikasema labda Serikali haina habari au vipi, kwa sababu naona watu madhubuti sana katika kufuatilia kodi lakini hili mbona wamelipa mgongo? Mafuta ya ndege yanayoingizwa nchini halafu yakawa *convited* kuwa mafuta ya taa kipindi hiki ambacho tumekuwa na matatizo ya umeme, tulikuwa hatutegemei kwamba mafuta ya taa yatumike sana. Lakini kiwango cha mafuta ya taa yaliyoletwa kwa mujibu wa takwimu tulizopewa na kiwango cha mafuta yaliyokuwa kabla ya hapo, sasa ndiyo hapo ninapouliza na kuingiwa na wasiwasi hivyo kwamba jamani Serikali kweli haioni au vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nalizungumza kwa sababu wamekuwa wanalilalamikia sana. Lakini imefika mahali inaonekana kwamba hawajui wamwambie nani wanavyosema watu sijui wamwandie Waziri hatujui. Lakini mimi nilisema hili nitali-*convey,* nitalizungumza hapa kinagaubaga tutasikilizana na nafikiri ujumbe huu utakuwa umeshafika. *(Makofi)*

Mimi nilitaka kulizungumza suala hili tu, kwa sababu hapo nilipokuwa nikiwauliza kule ofisini kwa kweli kama ningekuwa nimepata jawabu zuri, mimi nisingekuwa na haja ya kulizungumza hapa. Lakini najibiwa kama umeenda sokoni. Halafu isitoshe wale maofisa wa *TRA* kule waweze kuwajibu watu vizuri. Badala ya mtu anakuuliza *very politely,* badala yake anakuwa mkali. Sasa anakuwa mkali kitu gani? Toa maelezo ule ukali hata maana hauna, kama huna maelezo ukali haukusaidii. Toa maelezo yenye kufahamika kwamba suala hili liko hivi hivi. Lakini ulishaulizwa swali umeshaliona gumu tena unakuwa mkali unaanza kuwa mkali unataka kukunja ngumi. Sasa linahusiana na nini. Utapigana na watu wangapi? Kwa sababu kila atakayekuja atakuuliza hilo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda unakwenda nami nichukue muda huu uliobaki kwa kutoa pongezi. Naendelea kutoa pongezi. Mheshimiwa Waziri pamoja na hili Baraza ambalo liko mbele yetu. Hili Baraza madhubuti. Mheshimiwa Zakia Meghji naamini sana utendaji wako wa kazi isipokuwa awe macho. Kuna watu katika utendaji wako mzuri Mheshimiwa Waziri watajaribu kuchukua vumbi lile unalofagia ndani ya nyumba na kupeleka katika uvungu wa kapeti, kuwa macho na uwe mkali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kuwa macho uwe mkali, tunakuamini ni mtendaji mzuri wala huna matatizo. Haya yameanza kutokea huko nyuma, wewe umeyarithi tu kuwa macho, kuwa mkali. Hii hotuba uliyotusomea hapa ni nzuri sana na kwa kweli kama itatekelezeka kama ulivyosoma hapa umaskini kwa kiasi kikubwa sana utapungua Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwenye suala la mishahara. Lengo ni zuri sana, kweli mishahara ya wananchi imekuwa iko chini sana. Natoa pongezi sana kwenye suala la kuhifadhi mazingira, suala la matumizi ya makaa ya mawe pamoja na matumizi ya mafuta ya taa pamoja na gesi kuishushia kodi, nakupa pongezi sana. Natoa pongezi sana kwa Serikali kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura, kupitia Chama cha Mapinduzi, kwa sababu juzi juzi kuna gazeti lilisambazwa katika jimbo langu wakawapa *CUF*. Ni CCM. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kwamtipura, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia moja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi kwanza kabisa kwa niaba ya wapiga kura wangu ningependa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba mbili hizi zilizotolewa na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kwenda moja kwa moja katika eneo la elimu. Nianze kwa kutoa mfano wa ziara yangu niliyoifanya katika jimbo langu Lulindi kabla sijafika hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifanya mikutano 14 ya hadhara na Halmashauri Kuu za Kata. Nilipokuwa nikifanya mikutano hii nilikuwa na swali moja tu, kwa wananchi ambao ni wapiga kura wangu. Nalo ni hili lifuatalo, hapa tulipo ni wazazi wangapi wenye watoto wanaomaliza kidato cha nne mwaka huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha na inatia simanzi, kwa hesabu za haraka haraka mikutano hii ilikuwa haipungui watu 100. Mikutano 14 watu 1,400. Mikono niliyoipata yenye wazazi wenye watoto wanaomaliza kidato cha nne haizidi mitatu. Hii inaonyesha kwamba kiwango cha elimu katika Mkoa wa Mtwara, Jimbo la Lulindi, Wilaya ya Masasi, kiko chini sana. Tumewahamasisha kujenga shule za Sekondari kila Kata. Baadhi yao wamejenga. Kuna shule pale ya Lupaso, Kata ya Lipumburu. Kuna shule ya Namwombwe, Kata ya Mchauru, Shule ya Lulindi, Nanjota, Makong'onda, lakini wengine wako mbioni kujenga shule za sekondari. Lakini hizi nilizokutajia hazizidi walimu watatu na wengine shule nyingine ni mwalimu mmoja, mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ukizungumzia kuondoa umaskini huwezi kuuondoa katika mazingira haya ya elimu duni. Naomba basi katika Bajeti hii tuoneeni huruma watu wa Mkoa wa Mtwara. Wapelekwe walimu ili watoto wetu wasome kama wanavyosoma watoto wa maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Waziri Mkuu amefanya ziara katika Mkoa wa Lindi. Ameona hali halisi ya Mkoa ule na mimi namwomba hapa rasmi aende katika Mkoa wa Mtwara na aombe kupangiwa ratiba ya vijijini ndani kabisa kule akaone hali halisi.Watu hawakusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza kila siku elimu, elimu ni uti wa mgongo, kwetu sisi bado elimu haijawa uti wa mgongo katika maisha yetu. Hili lizingatiwe na litazamwe katika kiwango cha hali ya juu na Bajeti hii. Pelekeni walimu wakawafundishe vijana wetu katika Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie upande wa kilimo. Katika mkoa wa Mtwara, korosho ndiyo zao kubwa la biashara. Huwezi ukazungumza vinginevyo ukaeleweka kama huzungumzii korosho. Matatizo yafuatayo yanajitokeza katika zao la korosho. Bei haina uhakika mpaka leo hii. Mwaka jana wakulima wetu walihangaishwa, walitangaziwa bei ya korosho ni shilingi 600/=. Wafanyabiashara wakaacha kununua. Mikutano ikafanyika sasa unafika mahali unashindwa cha kuzungumza kwa wananchi. Kwa sababu mfanyabiashara amekataa kununua kwa bei iliyopangwa pamoja na Serikali. Unamwambia mkulima wa korosho apange utaratibu wake wa kuondoa umaskini, ataweza wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliitisha kikao cha wadau wa zao la korosho. Akaahidi kwamba Serikali itatenga shilingi bilioni 1 kwa ajili ya pembejeo. Hivi ninavyozungumza Bungeni hapa pembejeo hiyo haijafika na kama imefika, ni chache sana.

*(Hapa hakusikika kwa muda wa dakika mbili)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wapate korosho nyingi, wauze, waboreshe maisha yao na Serikali ipate kodi, iboreshe maisha ya Watanzania. Naomba sana, hivi ninavyozungumza wako redioni, wako kwenye televisheni, wanakisikiliza na kuangalia kilio hiki. *(Makofi)*

Narudia, naomba sana tena tutazameni kwa jicho la huruma watu wa Mikoa ya Kusini sisi maskini.Halmashauri zetu za Wilaya ndizo zinazofanya kazi na wananchi katika maeneo mbalimbali. Lakini Halmashauri hizi hazina uwezo hata kidogo.Tusidanganyane hapa, hiyo ruzuku wanayoipata haitoshi. Mfano, sisi kule kwetu mwaka 1990 tulipata mafuriko ya kutisha, miundombinu iliharibika, daraja hakuna. Maeneo ni makubwa, leo unasema Halmashauri zetu zitengeneze si kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawataweza hata kidogo, leo hii ukienda katika maeneo yale unakuta barabara zinatisha, hazipitiki. Mimi katika safari zangu za kwenda kuzungumza na wananchi maeneo mengi natembea kwa mguu. Magari hayapiti, nawauliza wale wenzangu kutoka hapa kwenda kule kilometa ngapi. Wanasema Mheshimiwa Mbunge, hapa ni kilometa tano, nawaambia twendeni. Twende kwa mguu, inasikitisha na kule kuna korosho nyingi. Kuna watu wengi, kuna mazao mengi kabisa. Mwaka huu tumelima karanga nyingi, tumelima choroko nyingi. Lakini watu wanakaa nazo majumbani, hawana kwa kuzipeleka. Barabara haipitiki. Kuna maeneo kama ya Mnavira kule, Makong'onda. Unakwenda Newala huko, kuna mchanga huwezi kuamini. Magari yanakwama pale kila siku, Mpindimbi, Mkundi, Mkululu, Lulindi, barabara hazipitiki, ni eneo zuri kwa kilimo. Jamani, tuoneeni huruma. Jengeni hizi barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaunga mkono kwa asilimia 100 Bajeti hii. Sina kipingamizi hata kidogo, lakini nawaombeni tuondoeni kwenye umaskini watu wa Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nizungumzie Bajeti hii. Kwanza kabisa ningependa kutoa pongezi kwa Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimpongeze Waziri Mkuu kwa kuchaguliwa na kuweza kufanya kazi nzuri sana wanazozifanya sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, niwapongeze Mawaziri wote waliochaguliwa na Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa ambao wamo humu ndani ya Bunge, kwa kazi nzuri zinazofanyika tunaungana nao pamoja na wenyewe lazima niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwanza naanza kujikita kabisa katika kuzungumzia suala zima la mapato yanayopatikana kutokana na Serikali yetu. Tuna uhakika kabisa kwamba asilimia kubwa ya Pato la Taifa linachangiwa na Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda ya Ziwa inachangia pato kubwa sana la Taifa katika Taifa letu hili. Lakini cha kushangaza unakuta kwamba Kanda ya Ziwa ndiyo imebaki maskini kuliko sehemu zingine zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nayazungumza haya tukiangalia katika nyanja mbalimbali. Tukiangalia kabisa kwamba Kanda ya Ziwa ndiyo Kanda ambayo ina madini mengi. Ina mifugo, kilimo kwa wingi, ndiyo kinachongia pato kubwa sana la Taifa letu. Lakini tusisahau hata uvuvi, kuna samaki, minofu inasafirishwa kwenda nje. Zote hizi zinaingiza Pato la Taifa. Sasa mgawanyo wake unapokuja unakuja tofauti. Mwaka jana nitoe mfano tu Mwanza, katika Pato la Taifa fungu la Maendeleo lilipata asilimia 12. Mwaka huu Mwanza imepewa asilimia 2 ya Pato la Taifa katika Fungu la Maendeleo.

Kwa hiyo, utakuta kwamba kupungua sasa hatujui ni kigezo kipi kilichotumika kuweza kupunguza asilimia zote hizo na kutokupelekewa fungu kubwa la maendeleo Kanda ya Ziwa inaendelea kuwa na umaskini mkubwa wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba yafuatayo, kwanza kabisa tunaomba kwa mwaka huu ruzuku inayotolewa kwa kilimo Kanda ya Ziwa na sisi tupewe. Kwa sababu kuna kawaida ruzuku hii inaelekezwa sehemu moja. Lakini mnatuambia kwamba tuzalishe pamba na pamba ifikie kilo 1,000 kwa heka moja. Tunazalisha kilo 300 kwa heka sasa uzalishaji huu utakuaje bila kupata vitu kama hivi. Tunaomba Serikali itupe ruzuku ya pamba. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kufanya hivyo, tutakuwa tunaendelea kuwa maskini ingawaje Taifa inazidi kuchukua Pato lake katika maeneo yale. Hilo nilikuwa naliomba sana katika awamu hii. Lakini lingine ambalo naliomba kilimo cha umwagiliaji, maji tunayo, ziwa lipo. Sasa kwa nini tuvukwe sisi ambao tuko karibu na Ziwa? Kwa mfano katika Wilaya ya Geita, tuna mabonde ambayo ni mazuri kabisa.Kuna bonde la Ibanda, Bonde la Lwezera Itobola kule, Kaboha, Isima. Yako mabonde mazuri ambayo wanaweza wakaanza kumwagilia na Serikali ikaweza kujinusuru katika janga la njaa ambalo limejitokeza sasa hivi. Naomba Serikali iweze kutupia macho Kanda ya Ziwa kuhamasisha ili na sisi tuweze kujinusuru katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakumbuka kabisa kwamba sasa hivi msingi wa maendeleo ambao tunaufuata ni Ilani ya Uchaguzi. Sura ya nne ya Ilani ya Uchaguzi, sehemu ya 44 ambayo inasema kwamba, nanukuu; "Katika kipindi cha miaka mitano 2005-2010 Serikali chini ya CCM itatekeleza yafuatayo katika upande wa ujenzi wa barabara." Kwa hiyo, katika ujenzi kuendelea kuimarisha mfuko wa barabara hiyo ambayo itatekelezwa katika miaka hii. Kukamilisha ukarabati wa barabara zote ambao unaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami ambao umekwishaanza katika barabara zifuatazo, kuna barabara nyingi lakini kuna barabara moja ambayo inatoka Usagara – Sengerema – Geita – Bwanga – Chato – mpaka Kaminyolwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi huu ungepaswa uanzie Usagara kwenda Chamnyolwa lakini ulianzia C kuja B na kwenda A. Sasa katika Bajeti hii barabara hii haipo. Sasa tukianza kuulizana kwamba hii barabara kwa nini imetolewa lakini imewekwa katika Ilani ya Uchaguzi na sisi kama wawakilishi wa maeneo yale tumejaribu kuwaelezea wananchi kwamba kuna lami inakuja katika maeneo haya na hicho ndio kichocheo cha kuweza kuleta maendeleo katika maeneo husika. *(Makofi)*

Sasa tunaponyimwa vitu kama hivi ni sawa sawa na kukata mishipa katika mwili wa binadamu usisafirishe damu. Hii ni damu ambayo inatembea, ni maendeleo. Sasa kukata au kunyimwa barabara ya kutoka Geita kwenda Usagara ina maana mnavunja maendeleo ya maeneo yote katika kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara ni kubwa, barabara hii ndiyo kiungo kikubwa katika Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Mara hata katika nchi jirani za Kenya na Uganda kuweza kuzungukia katika maeneo yote. Sasa mnapokiacha kipande kidogo kile Serikali ina maana gani. Naiomba Serikali iitupie macho kipande hiki kiweze kujengwa kwa kiwango cha lami kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kufanya hivyo, utakuta kwamba kuna uonezi mkubwa ambao unajitokeza kama nilivyosema kwamba Kanda ya Ziwa tunazalisha sana ni sawa sawa na ng'ombe kuanza kukamua maziwa yake lakini humlishi.

Sasa mfano huo uko katika eneo kama hili. Serikali inachukua mapato makubwa sana Kanda ya Ziwa lakini ukisema kwamba basi mlisheni huyo ng'ombe mnakataa.

Sasa naomba Serikali tujenge barabara hiyo kuweza kufumua maendeleo katika maeneo yanayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa kingine zaidi ambacho nilikuwa nakiomba licha ya kujenga barabara ile kuna vivuko ambavyo vimeharibika. Kivuko cha Kigongo - Busisi hakifanyi kazi, Kivuko cha Nyakalilo-Kome hakifanyi kazi, Kivuko cha Ukerewe hakifanyi kazi. Kwa hiyo, unakuta kwamba Ziwa Victoria vivuko vyake vyote vimeharibika. Ninaomba Serikali iangalie kwa sababu zote hizi zinaendana na mambo ya uchukuzi, mambo ya barabara, miundombinu. Naomba sana kitu hicho kifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja katika eneo lingine, tunasema kwamba umaskini umejikita Kanda ya Ziwa. Sasa hivi ukiangalia nitatoa mfano mmoja mdogo tu kwamba Wilaya ya Geita ni Wilaya mojawapo ambayo inazalisha sana katika nyanja mbalimbali. Kwanza, kuna dhahabu, kuna pamba, kuna mifugo, lakini mji wa Geita hauna maji na watu tumekaa muda mrefu. Mwaka 2004 niliuliza swali wakati Waziri Mkuu alikuwa Waziri wa Maji. Nikamwambia maji tutapata lini?Aliniahidi kwamba mwaka 2005 kuwa maji yatafika Geita. Lakini mpaka leo hii hakuna maji. Lakini nashukuru kwa sababu amepanda cheo ananisikia nina imani kabisa kwamba atauangalia mji wa Geita kwa macho mawili ili kuweza kupata maji na ninajua kabisa sasa hivi hata katika Bajeti hii unakuta kwamba mji wa Geita umewekewa pesa kidogo tu ya kwamba kutakuwa na upembezi yakinifu. Hiyo tumeenda nayo upembuzi yakinifu kwa muda wa miaka mitatu, milioni 5, milioni 5 upembuzi yakinifu. Hiyo milioni tano mpaka lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabisa mji wa Geita upewe kipaumbele, upate maji na ninajua kabisa Waziri wa Maji sasa hivi na yeye mji wake hauna maji. Sasa naomba mwaka huu basi akosee, alishe pua badala ya mdomo, asianzie kwenye mdomo akalisha pua. Nafikiri mtakuwa mmenielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa wengine katika kuzungumza wanasema kwamba aah, ukiwa katika jiko unapikapika lazima uonje onje ndiyo maana unakuta unapopata kacheo basi unaanzia kwako. Naomba hilo angalau wakubwa ambao mnachaguliwa kuwa Waheshimiwa Mawaziri, msianzie katika utaratibu huo, mtuangalie sisi kwanza halafu wewe ndiyo mwishoni. Hiyo ndiyo italeta maana zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyo ndiyo anakuwa Kamanda bora anaanza, wanakula askari yeye anakuwa wa mwisho. Nilikuwa hilo naliomba kabisa litekelezwe katika masuala hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la mafuta hasa katika migodi yetu. Nimesoma kitabu cha Bajeti wamesema kwamba watarekebisha kodi ambazo zinatozwa kwenye mafuta ambayo yako katika migodi. Naomba kabisa suala hili litekelezwe, hawa watu wa migodi si rafiki zetu, mara nyingi ni wafanyabiashara. Wamekuja hapa kufanya biashara. Lengo lao ni kupata faida wao na kila kunapokucha wao ripoti yao inatoa hasara tupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hata mkiwapa *favour* ya namna gani mpaka tutafikisha miaka hata 100 utakuta kwamba wanapata hasara tupu na ile asilimia 30 waliyosema kwamba mpaka tutakapopata faida hataweza kupata hapa Serikali yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, angalau kwa sababu wameonyesha kwamba hawatusaidii lolote basi kodi ambayo walikuwa wameondolewa kwenye mafuta wawekewe hiyo hiyo ili na wao waone kwamba uzalishaji unakuwa ni mgumu. Kwa sababu ukiwaambia watumie umeme wa Taifa hawakubali na kama hawakubali ina maana kwamba wanaonekana kwamba wanapata faida sana katika mafuta haya. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kabisa haya makampuni waanze kutoa kodi katika mafuta ili na wao uzalishaji uje gharama ambayo inajitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu yalikuwa ni machache ambayo nimeyazungumza lakini nisisite kuweza kumpongeza Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kuweza kuwakilisha hizi hotuba zao kwetu kwa wakati mzuri ambao tumeweza kuisikiliza na naunga hoja asilimia mia moja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. JOYCE N. MACHIMU:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema hadi leo hii tunapojadili Bajeti ya nchi yetu, tukiongozwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, wewe mwenyewe Naibu Spika. Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wote wanaotusikiliza kipindi hiki cha kujadili Bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Mheshimiwa Waziri Fedha, kwa maandalizi yao mazuri ya mipango ya nchi yetu, mipango endelevu na yenye matumaini kwa Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo na shukrani katika mapitio ya Bajeti ya mwaka 2005/2006 tumeona vikwazo vilivyojitokeza katika uzalishaji wa mazao yetu mojawapo yakiwa ni ukame, huduma duni za ugani na bei za mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti hii ya mwaka 2006/2007 naomba Serikali ijikite zaidi katika mambo yafuatayo, ili kuweza kuboresha maisha bora kwa kila Mtanzania kama tunavyotarajia katika Serikali yetu hii ya awamu ya nne.

Suala la kwanza Serikali itilie mkazo zaidi katika kilimo cha umwagiliaji, suala hilo ndilo litakuwa mkombozi wa Tanzania hasa katika Mikoa inayokumbwa na ukame wa mara kwa mara kama Mkoa wa Shinyanga ambao umekuwa na matatizo ya njaa mara kwa mara na inawezekana kabisa hata katika Bajeti hii Mkoa wa Shinyanga utakuwa ni mkoa utakaoleta adha kidogo kwa sababu mpaka sasa sehemu zingine mazao hayajakidhi ubora utakaoleta tija kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa huu wa Shinyanga pamoja na Wilaya zake zote nane una matatizo ya ukame wa mara kwa mara na kama mwenzangu aliyetangulia kuzungumza nilete kilio changu kwa Serikali kwamba ione umuhimu wa namna yake kuunusuru Mkoa huu kwa kufanya upembuzi yakinifu wa maeneo mengi zaidi katika Wilaya zote yatakapokuwa yameonekana kuwezekana ili waweze kuendelea na kilimo hicho cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili katika suala la kilimo kuna hili tatizo la ugani, Serikali pia iangalie namna ya kupata wataalam wengi ambao watapeleka elimu zaidi huko kijijini ili kuendeleza kilimo chetu na kuweza kuboresha tija ya mazao yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni kuhusu bei, pamoja na soko huria niombe Serikali iendeleze juhudi zake za kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili la bei hasa nikizingatia au nikiomba zaidi katika Mkoa wa Shinyanga ambao umekuwa na tatizo kubwa katika zao la pamba. Kama wenzangu walivyotangulia, zao la pamba nadhani ni zao linaloingiza mapato makubwa katika Taifa lakini limekuwa na msukosuko wa bei ambazo hazieleweki, basi nilikuwa naombi kama kuna uwezekano angalau bei kwa wakulima wa pamba wa Shinyanga na Mwanza basi isiwe inafikia chini ya shilingi 200/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la kilimo, suala la mwisho Serikali iangalie zaidi katika suala pembejeo, wenzangu waliotangulia wamezungumza habari ya pembejeo. Lakini nalileta hili suala la pembejeo kwa mkoa wa Shinyanga kwa masikitiko makubwa katika Wilaya moja ya Bariadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uchache wa pembejeo zinazopatikana na zinapatikana kwa muda usio muafaka wanakutwa wananchi kwa kuwa na elimu ndogo wanakuwa na hasira zisizo na msingi, hivyo wamepelekea ugawaji wa pembejeo hizi kupelekea kifo cha Mtendaji mmoja wa Kata ya Kilalo kwa hisia zisizokuwa na msingi kwamba ameficha idadi fulani ya dawa ya pamba. Naiomba Serikali suala hili ilifuatilie kwa karibu zaidi na iboreshe zaidi habari ya pembejeo katika Mikoa kama hii ambayo imekuwa na matatizo ya umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili naiomba Serikali itazame katika utawala bora iwe na ufuatiliaji wa karibu zaidi katika suala zima la watumishi ili tufikie katika malengo tunayoyataraji, wanatakiwa wawe wawazi zaidi katika shughuli zao wanapowahudumia wananchi. Ule urasimu wa hapa mara njoo kesho, mara fanya hivi unakosesha amani wananchi wetu kwa Serikali yake ambayo mipango yake ni mizuri kama leo hii tunavyoijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine usimamizi bora katika fedha zinazopelekwa katika Halmashauri zetu kuhusu miradi ya maendeleo, isimamiwe kwa ubora zaidi ili wale muchwa wakali walioko katika Halmashauri zetu basi Serikali ione namna ya kuwadhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne naiomba Serikali pamoja na mafungu machache iliyonayo ione namna ya kuharakisha mpango na kuboresha idadi kubwa zaidi

ya kupima mipaka ya vijiji, maeneo ya wakulima, kutenga maeneo ya ufugaji na katika maeneo haya ya vijiji mipaka itakapopatikana wananchi waweze kupata hati miliki na tuweze kuwafikisha pale ambapo tunasema kwamba mwananchi mmoja, mmoja wapate mikopo katika benki zetu ambayo itakuwa ni dhamana kubwa kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa suala hilo naomba Serikali hata kama haitakidhi kwenye Bajeti hii, basi Bajeti ijayo tujitahidi kuhakikisha kwamba angalau robo tatu y a nchi mipaka yake iwe imepimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tano, ni katika Serikali naiomba iangalie zaidi katika uwezeshaji wa wanawake. Wanawake wafanyabiashara wapo hata vijijini lakini kwa takwimu ambazo zimetolewa mfano wanawake 127 hadi wanawake 130 ambao walihudhuria uzoefu wa biashara katika maonesho ya Kitaifa ni wachache mno. Kwa hiyo, tunaomba elimu hii ipanuliwe zaidi hadi vijijini ambapo kuna wanawake wamechoka vibaya sana tunaomba tuwakomboe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la sita Serikali iangalie kuboresha miongozo na sheria katika Serikali za Mitaa kwa maana ya Halmashauri zetu kwa mfano katika sheria za manunuzi ya vifaa, naweza kutoa mfano mmoja kwamba katika wazabuni wanaokuwa katika Halmashauri mbalimbali wanaleta usumbufu kidogo kwa wananchi kwamba wao wanakuwa na uhuru zaidi wa kubadilisha bei kwa kisingizio kwamba mikataba yao inachukua muda mrefu kuweza kupata pesa. Lakini nikihisi katika kumbukumbu zangu kwamba sasa hivi Serikali inalipa vizuri wazabuni wetu, haicheleweshi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiki kisingizio kinatoka wapi na ukiwahoji Wakurugenzi wanadai kwamba hiyo ni miongozo ya Serikali, kama ndio hivyo Serikali ione namna ya kuboresha miongozo hiyo na kuwaweka wazi hawa wazabuni ili wasiendelee kuwanyanyasa wananchi hasa wanapokuwa katika ujenzi wa miradi ya maendeleo kwa mfano shule za sekondari ambazo zinaendelea sasa hivi nchini, mabati yanakuwa bei ya juu sana, *cement* na kadhalika. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo liboreshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, naomba Serikali iendelee kuwakubali wanawake katika uwakilishi wa maamuzi angalau kutoka katika asilimia zilizopo tuweze kufikia asilimia 50 na pili katika huko kutambua wanawake kwa mwaka huu wa Bajeti ya mwaka 2006/2007. Serikali katika kupandisha madaraja, watumishi mbalimbali katika Wizara na katika Mikoa na Halmashauri iwaangalie zaidi wanawake ili na sisi tuzidi kukidhi matarajio ya asilimia yetu ya 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa uwakilishi huo wa wanawake napenda nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wake wa wanawake katika uongozi, kwa mfano mama Zakia Meghji, Mawaziri na Manaibu Mawaziri Wanawake na wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika, imetia changamoto kubwa sana katika Taifa letu na ni shukrani za peke yake kwa hiyo, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwani ametupa heshima kubwa wanawake katika suala zima la kuwaenzi wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nawashukuru wanawake wa Mkoa wa Shinyanga ambao wameniwezesha leo hii kwa mara ya kwanza kujadili Bajeti ya Taifa la Tanzania. Ahsante.*(Makofi)*

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na vile vile napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa waliotoa hotuba zote mbili, Mheshimiwa mama Zakia Meghji, pamoja na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa. Katika hotuba yetu ya Waziri wa Fedha tulizungumzia masuala ya ushushaji wa ushuru wa mafuta ya taa, pamoja na kufuta kabisa mafuta *JET A-1* najua wenzangu wengi waliotangulia wamelizungumzia suala hili, lakini na mimi katika mchango wangu na kuishauri Serikali nitalizungumzia tofauti na walivyolizungumza wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti ya bei ya mafuta ya petroli na tofauti ya bei ya mafuta ya taa ni shilingi 263, tofauti ya mafuta taa na tofauti ya *diesel* ni shilingi 240. Pamoja na hotuba nzuri ya Waziri wa Fedha kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge msiwe na wasiwasi kwamba kimeundwa kitengo maalum cha kuhakikisha kwamba hamna udanganyifu wa aina yoyote. Lakini tukiangalia katika historia za mwanzo vitengo vingi sana vilishaanzishwa katika *TRA* vya kudhibiti masuala ya watu kutotafautisha mafuta ya taa na mafuta mengine na ndio maana kuna wakati ilifikia hatua bei ya mafuta ya taa na bei ya mafuta mengine ilikuwa sawa kwa ajili ya watu kutokwepa kodi. Kwa mfano, mtu analeta mafuta yake mwenyewe labda lita milioni 30, anashusha kupitia mita ya Serikali ambayo imewekwa pale, inakwenda kwenye *depot* yake mwenyewe na anayekaa pale kwenye mita ni hao hao tu ambao siku hadi siku pale hakai bosi wa *TRA* wanakaa watu wengi tu wa kawaida pamoja na kuwa wako *TRA*.

Tofauti ya lita milioni 30 ya petroli inaweza ikapitishwa katika mita hiyo lakini kwa kuandikwa kwamba yamekuja mafuta ya taa yakapitishwa pale kama mafuta ya taa lakini ni petroli. Kwa hapo tu Serikali itakuwa imeshakosa ushuru wa bilioni 10.9 kwa lita milioni 30, wakipitisha *diesel* kama mafuta ya taa na katika mita hiyo hiyo kwa sababu mita hiyo hata ukipitisha maji itasoma tu, hata ukipitisha maji itasoma. Kwa hiyo, akipitisha *diesel* lita milioni 30, lakini kwamba alishafanya mpango akaandika kwamba ni mafuta ya taa atakwepa bilioni 10.2, sasa sijui pale akae nani huyo ambaye akipewa bilioni mbili hawezi kukubali. *(Makofi)*

Kwa ushauri wangu, lazima tuige nchi zingine ambazo tunazo sambamba kama Kenya, Malawi, Kongo tunaweza tukaitumia *TIPER*, kwa sababu *TIPER* ina mitandao yote ya kupeleka mafuta katika *depot* zote za Dar es Salaam, kama *depot* ya Serikali mafuta yote yanayokuja nchi lazima yapitie katika *depot* ya Serikali, yakishapita katika *depot* ya Serikali panakuwa na ma-*tank* maalum kwamba hapa pana ma-*tank* ya petroli, pana ma-*tank* ya *kerosene*, pana ma-*tank* ya *diesel* na mafuta mengineyo. Sasa kama wewe ni *BP* au *TOTAL* au kampuni yoyote nyingine ile. Umeleta lita milioni 40 au 30 unataka mafuta yako labda milioni 10 unalipia ushuru wa lita milioni 10 kutoka *TIPER* inapampu kukupelekea kwenye *depot* yako, yale mengine yanaendelea kubaki pale. *(Makofi)*

Vile vile mafuta tunayoletewa Watanzania ni mafuta machafu machafu tu hayana ubora, kwa hiyo, yakipitia kwenye *depot* kama ile hata Serikali kudhibiti ubora inakuwa ni mwepesi zaidi na ndio maana magari mengi yanatoa moshi. Kwa hiyo Waheshimiwa wataendelea kupiga kelele mazingira, wakati mazingira wakati mazingira tunayachafua kwa vitu vya aina nyingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ushauri wangu tutumie *TIPER* kama *depot* ya Serikali na mafuta yote yanayokuja nchini yapitie pale kabla ya kwenda kwenye malipo mengine na *TIPER* lilishatengenezwa kipindi kile kwa ajili ya usafilishaji wa mafuta, sasa hivi inatumika kwa ajili ya uwekaji wa mafuta, kwa hiyo, ina bomba na ina mita zote za kwenda kwenye malipo yote ambayo yaliyoko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukianza sehemu kama Tanga, tunaweza tukatumia mita kwa sababu vimeli vinavyoshusha Tanga kutokana na kina cha bahari ni meli ndogo ndogo, kwa hiyo, udhibiti wake unaweza kuwa mwepesi lakini sio Dar es Salaam, Dar es Salaam haiwezekani hata imeshakuja vitengo tofauti vya *TRA*, wameshakuja wale sijui wale wazungu wanaitwa *SGS* wameshindwa, kila watu waliopita pale wameshindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii ni mbinu rahisi na huwezi ukamwambia bosi wa *TRA* nenda wewe ukaangalie pale, ukakae kwenye mita, haiwezekani watakao kaa hao hao, wataendelea kuiba, wataendelea kufukuzwa, watakaokuja wengine nao wataendelea kupata hela pale, mtu akipata bilioni mbili kwa meli moja ya bilioni 3 hata ukimfukuza kazi ana shinda gani, ana shida gani? Na huwezi, tutakuwa tunalaamu tu kwamba *TRA* bosi fulani bosi fulani, pale wanaokaa ni watu wa kawaida bosi hawezi kutoka pale akaenda kukaa pale, kwa hiyo mimi ushauri wangu ni huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa pili ni kuhusu habari ya kilimo, mimi mwenyewe ni mkulima pamoja na kuwa ni mfanyabiashara wa magari lakini ni mkulima mkubwa vilevile. Kilimo kimekuwa kinapewa majina mengi sana nchini hapa, uti wa mgongo, sijui ajira binafsi, lakini utekelezaji sifuri. Kwa mfano, sasa hivi tuna mkopo wa pembejeo, wakulima wanakaa vijijini na sana sana wanategemea benki ambazo ziko karibu na wao, unaenda kuwa *Exam Bank* wakopeshe mkulima, mtu atoke Dodoma hakuna tawi la *Exam* aende Dar es Salaam, anakwenda kule anaambiwa karatasi fulani hamna rudi ulikotoka, anatoka Singida anaenda Dar es Salaam, anaambiwa karatasi fulani hakuna kwa nini hii mikopo isihamie katika Benki za Wilaya *NMB* au *NBC*. *(Makofi)*

Sasa hapo tunawasaidia nini wakulima, na hata hao waliopata hii mikopo utakuta ni Mbunge, kama si Mbunge mtu yeyote tu mjanja mjanja wale walengwa hakuna. Sasa tunazungumza tunasema mkopo wa pembejeo mkulima ataamuka hii itakuwa ni hadithi ya miaka na miaka, miaka twende miaka rudi, hakuna atakayeamka.

Mimi kwangu Gairo, ni wakulima wanaofahamika katika Mkoa wa Morogoro, hata hii Dodoma ukisikia mahindi ya Dodoma, hakuna mahindi ya Dodoma ni mahindi ya Gairo tu. Hata soko la Kibaigwa pale hakuna mkulima Kibaigwa, wakulima wote ni wa Gairo. Lakini nenda kaulize pale kama kuna mtu keshawahi kupata mkopo wa aina

yoyote au hata msamaha wa kodi ya pembejeo sijui ruzuku chochote kile hakuna. Tunaisikia tu ruzuku katika hotuba, tunaiangalia tunaisoma lakini hatuioni, inakwenda labda mikoa mingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika hizi ruzuku iangalie na baadhi ya Mikoa nayo siyo ina- *base* katika baadhi ya Mikoa fulani tu. Basi kwa sababu ishaitwa *big four* yoyote huko huko. Sasa na sisi tutaingia lini tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha tatu na mwisho nataka kuchangia kuhusu habari ya madini. Madini tunakuwa tunazungumza kwamba yanachangia katika watu mia yanachangia mfanyakazi mmoja kutoa ajira, lakini lazima tukumbuke hata panya akitaka kuchimba lazima anuse kwanza halafu ndiyo anachimba.

Sasa hivi tunazo kampuni pale Kunduchi, Dar es Salaam ambayo mtu kabla hajachimba madini anakwenda pale katika ile kampuni Dar es Salaam anachukua wataalam, wanakuja kumtazamia pale eneo lake kwamba hapa yapo madini kiasi fulani kama ni dhahabu basi ipo dhahabu umbali kiasi fulani na tani fulani kwa hiyo ukiiingiza gharama ukichimba hapa utapata faida au acha usichimbe utapoteza pesa zako lakini ukiangalia katika hotuba hii nimezungumzia misamaha ya kodi katika makapumi makubwa kwamba wataweka uwiano wa kodi wanayotoa na mapato wanayozalisha makampuni kuwiana na mapato yaliyopatikana katika hayo makampuni na uzalishaji.

Sasa kwa Mtanzania au mchimbaji mdogo mdogo ambaye unataka kumuinua kimapato ili naye aongeze ajira itabidi kama ni msahama *(examption)* ni lazima umpe kwa kipindi fulani na Serikali kwa kupitia Wizara ya Madini iwasaidie kuwapatia wale wataalam ambao bado wanataka msahama wa kodi kwa hiyo, tuletee ripoti yako au tutakusaidia mtu aende akafanye pale uchunguzi kuonekana kwamba kama kweli pale yapo madini tutakusaidia ili uweze kuchimba lakini utakavyomwambia kwamba na yeye Mtanzania wa kawaida aanze kwanza kuzalisha halafu ndiyo umsamehe kodi hapo itakuwa ni kumuangusha tu na ataendelea kupiga sululu tu na hata amka hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Namwomba Mheshimiwa Hadidh Ali Tahir, atamalizia na Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti hizi mbili za Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Wizara ya Fedha na kama walivyoanza wenzangu kwa kupongeza basi mimi nawapongeza wote na itifaki nayo imezingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili nikiangalia kitabu cha Waziri wa Fedha ambacho mara nyingi nitakuwa nakiongelea hicho kwa kweli kitabu hiki kimekusanya

mambo mengi kama nilivyosema kina mwelekeo na ndiyo lengo la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwaondolea umaskini Watanzania kama Ilani na sera zao za Chama cha Mapinduzi zinavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la kwanza ambalo ningelipenda Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali yetu iliangalie kwa macho maangafu kwanza kwenye ukurasa wa 13 kuhusu Mifuko ya Uzeeni. Serikali imekuwa ikijitahidi kwa muda mrefu kuweza kuona kwamba wafanyakazi wa Tanzania wanapofika katika wakati wa kustaafu basi hali ya maisha yao inakuwa nzuri lakini acha kuwa nzuri lakini pia wanapata mafao yao kwa wakati unaotakiwa ili mfanyakazi yule aweze kujikimu katika muda wake wa maisha uliobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini namwomba sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwamba mkazo mkubwa hapa pamoja na wananchi wengine katika Wizara mbalimbali lakini kwa mtazamo wangu wafanyakazi waliomo katika vikosi vyetu Polisi na majeshi naomba Serikali itupie macho katika eneo hili ili wenzetu hawa wanapomaliza muda wao waweze kujikimu vizuri kwa sababu ni aibu askari wetu ambaye tulikuwa tunamtegemea katika kutulinda, yule ambaye alikuwa ana cheo cha *Major Left Hand Canal* anastaafu lakini unamkuta anarudi kukaa mlangoni kumlinda mtu ambaye amelala ndani ni aibu kwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mifano hai, nina mifano hai ya Meja wa Jeshi, *Left Hand Canal* wa jeshi kastaafu kwa sababu ya matatizo yaliyotokea katika kipengele hiki wengine wamekuwa wanafungua milango katika wakubwa fulani wao wanalinda usiku lakini hebu tujitazame basi hivi watu hawa kama kuna maadui wanataka kuwatumia kweli mtu huyu atashindikana kupatikana?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili ningeomba sana liangaliwe, wanajeshi na polisi wanapostaafu watafute jambo la kufanya ili waweze kuishi vizuri na badala yake kutokudhalilishwa katika sehemu mbalimbali. Kule Zanzibar kuna Meja mzima yupo mlangoni pale Bandarini pale anafungua milango, ni aibu haielekea, ni fedheha, sasa huku ningeomba sana kukaangaliwa vizuri ili basi wenzetu hawa wakaweza kujikimu katika maisha yao yaliyobakia kabla hawajaaga dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili nilikuwa nataka nizungumze ni kuhusu suala zima hapa la wananchi kupatiwa nyumba na kuishi vizuri pamoja na mikopo ya nyumba hili naliunga mkono lakini bado naiomba Serikali tena ibadilishe mfumo, badala ya kuwa Serikali inafanya biashara ya nyumba basi inajenge nyumba kuwapatia wananchi maisha mazuri waishi katika nyumba nzuri ambazo watanzania wote wanatarajia kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano upo hapa Dodoma nyumba za kisasa, nyumba za kisasa mimi huwa najiuliza kajengewa nani? Mfanyakazi wa kiwango kipi? Kwa sababu nyumba zile hivi sasa zinakodishwa kwa kodi ya shilingi laki moja na nusu (150,000/=) kwa mwezi anatakiwa akae nani? Kuna Wabunge wako humu wameshakimbia hawawezi, sasa Serikali inataka mfanyakazi akae mfanyakazi wa daraja

gani na mshahara wetu sisi sote tunaujua mishahara yetu wafanyakazi iko kiasi gani halafu tena Dodoma.

Sasa ni lazima tufanye kitu kwa mwelekeo tusifanye kwa sababu tunataka tuonekane tu tumefanya hapana, mimi ushauri wangu ni kwamba kama kweli tunataka tuwaweke wananchi wetu katika hali nzuri nyumba zile zisiwe zinatoleshwa kodi bali Serikali ifanye tathmini ya nyumba apewe mfanyakazi kwa tathmini ya nyumba ile na atakapomaliza deni la nyumba ile basi nyumba iwe yake, Serikali isifanye biashara tumesema Serikali inataka kujitoa katika biashara sasa isifanye biashara sasa ijenge halafu irudishe pesa zake katika kiwango chochote lakini katika kiwango ambacho mfanyakazi anaweza kukimudu. Hilo la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu tukiangalia katika luninga na tukisikiliza hotuba za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuna maneno anasema yafuatayo “Kwanza watumishi wa umma kwanza wanatakiwa wawe wanyenyekevu, pili wasiwe jeuri, tatu, wasipokee rushwa na nne wanatakiwa waheshimu taaluma waliyokuwa nayo.” Haya si maneno yangu haya ni maneno ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yanaendelea kutolewa katika *TVT* siku zote sasa haya yanatulenga sisi  Wabunge ambayo tumeajiriwa na Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliposimama hapa katika maelezo yake katika kitabu hiki kaisifu sana *TRA* sana, lakini nikimwangalia Mheshimiwa Waziri wa Fedha na ninavyomfahamu anajua kwamba kuna lugha kule Zanzibar kwamba: “Kizuri chochote hakikosi kasoro,” sasa ukisifu sana bila kutoa kasoro kuna hatari yake na unapoisifu *TRA* kwamba imefanya vizuri sana maneno manne haya ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete, yamejaa *TRA* na sisemi kwa kubahatisha maana Bungeni humu tuna kanuni humu unatakiwa mtu useme ambayo yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* kweli wamevuka lengo la 19.1, mimi nakubali na ninawapongeza lakini huu ulikuwa ni wajibu wao, huu ulikuwa ni wajibu wao na sijui wengine wamefika katika wajibu huu baada ya sisi wenyewe kuwafanyia tathmini ya kukusanya mapato yaliyochini ya uwezo wa *TRA* kwa sababu tulifanya hivyo *TRA* wamevuka malengo Mheshimiwa Waziri hebu wawekee sasa kiwango kingine katika miaka mitano ijayo utazame kama hawakuvuka. Tatizo tunashindwa kwenda kuitazama *TRA* iko vipi na uwezo wao ukoje na tunawataka akina nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* baadhi ya wafanyakazi si wanyenyekevu, si wanyenyekevu kabisa. Kunyenyekea maana yake ni kwamba ni mteja anapokuwa umtekelezee yale mambo ambayo yeye anataka katika hali nzuri, hivi umweke mtu pale *reception hotel* halafu kila ukienda wewe uso kakunja utakwenda mtu? Anatakiwa awe mnyenyekevu na ana bashasha na furaha. Huku hakuna unyenyekevu *TRA* kuna wafanyakazi baadhi yao ni jeuri mno, jeuri na hawajali shughuli zao za kazi hawaheshimu taaluma yao waliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Bunge lako hili kuna Wabunge walishakumbana na dhahama za *TRA* humu ndani, humu ndani ya Bunge hili kuna Mbunge kafika kuambiwa hili ulilolileta hapa sisi hatulifanyi wewe una Serikali yako na sisi tuna Serikali yetu, si mfanyakazi anayeheshimu kazi yake, si mfanyakazi aliyekuwa ananyenyekea watu narudia tena ndani ya Bunge lako basi Wabunge yalishawakumba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilichotaka kusema ni kwamba pamoja na mengine yote namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Serikali sisi tuna maneno tunasema, si kila kazi anapewa kila mtu, narudia tena Watanzania tumekubali kupeana kazi lakini si kila kazi anapewa kila mtu, hapana. Tuchague kazi ya kumpa mtu katika uwezo wake na yukoje ndiyo Tanzania itaelekea tunakotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni kwamba *TRA* hii Jamhuri ya Muungano hivi juzi kulikuwa na kikao baina ya Zanzibar na Tanzania Bara ndani ya Jamhuri ya Muungano kuondoa kero, *TRA* badala ya kuondoa kero wao wanaongeza kero, hizo tulizo nazo hatujamaliza bado wanatuletea nyingine. Mwenzangu kazungumza kwa ufupi sana pale, kero za gari za Zanzibar kuzuiwa kutembea Tanzania Bara linaudhi, ni unyanyasaji mkubwa unamnyanyasa Mtanzania ndani ya Jamhuri yake ya Muungano lakini huyu aliyetoa amri hii ni nani maana Bunge ndiyo hili. Mimi baadaye Waziri aje kuniambia na wewe ulikuwapo hivi miaka mitano iliyopita Bunge hili lilipitisha lini sheria ya kwamba gari za Zanzibar zisitembee Tanzania Bara nije niambiwe hapa nitakuwa mgumu sana kwa hili kama Waziri hajaniambia tarehe fulani Bunge letu la Jamhuri lilipitisha gari za Zanzibari zisitembee Tanzania Bara, huu ni udhalilishaji tena ni unyanyasaji mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana kuna wenzetu humu nembo ya Tanzania hawataki kuiona huku katika Tanzania Bara maana ikipita gari pale ZNZ Dar es Salaam kaja mgeni ataulizwa ZNZ maana yake nini? Unaambiwa ile gari imetoka Zanzibar, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania maana yake ni Zanzibar na Tanzania Bara, ndivyo ilivyosema hii Katiba, Katiba hii imesema hivyo na Katiba hii imesema ndani ya Jamhuri kutakuwa na Serikali mbili, kutakuwa na Serikali ya Zanzibar na kutakuwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kutakuwa na Rais wa Zanzibar na kutakuwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Katiba hii haijasema Serikali moja kubwa moja ndogo haikusema humu, Serikali zote ni sawasawa na zitakuwa na mamlaka maalum na rasmi ndiyo ilivyosema Jamhuri hii sasa huyu mwenzetu anayekataza gari za Zanzibar zisitembee huku Tanzania Bara anatupeleka wapi na nani? Kapewa amri na nani? Hivi zile zinazotembea kule Zanzibar atokeze mwendawazimu mmoja na zirudishe tunakwenda wapi? Sasa ndiyo nikasema Mheshimiwa Waziri Mkuu namuomba sana si kila kazi atapewa kila mtu, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho ni kwamba ndani ya Wizara zetu tuangalie basi ndiyo kila kazi asipewe kila mtu, tuwe waangalifu nina wasiwasi na siasa inacheza katika Wizara zetu, nina wasiwasi sana. Wasiwasi wangu umekuja wapi?

Mheshimiwa Waziri wa Mipango kanyanyuka hapa ndiye wa mwanzo kutoa Bajeti yake kuna watu wanamchezeachezea na nilimwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu hii ninayotaka kuzungumza sasa hivi rafiki zangu itawakera kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu hiki cha Mipango hebu twende basi katika hisia za kisiasa, hiki kitabu hiki cha Wizara ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kitawekwa bendera hii? Hii bendera ya nani? Tena ubaya wenyewe hii bendera imewekwa *front page* maana rangi hii mimi sijui maana yake nini katika kitabu hiki mimi sijafahamu halafu yaliyoandikwa hapa hayasomeki hata ukisoma hata ukisoma lakini aliyetengeneza kitabu hiki Mheshimiwa Waziri kaibiwa hajui. Lengo lake lilikuwa kije hapa na rafiki zangu wafurahi na wamefurahi kweli kweli kuona bendera hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuwe makini kidogo katika kufanya mambo yetu ndani ya Wizara zetu kuna mambo tumekubali wenyewe kuwa na vyama vingi lakini safari hii miaka mitano hii tuliyokuwa nayo chama kinachoongoza ni Chama cha Mapinduzi na kitaendelea kuongoza Chama cha Mapinduzi sasa wasije watu wakatuchezea katika mambo yetu ndani ya Wizara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Kicheko)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimwia Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami ya mwisho jioni ili nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu, kama ilivyo ada napenda nianze na kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kura nyingi alizozipata na nadhani ni hekima ya Mungu iliyoweka jicho lake tukamwona Watanzania wote. Nimpongeze vile vile Waziri Mkuu Ndugu yetu Mheshimiwa Edward Lowassa ambaye naye Mungu alimwongoza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, akamwona na Wabunge tukaridhia uchaguzi wake, nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Spika wetu naye kwa uchaguzi uliopita alipita vizuri sana, ni hekima na busara iliyoongoza Wabunge kumchagua na wao walipewa nguvu na Mwenyezi Mungu na nikupongeze wewe Naibu Spika kwa kupita bila kupingwa ukiwa nadhani ni Naibu Spika Mwanamke wa kwanza katika Bunge hili, hongera sana Mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha kwa kazi nzuri aliyoifanya na niwapongeze Wabunge wenzangu hili jengo kuingia nadhani ni mamlaka ya Mungu vile vile iliyoongoza wananchi kwa kutuchagua. Warumi 15 na katika Misahafu ya *Quran* tukufu inasema mamlaka hutoka kwa Mungu kwa hiyo, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kutupa nafasi hii, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze waliotangulia kuzungumza, wote wamejaribu kuzungumza maneno mazuri ya busara na Wapinzani nao niwapongeze kwa hotuba nzuri walizotoa, wamejaribu kutueleza na kutuelekeza na kutuunga mkono, nashukuru sana, wamesema mengine ambayo ni ya nyongeza nyongeza ikaonekana

mengine ni uongo lakini wamesema sema. Labda nisemee tu kidogo suala la ndege. Nadhani sasa hivi liwe ni kama jambo limepitwa na wakati kwa sababu ukizungumzia suala la ndege wakati wewe hukukataa kuingia kwenye jengo jipya zuri na ulikuwa na jengo lingine ni *contradiction* na mimi nasema lazima tuelewe kwamba ulimwengu unakimbia na tunatakiwa twende na vyombo ambavyo vinakwenda na hali halisi hata katika jengo letu unaweza kusema limekamilika lakini kuna vitu vingine vinahitajika.

Leo mimi nimesima karibu mara kumi lakini Spika hakuniona lakini bado kunahitajika chombo hapa cha kubonyeza Spika hakuna cha kuanza kuangalia angalia, akutafute, anaangalia tu jina la mtu lililotangulia ndiyo linaandikwa na mengine zinakuwa *negative* anasema ni Kabuzi anazungumza. Kwa hiyo, vitu kama hivi ni sayansi inabadilika, hata kompyuta sasa hivi tunazozitumia ambazo tumezitumia mwaka jana sasa hivi zinakuja kompyuta mpya ambazo ni lazima tuzitumie na tukubali katika hali hiyo. Sasa mtu anaposimama akasema kwamba ndege ya Rais sijui tulitumia hela nyingi, mimi nashangaa kwa sababu zile ndege za zamani ni za kutoka miaka ya 1960 mpaka 1970 na ndege hii mimi bahati nzuri mimi wiki iliyopita nilikuwa naongea na Rubani wa ndege hiyo Mhaiki nikamuuliza kuna tofauti gani kati ya zile ndege akasema ndege hii sasa hivi tunaweza kutua sehemu nyingi za ulimwengu.

Mimi mwaka juzi nilikuwa kwenye Tume ya Madini nikaenda Muslewhile. Muslewhile tulifika mahali tunatua kwenye uwanja hatuuoni lakini nilianza kusali nilikuwa na jamaa mmoja nyuma yao wa Ofisi ya Waziri Mkuu, walikuwa wananiona nasali mimi naona sasa tunakwenda wapi mbona muda wa kutua umefika lakini hatuoni eneo lakini akatua salama.

Juzi tulipokuwa tunatoka Mwanza kuja Dar es Salaama tumezunguka pale kwa *Boeng* tena ulikuwa unaweza kuona chini walikuwa wanasema hali ya hewa mbaya, hali ya matatizo ni mbaya tukazunguka karibu mara nne ndiyo tukatua ndizo ndege tulizonazo. Sasa mtu anasema tuendelee na hiyo kwa Rais wetu azungukezunguke huko maana yake akienda Muslewhile, Canada hawezi kupanda ndege yake lakini ndege hii ni kwmba mimi nilimwuliza ni kwamba anapaa juu, anapotea halafu wanakwenda wanashtukia kama wanakwenda Australia wanatua waa!

Sasa wewe kwa kufikiria ukale wako bado unafikiria kwamba Rais wetu ambaye ni mtu mmoja nchi nzima tumemchagua aende na ndege ya *Boeng*, akienda Nairobi abadilishe apande *Kenya Airways*, mara tairi wakati fulani ziwe na wasiwasi, kama anazunguka hapa nchini anaweza akaitumia lakini kuna sehemu nyingine vyombo na ndege ambazo zinatumika wanaangalia vyombo hakuna tena kuchungulia dirishani namna hiyo hakuna mnakwenda mnatua. Sasa ndugu zangu mnakuwa wapi? *The world is changing very fast* basi tuanze na mtu mmoja yule apate ndege ya uhakika na tujipongeze kwa hilo la kuwa na ndege mpya.

Ndugu zangu leo tupo hapa tunazungumzia mambo mazito ya Bajeti, nilikuwa najaribu kuangalia Bajeti karibu Wizara mbalimbali najaribu kujumlisha kila Wizara nadhani kuna haja ya kuangalia labda Waziri Mkuu tumwombe sijui kama kuna chombo bahati mbaya sielewi kwenye *Cabinet* wanafanyaje kuangalia kama *resourses* hii

kasungura kadogo haka namna ya kukagawa hakagongani sehemu moja au sehemu mbili sehemu nyingine zinakachwa bila kupata mnofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia baadhi ya Wizara nilianza na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, nimeangalia Bajeti yao *critically* nikaangalia jinsi walivyoweka fedha, nikaangalia imekwenda Arusha ikateremka, Manyara tulikuwa tunaiunganisha lakini Manyara sasa hivi iko pembeni hakuna kitu ikateremka Arusha, ikaenda Dar es Salaam ikateremeka sana ikaja Morogoro ikateremka ikaja na Mbeya ikateremka kidogo halafu nikaona nikawa najaribu nikaona maneno waliyozungumza kwa nadharia kwamba wanaweka na Chuo Kikuu Dodoma nikaona angalau wanakujakuja lakini nikaanza kujiuliza je wametumia *criteria* gani kuweka Chuo Kikuu Dodoma? Wameangalia umbali? Au wameangalia lini?

Je, au ni *centre* ni nia ya kuiendeleza Dodoma? Maana mimi mawazo yangu kuendeleza Dodoma ni ku-*open* njia hizo alizozungumza Mheshimiwa Omar Kwaangw', Simanjiro kwenda Iringa, Dodoma kwenda Mwanza. Lakini nikiangalia chuo cha watu elfu arobaini je, Dodoma bado ni katikati? Kwa sababu kama vitu vyote vipo Dar es Salaam unaweka hapa Dodoma, kwani Dodoma si katikati tena, kitu cha wanafunzi elfu arobaini maana yake ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama manne hivi unayajenga hapa kama vile unajenga *a University Town* hapa.

Kwa nini usijenge watu elfu kumi na watu wengine ukawapeleka Shinyanga, Tabora hata Singida au Mara unaweka tu hapa sehemu nyingine zikawa *off compass* nikamaliza hiyo Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikaangalia Wizara ya Afya nikaangalia tena bahati nzuri wao walituhalisia wakatupa na ramani nikaangalia jinsi mgawanyo ulivyo, wao wana sera kwamba sasa hivi watakarabati vituo vya afya vilivyopo kupitia *Basket Fund*, tukarabati zahanati zilizopo na hospitali zilizopo lakini ukiangalia angalia ramani ya waliyotupa ya mfuko wa afya au bima ya afya ilivyo utaona sehemu nyingine hazina hizo hospitali nzuri, hakuna. Nikaangalia Kagera nikiangalia hospitali ya Serikali washukuru Mungu wana hospitali za mission wana hospitali moja tu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikaangalia Mkoa wa Mbeya nikaangalia Tukuyu na Mbeya kuna nafuu na Kyela lakini wale wenzangu kama ni Bima ya Afya ni shida sasa watakarabati hospitali zipi? Nikaenda Mwanza nikaona kuna *Bugando Mission* ilitusaidia na sehemu nyingine lakini nikaenda kuangalia sehemu zenye miundombinu kuna vitu vingi nikajiuliza mh! Huu mgao vipi? Nikaenda kwenye miundombinu nikaanza kuangalia ile Bajeti nimeangalia kwa kweli nikaona kuna dalili ya hatari nikaanza kujiuliza sasa kasungura wanasema ni kadogo mbona inaonekana kuna sehemu nyingine kuna wengine wanakula figo, maini na moyo halafu wengine wanapata mapaja matamu hata wengine wanapata mabawa na wengine tunapata kwato ni nini hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kweli kuna haja ya kuangalia na kufanya *reconciliation* ya *budget* kwamba inakwenda mahali pote. Kuna barabara za aina nne, kuna *village roads, district roads* na *regional roads* na *trank roads*,

inasikitisha unapokuta *district road* au *village road* inawekewa lami wakati *trank road* bado ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilifikia mahali nikawa sielewi, nikashindwa kuendelea kupiga mahesabu nilikuwa naendelea na Wizara nyingine nikashindwa kupiga mahesabu nikaona mh! kitu gani hiki? Nilipoangalia nikawa naangalia barabara ya Usagala - Chamunyorwa iko kipande, Mheshimiwa Ernest Mabina amezungumza hapa kweli inasikitisha mpaka nikaanza kurejea maneno ya mtu mmoja aliyesema ninyi mtaendelea kuwa maskini tu. Barabara ya Usagala - Chamunyorwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM imezungumzwa Mheshimiwa Rais aliyepita alikuja Katoro ikiwa ni katikati akaunganisha Wakuu wa Mikoa wawili Mheshimiwa Daniel Ole Njoolay na mwingine wa Kagera sijui anaitwa nani, walikuja pale na viongozi wakafika pale wa Kitaifa pamoja na wazungu wa kutengeneza mimi nikiwa nasikia kwamba ni kauli wameitwa pale katikati Katoro na mpaka leo msingi upo Usagala - Chamunyorwa sasa leo kipande cha Geita - Usagala hakuna kitu Mungu wangu mimi sielewi, Mheshimiwa Waziri Mkuu sielewi, sielewi hata basi mheshimuni Mheshimiwa Rais aliyestaaafu, aliyetamka maneno kwamba barabara itatengenezwa kama hamtaki basi mheshimuni Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliyefika Mwanza akasimama katika kundi la watu akasema barabara hiyo itatengenezwa kwa hivyo imeshaanza kutengenezwa sasa leo hakuna kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu katika hili basi kama ni mama ninyi nyote ni mama yetu Meshimiwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Zakia meghji, wewe ni mwanamke, ni mama unaelewa uchungu, hatutarajii wewe utageuka kuwa mama wa kambo, wengine wapate vipapatio na wengine kwato na wengine wapate minofu. Kwa kweli barabara imetuuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu amezungumza si vizuri kutangulia lakini ni vizuri niweke mkazo, Geita upande wa Kaskazini na upande wa Magharibi umezungukwa na Ziwa Victoria na Geita ina mgodi wa dhahabu mkubwa na upande mwingine kuna mgodi mkubwa wa dhahabu *KMCL* ambao una *mine underground* upande wa Geita na sehemu kubwa leseni ya kwanza ilikuwa ni ya Butobela iko katika Kijiji cha Geita, pale kuna mgodi mwingine unawekwa Nyarubusu wa dhahabu. Sasa angalia hali ya watu wa Geita, maji hakuna, inalima sana pamba mpaka sasa hivi wakulima wa Geita hawajalipwa baadhi na wafanyabiashara wa pamba, Geita ina ng’ombe lakini Geita haina hata tone la bomba la maji mnashangaa nini kusikia Geita kuwa ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli inatia uchungu, umeme ulioletwa Geita ni umeme butu kama vile kutukomesha ukifika ukiwasha ni giza huwezi kupanuka sasa basi kama haiwezekani kuleta umeme ule tumieni ule wa *KMCL* unaokwenda Bukombe upitie kwenye vijiji. Naomba na watu wa madini wafanye biashara basi Wizara ya Nishati na Madini unapopeleka umeme Bukombe fikiria kupitisha njia ambayo mimi nimekuwa nikiwashauri fikiria kupitisha njia ambayo itafanya biashara kama unatoa umeme *KMCL* unapitisha Bukoli kuna *ginery* kuna wachimbaji unapeleka Nyarugusu unapeleka Ruamgasa unakwenda Katoro ambayo ni sawasawa na Mji wa Geita vilevile kisha

unakwenda Bukombe watu wanafanya biashara siyo unawalazimisha watu kulala saa 10 waende kulala wanafanya nini waende kuzaa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale sasa hivi lami ikipita watu watakesha wanafanya biashara zao na kwenye dhahabu *actually* kama utapeleka umeme kule hata wale wachimbaji wa dhahabu watafanya biashara kwa sababu wanahitaji umeme sasa mnapeleka Bukombe kupitia porini sasa mmefanya nini mawaya yale hayana faida njiani kuna nguzo, wananchi wakiyachoma moto mtasemaje? Kweli tuwe nafikiri na mipango ya kuelewa. Mchumi wenu afikirie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu anahusika ndiye anahusika anatugawia mgawo hapa ndiye anagawa mambo hapa. Namwomba Waziri Mkuu hebu kaliangalieni upya hili suala la barabara ya Geita inawezekana wengine wanafikiri mengine yanayozungumzwa kuwa Geita ni maskini, ni uongo, ni ukweli kama huna maji, umeme, pembejeo na barabara, lazima uwe maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja lakini naomba ulifikirie hilo la barabara ya Geita. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimwia Wabunge, dakika zilizobaki ni chache mno kwa kuweza kumpa msemaji mwingine lakini naomba niwashukuru kwa mkutano mzuri tuliokuwa nao siku hii ya leo na hivi sasa nakisitisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01.39 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano tarehe 20 Juni, 2006 saa 03.00 asubuhi)*